

KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO • OKTOBA 2019

# Lahona



**Watoto Wanaokabiliwa  
na Ponografia—Jinsi  
Upendo Unavyoweza  
Kusaidia, ukurasa wa 36**

Ubayana wa Lenzi ya Injili,  
ukurasa wa 12

Njia 5 Ambazo Kwazo Yesu  
Aliwalinda Watoto,  
ukurasa wa 18

Kusherehekea Miaka 100  
ya Baraka za Hekalu katika  
Pasifiki, ukurasa wa 28

KANISA  
LIKOKO  
HAPA

# Antananarivo **Madagask**



# a



PCHA KUTOKA GETTY IMAGES

Hizi ni kweli chache kuhusu Madagaska na kanisa huko:



Makabila ya asili  
katika kisiwa

Ushawishi mkubwa  
wa kitamaduni:  
Kipolinisiani, Kiarabu,  
Kiasia, Kiafrika, na  
Kifaransa

5



Watu milioni  
ndani ya  
Madagaska

Lugha rasmi:  
Kimalagasi na  
Kifaransa

2



Waumini wa  
Kanisa

40

Mikusanyiko



**1986** Muumini wa kwanza wa  
Kimalagasi alibatizwa, huko  
Bordeaux, Ufaransa

**1990** Watu watano walibatizwa na  
kuthibitishwa

**1998** Misheni ya kwanza iliundwa

**2000** Kigingi cha kwanza  
kiliundwa



# Yesu Anawapenda Watoto Wetu

**N**inatumia muda mwingu kuwfikiria watoto. Ninaswapenda watoto katika mduara wangu wa familia na marafiki. Kwa kuongezea, kazi yangu kwenye majarida ya Kanisa inahusisha kutengeneza na kuhariri kurasa kwa ajili ya watoto wote ulimwenguni. Lakini miaka kadhaa iliyopita, nilitambua kwamba sikuwahi kujifunza kile maandiko matakatifu yalichofundisha kuhusu watoto. Hivyo niliamua kusoma Agano Jipya na Kitabu cha Mormoni na kutoa umakini wa ziada kwenye kile nilichowea kujifunza kuhusu kundi hili maalumu.

lilikuwa ni zoezi la kubadili maisha! Kati ya kweli nydingi nilizogundua, moja yenye thamani kubwa ilikuwa ni ongezeko la uelewa wa kiasi gani Yesu anawajali watoto. Aliwahudumia watoto kama kundi maalumu, aliwatenga kutoka kwa wengine, tena na tena. Je, ni kwa jinsi gani sisi tunaweza kufuata mfano Wake?

Makala yangu kwenye ukurasa wa 18 inashiriki baadhi ya masomo niliyopata kutoka kwenye uzoefu huo wa kujifunza maandiko, yakiunganishwa na mawazo na mchango kutoka kwa wataalamu kadhaa katika eneo la kuzuia unyanyasaji.

Watoto wana thamani kubwa. Natumaini tunaweza kushirikiana kuwalinda na kuwawezesha, kuwatendea kama ambavyo Yesu angewatendea!

Kwa upendo,  
Marissa Widdison



**Baraka za Mtazamo wa Injili**  
*Na Mzee Gary E. Stevenson*

12



**Hekalu la Laie Hawaii: Karne ya Kukusanyika**

*Na Clinton D. na Angela R. Christensen*

28



**Kuwa au Kuwahi Kuwa:**  
*Hilo Ndilo Swalı*  
*Na Mzee Joni L. Koch*

24



**Kuzungumzia Ponografia:**  
*Linda, Itikia, na Ponya*  
*Na Joy D. Jones*

36



# Yaliyomo

## 5 Kuwalinda watoto kutokana na Ponografia

### 6 Taswira za Imani

Wilson Di Paula—San José, Uruguay

Wakati Di Paula alipopata ajali ya pikipiki na kisha mke wake kufariki punde baadaye, hakujua nini cha kufanya. Lakini injili ilitoa majibu.

### 8 Kanuni za Kuhudumu:

Je, Unakosa Sehemu Hii Muhimu ya Kuhudumu?

Hatupaswi tu "kulia na wale wanaolia" bali pia "kufurahi na wale wanaofurahi." Hapa kuna njia nne ambazo unaweza kufanya hivyo.

## 12 Baraka za Mtazamo wa Injili

Na Mzee Gary E. Stevenson

Tunapoendeleza usawa wa kiroho, tutakuwa na mtazamo bora wa injili.

## 18 Kuwalinda Watoto

Na Marissa Widdison

Yesu Kristo aliwapenda na kuwalinda Watoto. Ni kwa jinsi gani unaweza kufuata mfano Wake?

## 24 Kuwa au Kuwahi Kuwa: Hilo Ndilo Swalı

Na Mzee Joni L. Koch

Ni rahisi kuhukumu wengine, lakini lazima tuwe makini kuhukumu kwa haki na kuwaona wengine jinsi Mungu anavyowaona.

## 28 Hekalu la Laie Hawaii: Karne ya Kukusanyika

Na Clinton D. na Angela R. Christensen

Kwa miaka 100, hekalu katika Hawaii limewaruhusu Watakatifu kote katika Pasifiki kupokea baraka za hekalu.

## 32 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwisho:

Akina dada wawili wanaongozwa kuhudumu; ujumbe wa wamisionari ulileta tofauti; askofu anaamua kile atakachofanya kwa malipo yake ya ziada; barua inasaidia kurekebisha mahusiano yaliyoharibika.

## 36 Kuzungumzia Ponografia: Linda, Itikia, na Ponya

Na Joy D. Jones

Watoto wanaathiriwa na kuachwa kwenye ponografia, lakini upendo wako unaweza kuwasaidia kuepuka na kushinda ushawishi wake hatari.

 Kupitia kwa Haraka

### Juu ya Jalada

Picha kutoka Getty Images, imetumika kwa malengo ya kielelezo, imeandalowi kwa mtindo




# Sehemu

## Vijana Wakubwa

42

Mwezi huu unazungumzia **nini cha kufanya** ikiwa **una miadi na mtu anayehangai-ka na ponografia** na kushiriki **hadithi za matumaini** kutoka kwa wengine ambaao wamekumbana na ponografia katika mahusiano yao ya miadi.



## Vijana

50

Kile inachomaanisha kuwa **rafiki wa kweli**, jinsi kijana mmoja **anavyoshiriki injili**, na kukumbuka jiwe kuu la pembedi la Kanisa.



## Watoto

### Rafiki

Gundua **jinsi ya kuwapenda wengine** kama Yesu anavyowapenda. Sala humsaidia Prodi wakati anapoingiwa na woga. Florence anakuwa muu-guzi. Unaweza **kuijandaa kwa ajili ya hekalu**.



## MAKALA ZENYE HABARI MAALUMU ZA-KIDIJITALI PEKEE



### Nilikuwa Nimepambana Kushinda Ponografia. Kwa nini Yeye Hakufanya hivyo?

*Jina limefichwa*

Kijana kutoka Guatemala anashiriki uzoefu wake wa kumwamini Bwana katika kufanya uamuzi mgumu.



### Jinsi Nilivyojifunza Kujibu Wakati Mtu Anapokiri Wanapambana na Ponografia

*Jina limefichwa*

Kujua kuhusu matumizi ya mtu ya ponografia kunaweza kusababisha aina zote za hisia, lakini kijana huyu alimtegemea Mwokozi ili kujua jinsi ya kujibu kwa upendo.



### Kusonga Mbele baada ya Kujuu juu ya Matumizi ya Ponografia ya Mchumba Wangu

*Jina limefichwa*

Kijana huko Tahiti anashiriki utambuzi wake juu ya jinsi ponografia ilivyoathiri mahusiano yake.

### OKTOBA 2019 VOL. 6 NO. 2 LIAHONA 18610 743

Gazeti la Kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

**Uraisi wa Kwanza:** Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, Henry B. Eyring

**Akidi ya Mitume Kumi na Wawili:**

M. Russell Ballard, Jeffrey R. Holland, Dieter F. Uchtdorf, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd Christofferson, Neil L. Andersen, Ronald A. Rasband, Gary E. Stevenson, Dale G. Renlund, Gerrit W. Gong, Ulisses Soares

**Mhariri:** Randy D. Funk

**Washauri:** Becky Craven, Sharon Eubank, Cristina B. Franco, Walter F. González, Larry S. Kacher, Adrián Ochoa, Michael T. Ringwood, Vern P. Stanfill

**Mkurugenzi Mtendaji:** Richard I. Heaton

**Mkurugenzi wa Magazeti ya Kanisa:** Allan R. Loyborg

**Meneja wa Biashara:** Garff Cannon

**Mhariri Mtendaji:** Adam C. Olson

**Mhariri Mtendaji Msaidizi:** Ryan Carr

**Mchapishaji Msaidizi:** Camila Castrillón

**Kuandika na kuhariri:** David Dickson, David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Garrett H. Garff, Jon Ryan Jensen, Charlotte Larcabal, Michael R. Morris, Eric B. Murdock, Sally Johnson Odekirik, Joshua J. Perkey, Jan Pinborough, Richard M. Romney, Mindy Selu, Lori Fuller Sosa, Marissa Widdison

**Mkurugenzi Mtendaji Sanaa:** J. Scott Krudsen

**Mkurugenzi wa Sanaa:** Tadd R. Peterson

**Usanifu:** Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, Mandie Bentley, C. Kimball Bott, Thomas Child, Joshua Dennis, David Green, Colleen Hinckley, Eric P. Johnsen, Susan Lofgren, Scott M. Mooy, Emily Cheecko Remington, Mark W. Robison, K. Nicole Walkenhorst

**Mratibu wa Haki Milliki:** Collette Nebeker Aune

**Meneja wa Uzalishaji:** Jane Ann Peters

**Uzalishaji:** Ira Glen Adair, Julie Burdett, Thomas G. Cronin, Bryan W. Gygi, Ginny J. Nilson, Marriissa M. Smith

**Kabla ya Chapa:** Joshua Dennis, Ammon Harris

**Mkurugenzi wa Uchapishaji:** Steven T. Lewis

**Mkurugenzi wa Usambazaji:** Nelson Gonzalez

Kwa usajili na bei nje ya Marekani na Kanada, nenda kwene store.lds.org au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa katika eneo lako ama kiongozi wa katau tawi.

**Wasilisha miswada na maswali katika Liahona.lds.org:** na barua pepe liahona@ldschurch.org; ama kwa barua *Liahona*, Rm. 2420, 50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

*Liahona* (neni katika Kitabu cha Mormoni linaloamnia "dira" ama "kielekezi") imechapishwa katika Kialbeni, Kiarmeni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisabuano, Kichina, Kichina (kilichorahisishwa), Kikroesha, Kicheki, Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kifiji, Kifinishi, Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kiangaria, Kialislandi, Kiindonesia, Kitaliano, Kijapani, Kikiribati, Kikorea, Kilitavia, Kilithuania, Kimalagasi, Kimarshallizi, Kirmongolia, Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamo, Kislovenia,

Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalagi, Kitahai, Kitai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietnamu. (Masafa hutofautiana kwa lugha.)

© 2019 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa Limepigwa chapa Marekani.

**Taarifa ya Hakimiliki:** Isipokuwa imeelewa zwinginevyo, watu binafsi wanaweza kunakili yaliyomo katika Liahona hii kwa matumizi yao binafsi, yasiyo ya kibasha (ikijumuisha kwa mitto ya Kanisa). Haki hiyo yaweza kuondolewa wakati wo wote.

Kazi za picha zisizakilive kama kuna zuio linalolezea hiyo kwenye mstari pembeni ya mchoro. Maswali juu ya hakimili yaelekeze kwa Intellectual Property Office, 50 E. North Temple St., Fl. 13,

Salt Lake City, UT 84150, USA; email: cor-intellectualproperty@ChurchofJesusChrist.org.

**For Readers in the United States and Canada:** October 2019 Vol. 6 No. 2.  
**LIAHONA (USPS 311-480) Swahili (ISSN 2326-3695) is published twice a year (April and October) by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, 50 E.**

North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City, Utah. Sixty days' notice required for change of address. Include address label from a recent issue; old and new address **must** be included. Send Salt Lake Distribution Center at address below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit card orders (American Express, Discover, MasterCard, Visa) may be taken by phone or at store.ChurchofJesusChrist.org. (Canada Post Information: Publication Agreement #40017431)

**POSTMASTER:** Send all UAA to CFS (see DMM 507.1.5.2). **NONPOSTAL AND MILITARY FACILITIES:** Send address changes to Distribution Services, Church Magazines, P.O. Box 26368, Salt Lake City, UT 84126-0368, USA.

## TAFUTA ZAIDI

Kwenye programu tumizi ya Maktaba ya Injili au kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org, unaweza:

- Kupata toleo la sasa.
- Kugundua yaliyomo-ya kidijitali pekee.
- Kutafuta matoleo yaliyopita.
- Kuwasilisha hadithi na majibu yako.
- Kuagiza au kutoa agizo la zawadi.
- Kuzidisha usomaji kwa vifaa vya kidijitali.
- Kushiriki makala na video unazozipenda sana.
- Kupakua au kuchapisha makala.

## WASILIANA NASI

Tuma barua pepe ya maswali na majibu yako kwenda liahona@ChurchofJesusChrist.org.

Wasilisha hadithi yako-inayokuza imani kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org au barua pepe kwenda:

*Liahona*, flr. 23

50 East North Temple Street  
Salt Lake City, UT 84150-0023, USA



## KUWALINDA WATOTO KUTOKANA NA PONOGRAFIA

**D**ada Joy D. Jones, Rais Mkuu wa Msingi, anaelezea kwamba upendo ni silaha kubwa dhidi ya ponografia: "Kama usemi maarufu unavyosema, 'ponografia huua upendo,' lakini hebu pia tukumbuke kwamba upendo huua ponografia." Hapa kuna njia tatu ambazo kuonyesha upendo kunawaweka salama watoto dhidi ya ushawishi wa ponografia.

ULINZI:

### "Nakupenda"

Jenga mahusiano amba-po watoto wako wanahisi usalama na kupendwa.

MWITIKIO:

### "Bado Nakupenda"

Zungumza na watoto wako kuhusu ponografia na waalike waje kwako wakiwa na maswali yao.

UPONYAJI:

### "Daima Nitakupenda"

Wahakikishie watoto wako kwamba japoku-wa wanapambana na ponografia, upendo wako haubadiliki.

*Dada Jones anaelezea zaidi kuhusu kila moja ya mawazo haya katika makala yake kwenye ukurasa wa 36.*



### KILE UNACHOWEZA KUFANYA

- Kuwa huru kuzungumza na watoto wako kuhusu ngono na kwenye jinsi ya kuwalinda kutokana na ponografia.
- Wasaidie watoto kuelewa *kwa nini*.
- Kila simu janja, tablet na kompyuta vinapaswa kuwa na ulinzi, hata za vijana na watu wazima.
- Kamwe usimwache yeoyote chumbani kwenye kifaa cha vyombo vya habari.
- Usiwahukumu watoto amba-o wanaelezea kupambana na ponografia.



**"Tunawalinda watoto wetu mpaka pale wanapoweza kujilinda wao wenyewe."**

Jason S. Carroll, profesa wa maisha ya familia wa Chuo Kikuu cha Brigham Young



## Wilson Di Paula

San José, Uruguay



Ajali ya pikipiki ilimuacha Wilson akiwa amepooza. Mwaka mmoja baadaye mkeœœ akafariki. Kama mijane mwenye watoto warwili wadogo wa kike, Wilson hakujua nini cha kufanya. Hakujua ikiwa kulikuwa na lengo katika maisha. Wilson angeweza kuwa mkali. Badala yake, alianza kutafuta ukweli.

CODY BELL, MPIGA PICA



### GUNDUA ZAIDI

Ona mengi kuhusu safari ya imani ya Wilson, ikijumuisha picha za ziada, kwenye toleo la mtandaoni au Maktaba ya Injili ya makala hii kwenye [ChurchofJesusChrist.org/go/10196](http://ChurchofJesusChrist.org/go/10196).

### JINSI YA KWASILISHA TASWIRA YA IMANI

Kwenye [liahona.ChurchofJesusChrist.org](http://liahona.ChurchofJesusChrist.org), unaweza kutuma maelezo mafupi na picha yenyé muonekano mzuri wa mtu fulani ambaye imani yake imekupa msukumo.

Nilikuwa na maswali mengi. Kwa nini mambo mabaya hutokea? Nilikuwa nikie-nda wakati wote nikijaribu kufanya mambo sahihi, na mke wangu alichukuliwa kutoka kwangu na niliachwa kwenye kiti cha wale-mavu, kisha madaktari walitakiwa kum-fanyia upasuaji wa kichwa binti yangu ili kuondoa uvimbe. Nilianza kufikiri kwamba hakukuwa na lengo katika maisha.

Nilitambua kwamba nilihitaji kupata ukweli. Nilichunguza madhehebu tofauti na kupata Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Nilihisi kwamba lilikuwa ni ukweli.

Sasa ninajua kwamba kuna lengo la kuwa hapa duniani. Tuko hapa kama sehemu ya mpango wa Baba wa Mbinguni. Tunaye Mwokozi ambaye alishinda kifo na alifufuka. Kujua hili kunanipa nguvu. Sasa, ninajitahidi kuvumilia na kusonga mbele. Nina lengo na ninajua kwamba pale ninapajaribu kuishi maisha ya kustahili, ninaweza kuwa na familia ya milele.

# Kanuni za Kuhudumu

## Je, Unakosa Sehemu Hii *Muhimu ya kuhudumu?*

*Kuhudumu ni “kufurahi pamoja nao wafurahio” kama ilivyo “kulia pamoja nao waliao” (Warumi 12:15).*

Tunapofikiria kuhusu kuhudumu, ni rahisi kuwafikiria wale walio katika uhitaji. Tunazungumza kuhusu kutengeneza bustani kwa ajili ya mjane, kupeleka mlo wa usiku kwa mgonjwa, au kutoa kwa wale wanaosumbuka. Tunakumbuka ushauri wa Paulo wa “kulia pamoja nao waliao,” lakini je, tunafokasi vya kutosha kwenye kipengele cha *kwanza* cha fungu hilo—cha “kufurahi pamoja nao wafurahio”? (Warumi 12:15). Kufurahi pamoja na wale tunaowatumikia—hiyo ikiwa inamaanisha kusherehekeea mafanikio yao au kuwasaidia kupata furaha katika nya-kati ngumu—ni sehemu muhimu ya kuhudumu kama ambavyo Mwokozi angehudumu.

Hapa kuna mawazo matatu yanayoweza kusaidia (na moja kuepuka) tunapotazama kwenye kufokasi katika mema Mungu anayoweka katika maisha yetu.

### 1. Kuwa Mwangalifu

Bonnie H. Cordon, Rais Mkuu wa Wasichana, anatusaidia kuelewa kwamba tunahitaji *kuwaona*



### SHIRIKI UZOEFU WAKO

Tutumie uzoefu wako jinsi ulivyowahu-dumia wengine au ulivyohudumiwa. Nenda kwenye liahona.ChurchofJesus Christ.org na ubofye "Wasilisha Makala au Jibu."

wale tunaowahudumia—kuona si tu mizigo yao na mahangaiko bali pia uwezo wao, talanta, na mafanikio yao. Alisema kwamba tunahitaji kuwa "mshindi, na mwandani—mtu anayejua hali zao na kuwasaidia katika matumaini na matamano yao."<sup>1</sup>

Katika mfano wa kondoo na mbuzi, Mwokozi alisema wale ambaowangekuwa kwenye mkono Wake wa kuume wangeuliza: "Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha? au una kiu tukakunywesha?

"Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha? (Mathayo 25:37–38).

Akina kaka na akina dada, neno la msingi ni *ona*," Dada Cordon alisema. "Wenye haki waliwaona wale walio na mahitaji kwa sababu walikuwa wakinangalia na kutambua. Sisi pia tunaweza kuwa jicho la kuangalia ili kutoamsaada na kufariji, kusherehekeea na hata kuota."<sup>2</sup>

### 2. Tafuta Sababu za Kusherehekeea

Sherehekeea mafanikio makubwa au madogo. Ingeweza kuwa unashinda saratani au kushinda kuachana, kupata kazi mpya au kupata kiatu kilichopotea, kuvumilia mwezi mzima baada ya kumpoteza mpendwa au kuvumilia wiki nzima bila sukari.

Piga simu kwa ajili ya kupongeza, peleka kadi, au toka kwa ajili ya chakula cha mchana. Kwa kushiriki baraka zetu pamoja, kuishi kwa shukrani, na kusherehekeea baraka na mafanikio ya wengine, tunakuwa "tumeshangilia kwa shangwe kwa raha ya ndugu zetu" (Alma 30:34).



### MFANO WA MWOKOZI

Yesu Kristo mara zote alifurahia katika furaha ya wengine. Alihudhuria harusi huko Kana, ambapo hakusherehekea tu tukio lenye furaha bali aligeuza maji kuwa divai (ona Yohana 2:1-11). Tunaweza pia kufanya juhudzi za kuhudhuria matukio maalumu katika maisha ya wale tunaowatumikia.

Tunaona pia Mwokozi akifurahia juu ya uadilifu wa wengine. Wakati alipowatembelea Wanefi, Aliwambia, "Heri kwenu kwa sababu ya imani yenu. Na sasa tazama, shangwe yangu imetimia" (3 Nefi 17:20).

### 3. Ona Mkono wa Bwana

Wakati mwingine kushangilia pamoja na wengine humaanisha kuwasaidia kuona sababu ya kushangilia—bila kujali magumu yapi au mazuri yapi yanaingia katika maisha yetu. Ukweli rahisi kwamba Baba wa Mbinguni anatufahamu na yu tayari kutuinua unaweza kuwa chanzo cha kupendeza cha furaha.

Unaweza kuwasaidia wengine kuona mkono wa Bwana katika maisha yao kwa kushiriki jinsi ulivyouona katika maisha yako. Kuwa mzoefu vy'a kutosha kushiriki jinsi Baba wa Mbinguni alivyokusaida kupitia changamoto zako. Ushuhuda huu unaweza kuwasaidia wengine kugundua na kutambua jinsi Yeye alivyowasaidia (ona Mosia 24:14).

### 4. Usiwekee Ukomo Uwezo Wako wa Kufurahi

Kwa bahati mbaya, tunaweza wakati mwingine kuwekea ukomo uwezo wetu wenyewe wa kufurahi pamoja na wengine, hasa wakati tunapohisi mashaka kuhusu kile tunachopaswa kutoa au pale tulipo katika maisha. Badala ya kutafuta shangwe katika furaha ya mwingine, tunaangukia kwenye mtego wa kujilinganisha. Na kama Mzee Quentin L. Cook wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawilii alivyofundisha: "Kulinganisha baraka hakika ni karibu sawa na kutupilia nje furaha. Hatuwezi kuwa wenye shukrani na wenye vivu kwa wakati mmoja."<sup>3</sup>



“Ni kwa jinsi gani tunaweza kushinda tabia hiyo ambayo ni ya kawaida sana karibu kwa kila mmoja wetu?” aliuliza Mzee Jeffrey R. Holland wa Akiti ya Mitume Kumi na Wawili. . . Tunaweza kuhesabu baraka zetu nyingi na tunaweza kushangilia mafanikio ya wengine. Kizuri zaidi ya yote, tunaweza kuwatumikia wengine, zoezi zuri kuliko yote la moyo ambalo limewahi kuelezezia kabla.<sup>4</sup> Badala ya kujilinganisha, tunaweza kuwasifia wale tunawatumikia. Kwa uhuru shiriki kile unachopendezewa nacho kuhusu wao au wanafamilia wao.

Kama Paulo anavyotukumbusha, sisi sote ni viungo katika mwili wa Kristo, na wakati “kiungo kimoja kikitukuzwa, viungo vyote hufurahi pamoja nacho” (1 Wakorintho 12:26). Kwa msaada wa Baba wa Mbinguni, tunaweza kujua uzofu wa watu wengine, kufurahia mafanikio makubwa na madogo, kuwasaidia kutambua mkono wa Bwana, na kushinda vivu ili kwamba tuweze kufurahia pamoja kwenye baraka, talanta, na furaha ya wengine. ■

#### MUHTASARI

1. Bonnie H. Cordon, “Kuwa Mchungaji,” *Liahona*, Nov. 2018, 75.
2. Bonnie H. Cordon, “Kuwa Mchungaji,” 75.
3. Quentin L. Cook, “Furahi!” *Ensign*, Nov. 1996, 30.
4. Jeffrey R. Holland, “Mpotevu Mwingine,” *Liahona*, Mei. 2002, 64.

#### MWALIKO WA KUTENDA

Wafikirie wale unaowahudumia. Ni talanta na uwezo gani walionao? Ni fursa na mafanikio yapi waliyowahi kupata? Ni kwa jinsi gani unawenza kufurahi pamoja nao, kuwasifia, au kuwatia moyo?



**Na Mzee Gary E.  
Stevenson**

Wa Akidi ya  
Mitume Kumi na  
Wawili



# Baraka za Mtazamo wa Injili

Mtazamo wa injili utakupa ubayana mkubwa kuhusiana na jinsi unavyofikiria kuhusu vipaumbele vyako vya maisha, kutatua matatizo, na kukabiliana na majaribu binafsi.

**N**i baraka kuu iliojo kuwa muumuni wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho katika kipindi cha maongozi ya Mungu wakati ambapo urejesho wa funguo za ufalme na utimilifu wa unabii unaturuhusu kushuhudia moja kwa moja “injili ikienea hata miisho ya dunia, kama vile jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono litabiringika, hadi litaijaza dunia yote” (Mafundisho na Maagano 65:2).

Unabii huu uliotolewa na Danieli wa Agano la Kale na baadaye kurudiwa katika kipindi hiki cha maongozi ya Mungu, unaonekana kuwa katikati ya utimilifu wake wakati tunaposhuhudia vizingi 3,300 vilivyoundwa katika Kanisa leo. Katika miaka 50 iliyopita, uumini katika Kanisa umeongezeka kutoka milioni 2.1 hadi zaidi ya milioni 16.<sup>1</sup>

Cha kupendeza kwangu kama ulivyo ukuaji huu mkubwa na badiliko ni ukweli kwamba kanuni na utamaduni wa injili havibadiliki, ikiwa ni pamoja na mtindo wa uongozi wa kiungu uliofunuliwa kwa ajili ya Kanisa la Yesu Kristo. Mtindo huu huruhusu uanzishwaji wa vizingi, vilivyokusudiwa kuwa “ngome, na makimbilio wakati wa tufani, na ghadhabu wakati itakapomiminwa pasipo kuchanganywa juu ya dunia yote” (Mafundisho na Maagano 115:6).

Akina kaka na akina dada, Bwana ni mkarimu kwa baraka Anazotupatia. Kuelewa kwamba baraka ni matendo ya utiifu wetu wa amri na kwamba kutii amri ni onyesho

*Moja ya miujiza mikuu ya uwepo wenu hapa duniani utakuwa uwezo wenu wa kupata usawa kati ya mambo yenu ya kiroho na majukumu mengine muhimu ya maisha.*

la upendo wetu kwa Bwana ni kanuni za thamani kujifunza. Kanuni za injili kama hizi hutoa mtazamo muhimu kwetu.

Hii huongoza kwenye mawazo mawili ambayo ningependa kusisitiza. Niligundua kwamba Rais Dallin H. Oaks, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, aliwahi kushiriki mawazo haya mawili na vijana wadogo waseja mnamo 2015.

### **Dumisha Mtazamo wa Injili**

Rais Oaks amesema kwamba “mtazamo humaanisha kuona kweli zote katika mahusiano yenyе maana, mtazamo wa jumla.”<sup>2</sup> Hapa ni baadhi ya mambo unayolewa wakati unapoona kutokea kwenye mtazamo wa injili:

- Ninyi ni watoto wa Baba wa Mbinguni mwenye upendo (ona Mafundisho na maagano 76:24).
- Mko hapa duniani kwa lengo fulani, mkiwa na uwezo wa kufanya chaguzi (ona 2 Nefi 2:27; 10:23).
- “Kwani lazima, kuwe na upinzani katika vitu vyote” (2 Nefi 2:11).
- Yesu Kristo ni Mwokozi wetu na mtetezi wetu kwa Baba (ona 1 Yohana 2:1; Mafundisho na Maagano 110:4).

Fikiria nini hutokea ikiwa mtazamo wako wa injili unakutwa lenzi unayotazamia katika kila kipengele cha maisha yako. Mtazamo wa injili utakupa ubayana mkubwa kuhusiana na

jinsi unavyofikiria kuhusu vipaumbele vyako vyaa maisha, kutua matatizo, na kukabiliana na majaribu binafsi. Hii inaweza hakika kuathiri mtazamo wako kwa ujumla kwa maisha yako yote na maamuzi mbalimbali utakayofanya njiani.

Kwa mtazamo huu wa nje, tunajua kwamba Bwana anatamani kwamba tupokee sakramenti kila wiki na kwamba tusome maandiko na kusali Kwake kila siku. Kwa kuongezea, tunajua kwamba Shetani atatujaribu ili tusimfuate Mwokozi wetu au kusikiliza misukumo ya upole ya Roho Mtakatifu. Kisha tunaweza kujua zaidi kwamba mjaribu anajitahidi kuchukua uhuru wa kujiamulia na uwezo wa kuhimili juhudhi zake kuititia uraibu, ikiwa ni pamoja na madawa ya kulevyaa na ponografia.

Kinyume chake, lenzi ya injili hutupatia uoni angavu wa umuhimu wa kuanzisha familia—kuchagua ndoa na kuwalea watoto katika haki. Mtazamo huu pia hufungua macho yetu kuona kwamba mjaribu angependa kuangamiza kitengo chote cha familia na kukanganya majukumu ya jinsia, hivyo kuongoza kwenye upungufu wa thamani ambao jamii inaweza kwenye kuunda na kujenga familia.

### **Dumisha Usawa wa Kiroho**

Rais Oaks alisema: “Wakati vijana wakubwa wanapokuwa na mtazamo—mtazamo wa jumla—ni muhimu kwao kudumisha *usawa* wa kiroho katika maisha yao. Ili kufanya hivi, lazima mijiondoe kutoka kwenye baadhi ya vivutio vyaa ulimwengu na pia kufanya mambo muhimu ili kusogea karibu na Mwokozi.”<sup>3</sup>

Kwa upande mmoja, mna misukumo mingi na vipaumbele vyaa maisha vyaa aina zote na ukubwa wote, vyote vikihitaji umakini, fokasi, na mwelekeo. Orodha kwa kila mmoja wenu inaweza kuwa tofauti kulingana na hali zenu binafsi, lakini ndani yake hakika mtapata elimu, ajira, ndoa, na vyote

kuwa vizuri kihisia na kimwili. Ndiyo, changamoto yenu ni kuwekea usawa majukumu haya muhimu ya maisha dhidi ya mambo yenu ya kiroho.

Rais Oaks pia ameshauri kwamba mnapaswa kuwa makinii wakati “mnapopanga muda wenu ili kwamba msijishi-ndishe njaa kiroho wakati ambapo shughuli zenu za msingi ziko kwenye mambo mengine. Kanuni hii inaelezea kwa nini ni muhimu hasa kwa vijana wakubwa ... kufuata ushauri wa kuhudhuria mikutano ya Kanisa, kutumikia Kanisani na kusoma maandiko kila siku, kuwa na sala ya kupiga magoti ya familia, na kutumikia katika miito ya Kanisa.”<sup>4</sup>

Katikati ya mahitaji yenu binafsi na tofauti, kuwekea usawa utafutaji na changamoto pamoja na mambo ya kiroho, mtakuja kugundua kwamba usawa unawezekana. Bwana hawahitaji mfanye jambo ambalo hamwezi kufanikisha. Nilimsikia Rais Thomas S. Monson (1927–2018) mara kadhaa akishauri kwamba “yule ambaye Bwana humwita, Bwana humstahilisha.”<sup>5</sup> Ninadhani hili hasa ni kweli kwa waumini wa Kanisa.

Ya kutisha kama kuweka usawa huu kunavyoweza kuonekana, ninaahidi kwamba moja ya baraka kubwa ya kuwepo kwenu katika maisha haya itakuwa uwezo wenu wa kupata usawa kati ya mambo yenu ya kiroho na majukumu mengine muhimu ya maisha. Hii inaweza kutokea katika njia ambayo itawaruhusu si tu kudumisha mambo yenu ya kiroho na majukumu muhimu ya maisha kama hali ilivyo lakini pia kukua na kuendelea kwenye maeneo haya yote muhimu.

Sababu kuu ya hili kuwezekana ni kwamba Bwana yupo kwenye egemeo la wenzo. Yeye ni kitovu hasa cha mvutano cha usawa. Na Yeye ana mvuto wa kiungu kwako binafsi kama mmoja wa watoto Wake. Lakini matokeo haya huto-ka kwenye fokasi na juhudji yako inayofaa ya kutafuta usawa.

Kutoka kwenye ugunduzi wangu na uzoefu binafsi, inao-nekana kwamba tuna tabia kote katika maisha kuegemea zaidi upande mmoja au mwengine. Kubaki kwenye usawa katika maisha yetu kunahitaji juhudji na kujali kwetu kuliko endelevu. Kwa uchangamfu chagua kubaki imara.

Cha kuvutia, inaweza kuwa pande zote. Kunaweza kuwa na nyakati ambapo unajikuta unahitaji kujali ili kuwa na fokasi bayana kwenye kazi yako ya shule au ya kuajiriwa, pamoja na “shughuli za Kanisa zifanywe ndani ya muda wa shughuli za Kanisa.”<sup>6</sup> Hata hivyo, kumbuka kumweka Bwana kama egemeo lako la wenzo ili uweze kupata usawa wako wa kiroho unaofaa.

### **Bwana atakusaidia**

Tunapotunza mtazamo wa injili, inakuwa rahisi kuelewa ukweli wa msingi kwamba Bwana atatusaidia. Kanuni ya misi-ningi ya injili ni kwamba sisi ni watoto wa Wazazi wa Mbinguni wenye upendo. Ni asili Yao kutusaidia sisi katika kila njia ili turudi nyumbani kwetu mbinguni.

Ningependa kushiriki mfano wa jinsi gani Bwana anawenza kuwasaidia. Mmoja wa viongozi wangu wa vijana, Thad Carlson, alishiriki nami miaka mingi iliyopita. Thad, ambaye amefariki hivi karibuni, alikuwa na matokeo makubwa kwanza wakati nilipokuwa nakua. Alizaliwa wakati wa Mporomoko Mkuu wa uchumi, akiwa wa tisa kati ya watoto 14. Familia yake ilipata kipato kwa kulima na kufuga ng’ombe. Ulikuwa ni wakati mgumu kifedha, na mali yao kubwa ilikuwa kundi la ng’ombe.

Katika ujana wa Thad, moja ya majukumu yake ilikuwa ni kutunza na, ilipohitajika, kuchunga ng’ombe ili kuhakikisha kwamba walipata malisho mazuri—kazi nzito kwa mvulana mdogo. Aliweza kufanya hili kwa msaada wa farasi mdogo

*Kumbukeni kudumisha Mtazamo  
wa Injili. Tazama ulimwengu  
unaokuzunguka kupitia lenzi ya injili  
ya Yesu Kristo.*

mjanja ambaye alijua barabara nini cha kufanya kwa maelekezo kidogo. Farasi alipewa jina la Smoky Mzee. Lakini Smoky Mzee alikuwa na shida moja: hakutaka kukamatwa. Popote wakati mtu alipomsogelea, angekimbia, akijua kwamba angepewa kazi.

Siku moja, baada ya Smoky Mzee kukamatwa, kufungwa ugwe, na kuwekewa tandiko, kijana Thad alimwendesha kuelekea mahali ng'ombe walipokuwa wakilisha. Ardhi ili-kuwa kavu, na malisho hali kadhalika, lakini Thad aligundua kwamba nyasi nje ya malisho kandokando ya vyuma vya reli zilikuwa ndefu na za kijani. Hivyo alifikiri angewaongoza ng'ombe nje ya uzio wa malisho na kuwaacha wafurahie malisho mazuri kandokando ya vyuma vya reli.

Kwa msaada wa Smoky Mzee, Thad aliongoza ng'ombe nje ya malisho, ambapo walianza kwenda mbele na nyuma kando-kando ya vyuma vya reli walika nyasi nzuri, za kijani. Ng'ombe walioridhika walionekana kujisimamia wenyewe, hivyo Thad alishuka kutoka kwenye farasi wake na kuketi juu ya kamba za ugwe, akifurahia mazingira yaliyomzunguka, akicheza na kuifurahisha mwenyewe. Akitafuta kujichunga mwenyewe kwenye nyasi za kijani, hata hivyo, Smoky Mzee hatimaye alienda zake, kamba zake zikiteleza nje kutoka chini ya Thad.

Wakati huu wa kupendeza na wa amani ulifikia kishindo na kusimama ghafla wakati Thad ghafla aliposikia kelele nyingi kutoka mbali. Ilikuwa ni king'ora cha kichwa cha garimoshi iliyokuwa ikija kwa kasi kwenye vyuma vile vya reli ambapo kundi la ng'ombe wake walikuwa wametapaka kizembe mbele yake! Aligundua kwamba madhara yangeweza kuwa ya kutisha kwa kundi la mifugo na pia kwa familia yake kama asingefanya uamuzi wa haraka kurudisha ng'ombe kwenye malisho na mbali na garimoshi iliyokuwa inakuja. Alihisi kwamba asingeweza kuji-samehe kwa kutotimiza majukumu yake alioaminiwa kwayo.

Thad kwa haraka aliruka na kusimama na kukimbia ili kushika kamba za Smoky Mzee. Smoky Mzee alimwona Thad akija na haraka aliruka mbali naye, kwa kutotaka kukamatwa.

Bila pumzi na kwa kukata tamaa, pamoja na taswira za ng'ombe waliokufa na janga la familia vikipita akilini mwake, Thad alijua alipaswa kutenda kwa haraka.

Baadaye aliandika kile kilichotokea: "Mwalimu wangu wa Msingi alikuwa ametufundisha jinsi ya kusali na kuimarisha mafunzo niliyojifunza kutoka kwa mama yangu. Bila kuwa na njia nyingine, nilipiga magoti na kuanza kusali kwa ajili ya msaada wa kuwaondoa ng'ombe kutoka kwenye vyuma."

Thad hakisikia sauti, lakini wazo dhahiri lilimujia: "Umegundua jinsi ng'ombe wanavyoweza kutembea kando ya Smoky Mzee na hakimbii. Hivyo . . . sasa kwa kuwa umepiga magoti, pia weka mikono yako kwenye kazi. Fanya kama vile wewe ni ng'ombe na tambaa kuekekea kwa Smoky Mzee."

That alisema: "nilifanya hivyo. hakukimbia. Nilishika kamba zake, kumuongoza kwenye uzio, nikaruka mgongoni kwake, na tulikimbia kama upepo kuwarudisha ng'ombe kwenye malisho. Smoky Mzee alikuwa mzuri sana kwenye kupindapinda na kugeuka."

Baadaye, wakati Thad alipokuwa shule ya upili, ilieleweka kwake kikamilifu kwamba alikuwa amepokea jibu dhahiri kwa sala yake katika wakati hasa wa uhitaji. Alisema, "Malaika walimhudumia Smoky Mzee kupita uwezo wangu, na familia yetu ilikuwa imeepushwa na janga." Baadaye alisema: "Huu ulikuwa wa kwanza kati ya misukumo mingi ambayo [ilipaswa] kuja kwangu. 'Na chochote mtakachomwomba Baba katika jina langu, ambacho ni haki, mkiamini kwamba mtapata, tazama, kitapewa kwenu' (3 Nefi 18:20)."<sup>7</sup>

Sote tuna ng'ombe wa kuwaondoa kutoka kwenye vyuma vya reli kabla ya garimoshi kufika. Magumu yetu huja kwa maumbo mengi na ukubwa tofauti. Baadhi ni hatari kama hali ya hatari ya Thad, yakiwa na madhara ya kutishia maisha au kutishia nafsi zetu au za wapendwa wetu.

Hali zingine tunazokumbana nazo zinaweza zisiwe na madhara ya hatari kama hayo lakini hata hivyo huelemea akili na mioyo yetu. Kitu kimoja ni hakika—kila mmoja wetu atapata dhiki na mateso katika maisha yetu kwa sababu ni sehemu ya uzoefu wetu wa maisha ya duniani. Lakini kumbuka, Bwana atatusaidia!

Ninayapenda maneno haya yanayopatikana kwenye Kitabu cha Mormoni: "Tunaona kwamba Mungu ni mwangalifu kwa

kila watu, nchi yoyote ambayo wangekuwa ndani; ndio, huhesabu watu wake, na ana huruma za kutosha kwa ulimwengu wote” (Alma 26:37).

Hiyo humaanisha kila mmoja wetu. Ni faraja kuu ilioje kujua kwamba Bwana atatusaidia.

### **Imani, Tumaini na Mtazamo wa Injili**

Kwa ufupisho, ninawahimiza kukumbuka kudumisha mtazamo wa injili. Tazama ulimwengu unaokuzunguka kuititia lenzi ya injili ya Yesu Kristo.

Dumisha usawa wa kiroho. Sote tunapata changamoto na fursa katika majukumu yetu mbalimbali ya maisha, na yanahu-dumiwa ipasavyo wakati tunapoyawekea usawa na imani yetu katika Yesu Kristo na Upatanisho Wake.

Mwisho, kuwa na imani na tumaini kwamba Bwana atakusaidia. Ufahamu huu ndio unaokusaidia kwa ujasiri

kupambana na changamoto ambazo ni schemu isiyoepukika ya misheni yako ya maisha ya duniani. ■

*Kutoka kwenye hotuba ya ibada, “Mtazamo wa Injili,” Ilyotolewa katika Chuo Kikuu cha Brigham Young-Hawaii mnamo Septemba 19, 2017.*

### **MUHTASARI**

1. Ona “Ripoti ya Takwimu, 2018,” *Liahona*, Mei 2019, 112.
2. Dallin H. Oaks, mukutano wa mafunzo wa vijana wakubwa waseja, Feb. 8, 2015, Jiji la Salt Lake, Utah.
3. Dallin H. Oaks, mukutano wa mafunzo wa vijana wakubwa waseja, Feb. 8, 2015.
4. Dallin H. Oaks, mukutano wa mafunzo wa vijana wakubwa waseja, Feb. 8, 2015.
5. Thomas S. Monson, “Wajibu wa Mito,” *Ensign*, Mei 1996, 44.
6. Dallin H. Oaks, mukutano wa mafunzo wa vijana wakubwa waseja, Feb. 8, 2015.
7. Thad Carlson, barua binafsi.







# Kuwalinda Watoto

---

Nini tunaweza kufanya ili kuwalinda vyema na kuwawezesha watoto katika maisha yetu?

**Na Marissa Widdison**

Majarida ya Kanisa

**K**ati ya makundi yote ya watu Yesu aliowafundisha, tunajua Aliwpenda hasa watoto. Aliwapa umakini watoto hata wakati hali hai-kwua ya kufaa. Aliwaalika watoto kupokea baraka binafsi kutoka Kwake. Aliwashutumu wale waliowaumiza watoto. Na Alifundisha kwamba tunapaswa kuwa zaidi kama watoto ili kuingia ufalme wa mbinguni.<sup>1</sup>

“Tazama wachanga wenu,” Yeye aliwaambia wale waliokuwa bara la Amerika baada ya Ufufuo Wake. Mbingu zilifunguka, na malaika walinzi, wenye upendo waliteremka kutoka mbinguni na kuzunguka wale wachanga, na walizungukwa na moto. (Ona 3 Nefi 5:23–24.)

Pamoja na hatari zote ulimwenguni leo, tungetamani kuwa watoto wetu wangekuwa daima wamezungukwa na moto wa mbinguni. Inakadiriwa kuwa mmoja kati ya watu wanne ulimwenguni amenyanyaswa akiwa mtoto, na was-tani huo unaongezeka unapotazama makundi ya waathirika, kama vile wale wenye ulemavu.<sup>2</sup> Habari njema ni kwamba kuna mengi tunayoweza kufanya kuwa wenye kujihusisha kuhusu kuwalinda watoto.

“Pata taswira akilini mwako ya mtoto unayempenda,” alisema Rais Mkuu wa Msingi. “Unapomwambia mtoto huyu, ‘ninakupenda,’ hiyo ina maana gani? . . . Tunatoa ulinzi ili kwamba tuweze kuwasaidia wale tunaowapenda kuwa bora na kukabiliana na changamoto za maisha.”<sup>3</sup>

Pengine kutazama kwa karibu zaidi kwenye mfano wa Mwokozi kunaweza kuchochea mawazo kuhusu jinsi tunavyoweza kuwalinda vizuri watoto katika maisha yetu.



*Mwokozi alipowatemelea Wanefi,  
Alimbariki kila mtoto kibinafsi.  
Vivyo hivyo, sisi tunapaswa  
kumfahamu kila mtoto.*

### Yesu Alitenga Muda kwa Ajili Yao

Yesu alitenga muda kuwapa umakini watoto na wenyewe kuteseka (ona Mathayo 19:14). Sisi pia tunaweza kutenga muda kuwasikiliza watoto wetu na kujaribu kuelewa changamoto zao.

“Kadiri mtoto anavyohisi upendo mwingu, ndivyo inavyokuwa rahisi kwake kufunguka,” Dada Jones alisema. “... *Sisi tunapaswa kuanzisha mazungumzo na si kusubiri watoto waje kwetu.*”<sup>4</sup>

Mama mmoja aliona ni msaada kuwaliza watoto wake kila jioni, “Je, mlisikia maneno yoyote leo ambayo hamkuyaelewa?”

Silika ya kwanza ya watoto wetu inaweza kuwa kutazama mtandaoni kutafuta majibu kwa sababu mtandao unatoa msaada wa haraka na hauhukumu, lakini tunahitaji kuwashawishi kwamba *sisi* ni chanzo cha kuaminika zaidi cha taarifa. Na hilo linajumuisha kutokujibu kwa hasira wakati watoto wetu wanapotuambia kitu ambacho si cha kuleta hisia nzuri. Kwa mfanano, ikiwa tumekuwa na hisia za hasira wakati mtoto wetu alipokiri kwamba wametafuta ponografia, wanaweza wasirudi kwetu tena kwa ajili ya usaidizi. Lakini ikiwa tutajibu kwa upendo, tuna fursa ya kutuma ujumbe wa wazi—kwamba tunawataka kuzungumza nasi kuhusu *kitu chocote*.

Dada Jones alisema, “Matatizo madogo yakizungumzwa katika njia ya upendo yanatengeneza msingi wa mjibizo wenyewe afya ili kwamba matatizo

makubwa yanapokuja, mawasiliano yanaendelea kuwa wazi.”<sup>5</sup>

Baadhi ya mazungumzo ya muhimu, yenye ulinzi ambayo wazazi wanaweza kuwa nayo pamoja na watoto wao ni kuhusu mili yao. Mazungumzo haya yanajumuisha maneno sahihi ya sehemu za mwili, taarifa kuhusu usafi, na mabadiliko ya kutarajia katika miaka ya usoni. Tunapaswa kuzungumza kuhusu kujamiihana na jinsi vitendo vya kimpenzi vya kimwili na kihisia ni sehemu muhimu ya mpango wa Baba wa Mbinguni. Tungeweza pia kuzungumzia mada kama vile unyanyasaji na ponografia. Mazungumzo haya yanahitaji kuwa sahihi-kwa umri na yanayoongozwa na maswali waliyo nayo watoto wetu. Kwa hakika, tungakuwa na mazungumzo baada ya muda, tukiongeza taarifa pale watoto wetu wanapokua na ufahamu wao kuongezeka. (Ona mwisho wa makala hii kwa nyenzo zenye kutoa usaidizi.)

### Yesu Aliweka Mfano kwa ajili Yetu

Yesu aliweka mfano mkamilifu kwa ajili ya kila mtu (ona Yohana 8:12). Kama watu wazima, tuna fursa na wajibu wa kuwa mifano. Moja ya njia bora ambazo kwazo tunaweza kuwasaidia watoto wetu kuwa salama ni kwa kufanya chaguzi salama sisi wenywewe. Watoto wanagundua jinsi wazazi wao wanavyowatendea wengine na wanavyowaruhusu wengine kuwatendea wao.

Tafadhali, ikiwa upo katika mahusiano au unapambana na uraibu unaokuweka wewe na familia yako hatarini, pata msaada. Tafuta mamlaka za kiraia na wataalamu wa ushauri, vilevile askofu wako au rais wa Muungano wa Usaidizi wa akina Mama, ambao wanaweza kukuunganisha na nyenzo sahihi za Kanisa na jamii. Unastahili usalama na heshima.

Tunapaswa pia kuwa mfano wa kujali kwa ajili ya nguvu yetu ya kiroho. Je, watoto wetu wanatuona tukisali? Je, wana-jua kuwa tunasoma maandiko? Je, wamewahi kusikia shuhuda zetu? Je tunavaa “silaha zote za Mungu” kama familia asubuhi kabla ya kutoka kwenda ulimwenguni? (ona Waefeso 6:11–18; Mafundisho na Maagano 27:15–18).

### **Yesu Alizungumza kwa ajili Yao**

Mwokozi alizungumza dhidi ya wale waliowaumiza watoto (ona Mathayo 18:6). Sisi pia tunaweza kuwa mawakili kwa ajili ya watoto katika maisha yetu.

“Watoto wanahitaji wengine kuzungumza kwa ajili yao,” alifundisha Rais Dallin H. Oaks, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, “na wanahitaji wafanya-maamuzi wan-oweka maslahi yao mbele ya maslahi ya kibinasi ya watu wazima.”<sup>6</sup>

Wakati hatupaswi kuwa waoga kupitiliza au kuwa na mashaka juu ya wengine, tunapaswa kujua vitisho vinyo-wezekana na kufanya maamuzi ya busara na salama. Viongozi wa msingi wanapaswa kufuata miongozo ya kuzuia-unyanyasaji<sup>7</sup>—kuna ulinzi kwenye kuwa na walimu wawili darasani na mtu kutoka kwenye urais akiangalia darasa.

Wazazi na viongozi wanapaswa kushauriana pamoja na kuamua ikiwa kuna tahadhari zaidi wanaweza kuchukua ili kupunguza vitisho mahususi. Kwa mfano, majengo mengi ya Kanisa yana madirisha kwenye milango ya madarasa. Ikiwa jengo lako halina, unaweza kufikiria kuacha mlango wazi kidogo wakati wa madarasa na kuzungumza na mwakilishi wako wa utawala wa-nyenzo katika eneo lako kuona ikiwa kuweka dirisha ni mbadala. Licha ya miito yao, watu wazima wote wanaweza kuweka umakini kanisani na kusaidia inapo-hitajika, kama vile kuwakaribisha wageni ambao wararanda-randa ukumbini, au kumuhimiza mtoto anaezagaa nje kurudi darasani.

Kwa huzuni, wakati mwengine watoto wanaumizwa na watoto wenzao. Ikiwa tunatambua aina yoyote ya uonevu au

mgusano wa kimwili usio sahihi kanisani au mahala popote, tunapaswa kuingilia kati haraka. Kama sisi ni viongozi, tunahitaji kuwa radhi kuzungumza na familia inayohusika—hata kama mazungumzo hayaleti hisia nzuri—kuhakikisha kwamba watoto wote wako salama. Zungumza kwa huruma na uwazi kusaidia kujenga utamaduni wa ukarimu.

Ikiwa tunaamini kwamba mtoto ananyanyaswa, tunapaswa kutolea taarifa wasiwaso huo kwa mamlaka ya kiraia mara moja. Katika nchi nydingi, simu za dharura zinapatikana ambazo hutoa huduma za kuingilia janga, taarifa, na msaada. Tunapaswa pia kumwambia askofu juu ya unyanyasaji unaodhaniwa, hasa unaomhusisha yejote anayeweza kuwafikia watoto kupitia Kanisa. Kwa kuongezea kwenye kuchukua hatua kuzuia ufikiaji wa baadaye wa wakosaji kwa watoto, askofu anaweza kutoa faraja na msaada kwa wahanga na kuwasaidia kuunganika na nyenzo za ziada kutoka Huduma za Familia.

### **Yesu Aliwabariki Mmoja Mmoja**

Yesu aliwajua na aliwabariki watoto mmoja mmoja (ona 3 Nefi 17:21). Vivyo hivyo, tunapaswa kumfahamu kila mtoto na kujaribu kumsaidia yeeye mahususi.

Ni kwa jinsi gani tunaweza kufanya kanisa kuwa salama kwa ajili ya watoto wenye hali za tiba? Je, tuna mpango kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa Msingi wenye ulemavu?



Je, masomo ya Msingi tunayofundisha yanaangalia hali tofauti za nyumba-ni? Nini kagine tunaweza kufanya kuwa wenye kujihusisha zaidi?

Maoni ya kibaguzi, maneno ya kushusha hadhi kuhusu tamaduni zingine, na mitazamo ya kushutumu kwa waumini wa imani zingine vinapaswa kutokuwa na nafasi katika ujumbe tunaoshiriki. Katika darasa moja la msingi, mvulana hakuzungumza lugha vizuri kama watoto wenzake. Kumsaidia ahisi kukaribishwa, walimu walihakikisha wanachapisha vipeperushi katika lugha zote. Matendo rahisi ya kujali huwonesha watoto kwamba tunawajua na tunawajali kibinagsi, na matendo haya yanaweza kuweka mfano kwa ajili yao kufuata.

Tunaweza kugundua kwamba baadhi ya watoto wanahitaji msaada katika njia ya dharura. Kwa mfano, japoikuwa kuwa na sununu ni sehemu ya kawaida ya ukuaji, ikiwa mtoto ana hasira, anajitenga, au ana huzuni kwa wiki kadhaa, kunaweza kuwa na tatizo kubwa zaidi ambalo linahitaji msaada wa kitaalamu. Wakati tabia za uadilifu kama sala na kusoma maandiko ni muhimu, mara nyingi msaada zaidi unahitajika kwa wale wanaopitia ugonjwa wa akili unoibuka au kuvumilia kiwewe cha siri. Kupuuzia hali hakutafanya mambo kuwa mazuri. Katika maeneo mengi, askofu anaweza kutoa usaidizi wa kifedha kwa watu binafsi na familia kwa ajili ya ushauri kuititia Huduma za Familia au watoa huduma wengine.



### Yesu Aliwawezesha

Wakati akiwalinda watoto, Yesu pia aliwawezesha. Aliwaonyesha watoto kama mifano (ona Mathayo 18:3). Baada ya kuzuru Kwake Amerika, watoto wadogo waliweza kuwfundisha watu wazima “vitu vya kustaajabisha” (3 Nefi 26:16).

Tunaweza kuwawezesha watoto tunaowafahamu kwa kuwfundisha kutambua jinsi Roho anavyozungumza na kisha kumfuata Roho wakati wa kufanya maamuzi—kuwasaidia kujenga chujio la ndani la kulinda matendo yao. Kama Dada Jones alivyofundisha, “Kuwasaidia watoto kujenga mantiki yao wenye ya ndani ya kutaka [kufanya maamuzi salama] ni muhimu.”<sup>8</sup> Hapa kuna baadhi ya mawazo ambayo yamewezesha familia zingine:

- Mama mmoja aliwfundisha watoto wake kuwa makini kwenye “hisia zao za “uh-oh” na kuwa makini kati ya watu wanaonekana “wenye hila.” Hii ilifanya kazi wakati baadhi ya watu walipajaribu kumshawishi kijana wake kuwafuata maliwatoni, na alisikiliza hisia zake za kuonya na akakataa.
- Baadhi ya familia hutengeneza mpango wa njia ya uzio kabla ya muda ili kutumika wakati wanapokutana na jambo la kudhuru. Kwa mfano, mpango wa njia ya uzio wa familia moja uliitwa “angamiza na sema” na ulijumuisha kuzima kompyuta na kumwambia mzazi mara moja ikiwa picha mbaya imetokea. Watoto wao kamwe hawakujiuliza kuhusu jinsi ya kushughulikia vyombo vya habari visivyo-faa—walijua nini cha kufanya!
- Familia nyingine ilitengeneza mfumo wa neno ambalo watoto wao wangeweza kutuma arafa kwa wazazi wao au kusema kwenye simu ikiwa walihitaji kufuatwa mara moja.
- Ungeweza kuwasaidia watoto wako kufanya mazoezi kusema, “Hapana!” wakati mtu anapajaribu kufanya jambo ambalo linawapa hisia mbaya. Kila mtoto anapaswa



Kujua kwamba wanaweza kuomba msaada, na wanapaswa kuendelea kuomba mpaka wanapokuwa salama.

### Jukumu Letu kama Watu Wazima

Hebu turejee tena tukio katika 3 Nefi 17, wakati Yesu alipochukua watoto wao wachanga, mmoja mmoja, na kuwabari, na kuomba kwa Baba juu yao. . . Na walizungukwa na moto; na malaika waliwahudumia” (mistari ya 21, 24). Pengine kipengele muhimu cha hadithi hii si tu kutufundisha sisi jinsi watoto walivyo muhimu bali pia kuelezea nini jukumu *letu* linapaswa kuwa, kama watu wazima. Sisi ni walinzi wa kizazi kijacho. *Sisi* tunapaswa kuwa malaika ambao wanawazunguka na kuwahudumia watoto. Acha tuendelee kumtazama Yesu kama mfano wetu mkamilifu na kisha kujitahidi kadiri tuwezavyo kuwazunguka wachanga wetu kwa upendo na ulinzi. ■

### MUHTASARI

1. Ona marejeleo ya maandiko chini ya kichwa cha habari cha kila kipengele katika makala hii ili kupata hadithi hizi katika maandiko.
2. Ona “Child Maltreatment (Child Abuse),” World Health Organization, [who.int/violence\\_injury\\_prevention/violence\\_child/en](http://www.who.int/violence_injury_prevention/violence_child/en).
3. Joy D. Jones, “Kuzungumzia Ponografia: Linda, Itikia, na Ponya,” *Liahona*, Okt. 2019, 38.
4. Joy D. Jones, “Kuzungumzia Ponografia,” 39, 40.
5. Joy D. Jones, “Kuzungumzia Ponografia,” 39.
6. Dallin H. Oaks, “Kuwalinda Watoto,” *Liahona*, Nov. 2012, 43.
7. Ona “Preventing and Responding to Abuse,” [newsroom.ChurchofJesusChrist.org](http://newsroom.ChurchofJesusChrist.org).
8. Joy D. Jones, “Kuzungumzia Ponografia,” 40.

### NYENZO ZA MTANDAONI ZENYE MSAADA

- OvercomingPornography.ChurchofJesusChrist.org
- “Unyanyasaji,” Mada za Injili, topics [.ChurchofJesusChrist.org](http://ChurchofJesusChrist.org)

### VIDOKEZO KWA AJILI YA KUWALINDA WATOTO


#### Nyumbani

- Tengeneza mpango wa familia kwa ajili ya kuepukana na vyombo vibaya nya habari au kuepuka hali za kudhuru.
- Zungumza katika njia zinazofaa kiumri kuhusu miili, kujamiiiana na vitendo nya kimapenzi.

#### Kanisani

- Fuata maelekezo ya Kanisa ya kufundi-sha, ikijumuisha kuwa na watu wazima wawili katika kila darasa.
- Himiza utamaduni wa ukarimu na usiruhusu uonevu.





Na Mzee  
Joni L. Koch  
Wa Sabini

# Kuwa au Kuwahi Kuwa: Hilo Ndilo Swalii

---

Tunatarajiwa kuhukumu. Lazima. Lakini  
*hatupaswi* kubagua au kumpachika  
jina mtu yejote.

**M**iaka kadhaa iliyopita mimi na mke wangu tulizuru Kasri la Kronborg huko Helsingør, Denmark. Kasri hili lilikuwa limepewa umaarufu na igizo la William Shakespeare *Hamlet*. Tulipokuwa tukitembea kwenye kuta za kasri, mawazo yetu yalijawa na matukio na mazungumzo kutoka kwenye igizo, hususan ombi maarufu la Hamlet, “Kuwa, au kutokuwa: hilo ndilo swalii.”

Lakini nilifikiria juu ya swalii lenye uhusiano zaidi la kuijiliza sisi wenyewe: “Kuwa au *kuwahi kuwa*: hilo ndilo swalii.”

## Ruhusu Maboresho

Kwa bahati mbaya, mara nyingi tunabandika majina wakati tunapozungumza kuhusu wengine. Kwa mfano, tunaweza kusema mambo kama vile:

- “*Mzee Brown ni mmisionari mvivu.*” Badala yake tunapaswa kusema, “Mzee Brown amekuwa hafanyi kazi kwa bidii siku za karibuni, lakini ninaamini anaweza kubadilika.”
- “*Mary siyo mtu wa dini.*” Kinyume chake, tungeweza kusema, “Mary amekuwa havutiwi sana katika dini, lakini anaweza kumhisi Roho ikiwa nitatoa ushuhuda wangu kwake.”

Wakati tunaposema mtu fulani *ni* kitu fulani, tunaweza kuishia kupa-chika jina au kubagua, kuhukumu pasipo kutoa nafasi ya uwezekano wa badiliko na maboresho. Lakini tunaposema *amekuwa*, tunaonesha kwa-mba tunaamini ukuaji na uendelevu vinawezekana.

### Je, ni makosa Kuhukumu?

Tafsiri nyingi za Biblia zinatoa toleo lifuatalo la fundisho la Mwokozi: "Msihukumu, msije mkahukumiwa ninyi" (Mathayo 7:1). Lakini Tafsiri ya Joseph Smith inatoa usafanuzi: "Msihukumu ninyi *pasipo haki* . . . , bali hukumuni hukumu ya haki" (katika Mathayo 7:1, tanbihi *a*; msisitizo umeongewza).

Hakika inakubalika—na hata kutege-mewa—kwamba tunatoa hukumu pale tunapokadiria, kutathmini, na kutambua hali na kufanya maamuzi. Na ni muhimu hasa kwamba tufanye hukumu ya haki pale tunapochangamana na watu.

Kwa mfano, tunapaswa kutathmini kwa makini nani tunakwenda kufunga naye ndoa, kutumia ufahamu kuelewa madhumuni ya mtu, au kukadiria uwezo wa mtu wa kutimiza jukumu la kazi ya kulipwa.

Tunapaswa daima kutathmini matendo ya watu au sifa kwa kutumia viwango vya Bwana, kama vili-vyo katika maandiko matakatifu na maneno ya manabii. Zaidi ya yote, tunapaswa kuwa na uhakika kwamba hukumu zetu hazijaribu kumtambu-lisha mtu bila ukarimu, kubagua kwa haraka, au pasipo haki kumpachika jina yejote.

### Kuweza Kubadilika

Tunatoa hukumu isiyo ya haki waka-ti bila usahihi tunapowaelezea wengine, hasa ikiwa kwa kufanya hivyo tunaone-sha kwamba hawawezi kubadilika. Katika miingiliano yetu yote na wengine, tunapaswa kukumbuka kwamba kwa sababu ya dhabihu ya upatanisho wa Bwana, kila mmoja wetu ana uwezo wa kujiboresha. Fikiria mifano hii kutoka kwa Mwokozi:

- Alisema kwa mwanamke aliye-ka-matwa kwenye uzinzi, "Enenda zako, wala usitende dhambi tena" (Yohana 8:11).
- Alimwambia mmoja wa watu waliokuwa wamesulubiwa kando Yake, "Leo hivi utakuwa pamoja nami peponi" (Luka 23:43).
- Kama kiumbe mfufuka, Yeye aliendelea kuuona uwezekano wa Petro na kumshauri, japokuwa Petro alikuwa amemkana mara tatu (ona Mathayo 26:34 na Yohana 21:15–17).
- Alimwambia Sauli, ambaye aliku-wa amewatesa Watakatifu, kutu-bu. Sauli, ambaye alikuja kuwa Paulo, alitii na kuwa mwenye haki. (Ona Matendo ya Mitume 9:3–6.)

Bwana Yesu Kristo ni shujaa wa nafasi za pili—na za tatu na za nne pia. Alitufunza kusamehe "hata saba mara sabini" (Mathayo 18:22). Yeye ni mtu pekee aliyeishi maisha makamilifu kwenye dunia hii, lakini kwa sababu ya maisha Yake, mafundisho Yake, dha-bihu Yake ya upatanisho, na Ufufuo

Wake, na kupitia ibada za injili Yake, sisi pia tunaweza kuwa wakamilifu siku moja. Kuwarejelea akina kaka na dada zetu katika njia ambayo huelezea kuto-kuwa na imani katika uwezo wao wa kubadilika kungeelezea pia kutokuwa na imani katika nguvu ya Mwokozi na Upatanisho Wake.

### Nje na Ndani

Ni uhalisia wa maisha kwamba mara nyingi tunahukumu (na tunahukumi-wa) kwa muonekanu wa kwanza. Tuko katika hatari ya kuhukumu pasipo haki, hata hivyo, wakati tunapohukumu tunategemea tu muonekanu wa kwanza na kushindwa kutathmini sifa ya kweli ya mtu.

"Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu hui-tazama sura ya nje, bali Bwana huu-tazama moyo" (1 Samweli 16:7). Yesu aliwarejelea wanafiki katika siku Yake kama "makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa . . . uchafu wote" (Mathayo 23:27).

Mwokozi alikuwa hafundishi kwamba mwonekanu chanya na wa kupendeza wa nje si kitu kizuri bali kwamba sifa ya ndani ya mwanamu-me au mwanamke (hali ya kimwili na kiroho) ni muhimu zaidi. Fikiria mahekalu yetu ya kupendeza, lakini muhimu zaidi ni ibada ambazo hufanywa ndani.

Wamisionari pia wanahitajika kue-ndeleza viwango vya uvaaji na maadili. Kwa kuwa wasafi, kuvala kwa staha, na kutumia lugha inayofaa, wana-weka mfano mzuri kwa wale ambao

kutambulishwa kwao kwenye injili ya Yesu Kristo kutakuja kupitia kile wanachooona na kusikia kutoka kwa wamisionari.

### Kutumia Utambuzi

Tunapajaribu kufanya hukumu za haki, ni muhimu kutumia utambuzi. Mwongozo kwenye Maandiko unasema utambuzi ni “kuelewa au kujua jambo kupitia nguvu ya Roho. . . Unajumisha kutambua sifa ya kweli ya mtu na chanzo na maana ya onyesho la kiroho” (“Utambuzi, Kipawa cha”).

Wakati mwingine watu ambao ni waovu ndani hutumia muonekano wa kidunia kujaribu kutuhadaa katika kudhani wanastahili kuigwa. Wao ni “wenye hekima katika macho yao wenyewe, na wenyewe busara katika fikira zao wenyewe” (Isaya 5:21; 2 Nefi 15:21). Mwokozi aliweza kuona zaidi ya uongo huu, na aliweza kutambua nguvu na sifa na kusudi la uamini-fu la moyo kati ya hata wale walio-kuwa wanyenyekevu na kutupiliwa mbali.

Alma alitumia utambuzi kama huo wakati alipozungumza na wale walio-kuwa “wametupwa nje kwa sababu ya umasikini wao” na bado walibarikiwa kwa sababu walikuwa wamejishusha na “wanyenyekevu miyoni (ona Alma 32:5–8).

Tunapaswa kukumbuka kwamba “mambo ya Roho wa Mungu . . . yatambulikana kwa jinsi ya rohoni” (1 Wakorintho 2:14). Tunapowaona wengine kama Baba yetu wa Mbinguni anavyowaona, utambuzi unaturuhusu kutoa hukumu ya haki.

### Hukumu ya Haki


Kila siku ya maisha yetu tunahukumu kwa kukadiria, kutathmini, na kutambua. Hata hivyo, Bwana anaturajia kufanya hivyo kwa haki. Kama wafuasi wa Bwana Yesu Kristo, maneno na matendo yetu, yanapaswa kuonesha kwamba sisi ni wenyewe huruma, upendo, na tuko radhi kusaidia.

Kama waamuzi wa haki, tunahitaji kuhakikisha kwamba tunakuwa makinii zaidi kwenye sifa ya mtu badala ya muonekano wao. Wakati huo huo, tunapaswa kukumbuka kwamba kila

siku tunatengeneza mwonekano wa kwanza kwa jinsi tunavyoonekana na maneno tunayotumia. Watu wengi watavutwa kujua zaidi kuhusu sifa na ujumbe wa injili ikiwa mwonekano wetu unaakisi thamani kubwa ya ujumbe wetu.

Bwana wetu, Yesu Kristo, ametuonyesha mfano mkamilifu wa kufuata pale tunapojitahidi kuhukumu kwa haki. Tunapaswa—kama Yeye anavyofanya—kuwekea usawa kile tunachoona kwenye umbo la nje na kile kinachoe-ndelea ndani ya kila mtu. ■





*Utoaji wa usanifu kutoka  
kwa wasanifu majengo  
Hyrum Pope na Harold W.  
Burton.*

*Kulia: Moja ya ukanda wa  
nakshi kuzunguka hekalu  
ukiwakilisha vipindi vinne  
vya injili vya maongozi ya  
Mungu.*




*Pambo la sahani likibeba  
mahekalu ya kwanza nane  
ya Kanisa. Laie ni chini  
katikati.*



*Katikati: Rais Heber J.  
Grant akiwa Laie kwa ajili  
ya kuweka wakfu hekalu.  
Juu: Rais Joseph F. Smith  
(mwisho kushoto) akiwa  
Laie. Aliweka wakfu eneo  
kwa ajili ya hekalu mna-  
mo Juni 1915.*



*Ukanda wa nakshi wa uza-  
zi na Avard Fairbanks.  
Kushoto: Waumini wame-  
kusanyika hekaluni (1920).*



# Hekalu la Laie Hawaii

## KARNE YA KUKUSANYIKA

Likiwekwa wakfu miaka 100 iliyopita, Hekalu la Laie Hawaii limewaru-husu Watakatifu kuku-sanyika kupokea baraka za hekaluni wakati injili ilipoanza kuenea kote ulimwenguni.

### Na Clinton D. na Angela R. Christensen

Mwandishi anaishi Utah, Marekani. Kaka Christensen anafanya kazi katika Idara ya Historia ya Kanisa.

**M**oya ya misheni kubwa ya Kanisa la Yesu Kristo katika siku za mwisho ni kutoa baraka za hekalu kwa watu wa ulimwengu, wote walio hai na walio kufa. Nabii Joseph Smith alifundisha kwamba “kusudi la kuwakusanya . . . watu wa Mungu katika kipindi chochote cha ulimwengu . . . likiwa ni kumjengea Bwana nyumba ambapo Yeye angewaza kufunua kwa watu Wake ibada za nyumba Yake.”<sup>1</sup>

Mwanzoni mwa karne ya 20, mahekalu manne tu yaliyofanya kazi yalikuwepo duniani, yote yakiwa Utah. Hivyo, kusanyiko la kimwili Utah ilikuwa ndiyo njia ya msingi ya kuweza kufikia baraka za hekaluni. Mnamo 1919, hilo libadilika. Mnamo November 27, 1919, Rais Heber J. Grant (1856–1945) aliweka wakfu Hekalu la Laie Hawaii. Hii iliweka historia katika Urejesho pale baraka za hekaluni zilipoweza kupatikana kwa mataifa mengi.

Kwa hili, Hekalu la Laie Hawaii likiwa hekalu la kwanza kimataifa. Mara moja lilihudumia waumini kutoka Hawaii, New Zealand, Samoa, Tonga, Tahiti, Japan, na Australia. Wakati Kanisa lilipoendelea kukua kote katika Pasifikasi na Asia, idadi ya nchi zilizobarikiwa na hekalu hili iliendelea kuongezeka.

Mwaka huu unaashiria kumbukumbu ya miaka 100 ya tukio hili muhimu la kihistoria katika kukusanya Israeli pande zote za pazia.

### Kusanyiko kutoka Samoa

Visiwa vya Samoa vimejinyoosha karibia maili 2,500 (4,023 km) kutoka Hawaii. Mnamo 1919, John Q. Adams, rais wa misheni katika Samoa, alisema, “Juu ya ukamilikaji wa hekalu la Laie, watu wetu walionekana kupatwa na hamu nzito ya kukusanya bidhaa za kutosha za ulimwengu huu ili kwenda hekaluni.” Aulelio Anae, kwa mfano alikuwa ametumikia kama mmisionari bila malipo kwa miaka 20. Kwa sababu ya miaka yake ya dhabihu, hakuwa na pesa za kutosha kusafiri hadi Hawaii. Hivyo kaka Anae aliuza kila kitu alichokuwa

nacho na akaweza kudunduliza \$ za Marekani 600 au \$700.<sup>2</sup> Kaka Anae na Wasamoa wengine walitoa dhabihu ya kila walichowenza ili kuhamia Laie mnamo miaka ya 1920s.

Familia moja, ya Leota, ilifika Hawaii Siku ya Mwaka Mpya mnamo 1923. Vailine Leota wa miaka saba anakumbuka, “[Mtazamo] wetu wa kwanza wa hekalu . . . ulikuwa mtazamo mzuri kuliko yote.”<sup>3</sup> Wiki mbili tu baadaye, wazazi wa Vailine, Aivao na Matala, walipokea endaumenti zao na waliunganishwa kama wanandoa, na watoto wao waliunganishwa kwao. Aivao na Matala Leota walitumikia kwa uaminifu katika nyumba ya Bwana kwa miaka 50 na walizikwa “karibu na hekalu walilolipenda sana.”<sup>4</sup> Leo, mamia ya vizazi vyao waaminifu wanaishi kote katika Hawaii.

### Jukumu LisiLOWEZEKANA

Wakati waumini wengi huko Pasifikasi waliacha ardhi zao na kuhamia Hawaii, kata na matawi mengi kutoka mataifa tofauti yalipanga safari za makundi, zilizoitwa matembezi, kwenda hekaluni. Aina hii ya kukusanyika kiroho ilitoa njia kwa waumini wa Kanisa kusafiri ili kupokea ibada za hekaluni na kisha kurudi nyumbani kujenga Kanisa katika mataifa yao wenyewe.

Katika kuweka wakfu, Rais Grant aliomba kwa ajili ya Bwana kufungua njia kwa Watakatifu huko New Zealand na visiwa vyote vya Pasifikasi na kupata vizazi vyao ili waweze kuja hekaluni na kuwa waokozi kwa mababu zao.

Matembezi kwenda hekaluni yalianza na kundi la Watakatifu wa Maori huko New Zealand miezi sita tu baada ya kuwekwa wakfu. Japokuwa ni maili 5,000 (8,045 km) mbali na Hawaii, Watakatifu hawa walishangilia kwa taarifa ya kuwekwa wakfu.

Waimate na Heeni Anaru walitamani kuwa sehemu ya kundi la kwanza kwenda hekaluni. Bado jukumu lilionekana kutowezekana kwa sababu ya umasikini wa familia na gharama zilizohitajika za paundi 1,200 za New Zealand kwa ajili ya safari—kiasi kikubwa sana. Wangehitaji muujiza.

Kwa miaka, familia ya Anaru ilifuata ushauri wa nabii na kukusanya kumbukumbu za vizazi. Kumbukumbu hizo kisha zilikaa kwenye rafu wakati familia ya Anaru wakisubiri muujiza utokee. Kijana wao, Wiwimi, alijua kuhusu imani ya wazazi wake: “Mama kamwe hakukata tamaa kwamba [asingeweza] siku moja kupiga magotii na Baba kwenye madhabahu ya hekalu.”

Muujiza ultendeka. Wimate alishinda mataba kutoka serikali ya New Zealand kwa ajili ya mradi mkubwa wa kuendeleza-ardhi. Kipato chake kutokana na mradi huu kilitoa kiasi cha kutosha kulipia kabla ili kukidhi gharama ya safari kwenda Hawaii. Wimate na Heeni walishinda hofu yao ya kusafiri baharini na kufika Hawaii pamoja na kundi la Watakatifu 14 mnamo Mei 1920. Walipokea endaumenti yao na kuunganishwa. Kisichowezekana kilikuwa kimewezezana.

Hadithi ya Anaru ni moja kati ya maelfu kuhusu Watakatifu wa Siku za Mwisho amba walisafiri kwenda hekaluni la Laie Hawaii kupokea ibada na kudai ahadi zilizotolewa na Bwana katika nyumba Yake. Hii ilihitaji dhabihu kubwa, lakini ilizalisha Watakatifu imara amba walirudi katika nchi zao wakiwa wamejandaa kuongoza Kanisa.<sup>5</sup>

### Kukusanyika Kiroho kutoka Asia

Kufuatia Vita vya pili vya Dunia na kujengwa upya kwa Kanisa huko Japani, Watakatifu huko

**1850**

1850: Wamisionari wanawasili katika Ufalme wa Hawaii kuhubiri injili iliyorejeshwa.

1855: Joseph F. Smith anatumikia misheni yake ya kwanza huku Hawaii.

**1875**



1865: Kanisa linanunua ardhi huko Laie ambapo nyumba ya mukutano imejengwa. Jengo hili linahamishwa mnamo 1916 kupisha hekalu.

**1900**



1915: Hekalu la Laie Hawaii linatangazwa na Rais Joseph F. Smith.

**1925**

1923: Familia ya Leota (chini) inahamia Laie kutoka Samoa.



Novemba 27, 1919: Hekalu linawekwa wakfu na Rais Heber J. Grant (kama inavyonekana juu, katikati).

1920: Wimate Anaru anasafiri kwenda hekaluni kutoka New Zealand.

waliunda matembezi ya kwanza ya hekaluni ya Asia. Mnamo 1965 ndege iliyojaa Watakatifu wenyewe kujitolea 165 walisafiri kutoka Tokyo mpaka Hawaii ili kupokea ibada za hekaluni. Safari hii ilileta nguvu ya ajabu kwa Kanisa huko Japani. Asilimia tisini na tano ya waumini hawa walibaki hai Kanisani. Watano baadaye walikuwa marais wa hekalu katika nchi zao, ikiwa ni pamoja na Mzee Yoshihiko Kikuchi, Kiongozi Mkuu mwenye Mamlaka wa kwanza kutoka Japani.<sup>6</sup>

Mnamo 1970 kundi la waumini wa Kikorea walisafiri kwenda Laie. Choi Wook Whan, rais wa tawi, alisema, "Tulikwenda hekaluni na ilifungua akili zetu na kutufahamisha jinsi tunavyoweza kupokea wokovu. Mpango wa milele ulikuwa halisi; shuhuda zetu zimekuwa zikii-marishwa kiasi kwamba ni vigumu kuelezea. Ni baraka kuu ilijoje kwa watu wa Korea kuwa na fursa ya kuhudhuria hekaluni."<sup>7</sup>

### Kukusanya Vizazi Vyetu Viliviyokufa

Wakati ibada za hekalu zinapopatikana kwa taifa, zinaleta baraka za Bwana si tu kwa wale walio hai katika nchi ile bali pia kwa wale kutoka katika taifa lile walio upande mwingine wa pazia. Baraka hii imehisiwa na waumini wa nchi za Asia, ambapo utamaduni wao kwa umakini umeweka kumbukumbu ya vizazi kwa karne nyingi.



1965: Kwa matembezi ya kwanza ya Kiasia ya kwenda hekaluni, Wajapani 165 wanafika Hawaii.

1970: Watakatifu kutoka Korea wanaungana na Watakatifu wa Kijapani wenyewe matembezi ya kwenda hekaluni.

Wazazi wa Kwai Shoon Lung walihama kutoka China kwenda Hawaii. Alizaliwa huko Kauai mnamo 1894 na kubatizwa mnamo 1944 kwenye siku yake ya kutimiza miaka 50. Kaka Lung alifundisha historia ya familia kanisani na kuliambia darasa lake, "nilipata ndoto usiku mmoja ambapo niliona wengi wa uzao wangu waliokufa wakiniita niwafanyie kazi." Siku tatu baadaye alipo-ke nasaba kutoka kwa shangazi yake huko China: kurasa 22 za muswada wa Kichina ukionyesha uzao wake wa nyuma mpaka 1221 BK. Pamoja na mwanawae Glenn na mkwewe Julina, wamekamilisha maelfu ya ibada hekaluni kwa ajili ya familia yao. Glenn na Julina Lung baadaye walitumikia kwa uaminifu kama rais na mlezi wa Hekalu la Laie toka 2001 hadi 2004.<sup>8</sup>

### Kukusanya Kunaendelea

Likiwa kwenye njia panda ya Pasifikasi kati ya Amerika na Asia, Hekalu la Laie Hawaii limefungua mlango wa baraka za hekalu kwa mataifa mengi. Hivyo, kukusanya kwa Israeli kukawa kimsingi kukusanya kiroho wakati waumini wanapoweza kupokea baraka za hekalu na kisha kurudi ili kujenga Kanisa katika nchi zao za asili. Fursa hii imesaidia kuenea kwa injili ya urejesho kwa tamaduni nyingi na watu wengi katika pande zote za pazia.

Tunaposherehekeea maadhimisho ya miaka 100 ya Hekalu la Laie Hawaii, tunapata fursa ya kushuhudia tukio muhimu katika Urejesho na kutimia kwa unabii wa nabii Yakobo katika Kitabu cha Mormoni: "Kubwa ni ahadi za Bwana kwa wale walio kwenye visiwa vyta bahari" (2 Nefi 10:21). ■

### MUHTASARI

1. *Mafundisho ya Marais wa Kanisa: Joseph Smith* (2007), 416.
2. Ona James Adams Argyle, comp., "The Writings of John Q. Adams," 14, FamilySearch.org.
3. Vainile Leota Niko, katika Clinton D. Christensen, comp. *Stories of the Temple in Lā'ie, Hawai'i* (2019), 70–71.
4. Aivao Frank Leota (1878–1966), FamilySearch.org.
5. Ona Christensen, *Stories of the Temple in Lā'ie, Hawai'i*, 64–65.
6. Ona Christensen, *Stories of the Temple katika Lā'ie, Hawai'i*, 114–17.
7. Choi Wook Whan, katika "Going to the Temple Is Greatest Blessing," *Church News*, Apr. 17, 1971, 10.
8. Ona Christensen, *Stories of the Temple in Lā'ie, Hawai'i*, 166.

1950

1975


2000

2015

November 21, 2010:  
Kufuatia marekebisho  
ya tetemeko na mareke-  
bisho ya umbo, Rais  
Thomas S. Monson aliwe-  
ka wakfu upya hekalu.



Juni 13, 1978: Rais Spencer W. Kimball ana-  
weka wakfu upya hekalu baada ya upanuzi  
muhimu. Yeye pamoja na Rais N. Eldon  
Tanner (juu) pia wanazuru Kituo cha Utama-  
duni cha Polinisi.



## Tuliongozwa kwa Monica

Wakati nikiishi São Paulo, Brazil, nilipata kumfahamu mwanamke wa kipekee aliyeitwa Graça. Alikuwa mwanamke wa kupendeza na mkarimu na rafiki wa wote.

Graça alikuwa mwenza wangu katika mafundisho ya kutembeleana. Alikuwa mama wa watoto watatu, alifanya kazi ya muda, na hakuwa na gari wala simu, lakini haya hayakumzuia kutumikia.

Kutoka kwenye ubaraza wangu wa ghorofani ningeweza kuona dirisha moja la nyumba yake. Alipokuwa nyumbani, Graça angeweka kipande cha nguo nyekundu kwenye dirisha lile kuashiria kuwa alikuwa tayari kwenda kutembelea.



*Graça angeweka kipande cha nguo nyekundu kwenye dirisha lake kuashiria kuwa alikuwa tayari kwenda kutembelea.*

Hakuwahi kupata sababu ya kutohudumia. Mara nyingi nimefikiria kuhusu ishara ya Graça na mfano wake wa kupendeza wa huduma ya uaminifu na rahisi.

Uzoefu mmoja unajitokeza katika akili yangu. Tulijiandaa na kuomba kabla ya kwenda kumtembelea mmoja wa dada zetu. Tulipoikaribia nyumba, tuligundua tulikuwa tumeenda kwenye nyumba ya dada tofauti! Tulikuwa tumepangiwaa kumtembelea dada huyu, mama wa watoto watatu asiyeshiriki kikamilifu, lakini hatukuwa tumepanga kumtembelea siku hiyo. Kwa sababu tulikuwa pale, tuligonga, lakini hakuna aliyejibu.



Tuliamua kuwa wavumilivu na kusubiri. Dada yule, Monica, hatimaye alikuja na kutuambia kwamba alikuwa na shughuli nyingi. Tuligundua alikuwa amechoka na machozi yalimlengalenga. Tuliposema tulikuwa pale kusaidia, alituruhusu kuingia. Mtoto wake alikuwa akilia, hivyo tulimwambia amshughulikie mtoto na sisi tungesubiri. Wakati Monica alipopanda ngazi kwenda juu pamoja na mtoto, tulianza kazi, tukisafisha vyumba kadhaa na kukunja nguo zote ambazo tungeweza kuziona.

Wakati Monica alipoona jinsi nyumba yake ilivyopendeza, alianza kulia, akafungua moyo wake kwetu, na kushiriki baadhi ya changamoto zake. Tuliahidi kumsaidia, na tulizungumza na rais Muungano wa Usaidizi wa Akina mama kuhusu changamoto zake. Jumapili iliyoofuata, Monica alikuwa kanisani.

Monica alikuwa dada aliyeshiriki kikamilifu na mwenye furaha, na tuliedelea kumhudumia kwa upendo na kujali. Bado ana changamoto zilezile, lakini aliweza kukabiliana nazo kwa imani zaidi na ujasiri kwa sababu ya kushiriki kwake kikamilifu Kanisani.

Nina shukrani kwa mfano wa Graça wakati tulipotumikia pamoja. Tuliomba kwa ajili ya mwongozo, na Mungu alituongoza kwa Monica. ■

**Rosana Soares, Utah, USA**

## Walipanda Mbegu katika Moyo Wangu

**N**ilitoka wapi? Ninafanya nini hapa? Nitaenda wapi baada ya maisha haya?

Wakati nikiwa na umri wa miaka 29, maswali haya yaliendelea kujirudia kwantru. Wazazi wangu walikuwa wamefari-ki. Niliomboleza kwa kumpoteza mwana wangu wa kwanza mchanga. Nilikuwa na watoto wengine watatu wa kulea na maisha yalijaa changamoto.

Bwana alianza kujibu maswali yangu wakati alipowaongoza wamisionari wawili vijana nyumbani kwangu. Nilipowakaribisha ndani, waliniuliza ikiwa kulikuwa na chochote nilichohisi kilikosekana katika maisha yangu. Niliwaambia kuhusu wazazi wangu na mwanangu. Niliwaambia nilidhani isingekuwa sawa kuwa na watoto na kuunda familia ikiwa kila kitu kilihitimishwa na kifo. Niliuliza ikiwa ningeweza kuwaona tena wazazi wangu na mwanangu.

“Marta,” walisema, “unaweza kuwa na familia yako milele.”

Shangwe ilijaza nafsi yangu. Nilitaka kujua zaidi. Kwenye matembezi yao yaliyofuata, walinifundisha zaidi kuhusu injili ya Yesu Kristo. Walinipa Kitabu



**N**ilihisi kwamba nilipaswa kuwaambia akina dada ambao walinifundisha mwanzo kwamba nilikuwa nimejiunga na Kanisa na kwamba walikuwa wamepanda mbegu ya injili ya urejesho ndani ya moyo wangu.

“Nilifundisha miaka mitano iliyopita!” Nilijibu.

Mimi na watoto wangu tulifundisha masomo. Siku yetu ya ubatizo ilikuwa siku yetu ya furaha kuliko siku zote za maisha yetu.

Miaka kadhaa baadaye, nilihisi kwamba nilipaswa kuwaambia akina dada ambao walinifundisha mwanzo kwamba nilikuwa nimejiunga na Kanisa. Kwenye Facebook, nilipata kundi la wamisionari waliorudi kutoka Misheni ya Brazil Santa Maria. Lilimjumuisha mmoja wa akina dada aliyenifundisha. Nilimuomba urafiki na kumwambia nilikuwa nani, jinsi nilivyokuwa muumini wa Kanisa, kwamba familia yetu ilikuwa imeunganishwa hekaluni, na kwamba kijana wangu alikuwa akitumikia misheni kwa muda wote. Nilimwambia haya yote yaliwezekana kwa sababu yeye na mmisionari mwenzake walikuwa wamepanda mbe-gu ya injili ya urejesho ndani ya moyo wangu. ■

**Marta Algarve, Santa Catarina, Brazil**



## Baraka ya Bonasi

**M**imi na mke wangu, Carmen, tulipata mtoto wetu wa kwanza wakati nilipoitwa kuwa askofu wa kata yetu. Wakati huo, tulikuwa na hali mba-ya kifedha. Ilinipa msongo wa mawazo kuwahudumia familia yangu na wakati huohuo kuwaangalia na kuwatunza waumini wa kata yangu.

Jumapili moja, nilimwona mama asiyé na mume akiwa na watoto wake wanne katika mkutano wa sakramenti. Alikaa kwenye kiti cha mwisho kanisani na alijaribu kadiri alivyoweza kuwaweka kimya watoto wake. Nilijua alikuwa vilevile na hali mbaya kifedha, lakini hakuwahi kuomba usaidizi. Wiki zili-pita, na kila Jumapili alikuja kanisani pamoa na watoto wake.

Siku moja, nilipokea hundi yangu ya malipo. Nikiwa nimebarikiwa kupokea bonasi, niliamua kutumia pesa ya ziada kununua vifaa kwa ajili ya ukarabati

muhimu uliohitajika katika nyumba yangu. Lakini nilipokuwa nikielekea sokoni, dada huyu na watoto wake waliniijia akilini mwangu. Nilihisi nilipaswa kutumia pesa ya ziada kununua chakula kwa ajili yao. Nilimpigia Carmen na kumwambia kile nilichohisi nilihitaji kufanya. Alikubali.

Wakati nikifanya manunuzi, macho yangu yalitua kwenye biskuti. Niliwaza kwamba pengine watoto wangependa peremende. Nilijaza mifuko miwili kwa vyakula na kushika njia kuelekea kwenye nyumba ya dada huyu.

Niligonga mlango wa mbao uliochaka mara kadhaa. Nilipokuwa karibu kuondoka, mlango hatimaye ulifunguliwa. "Askofu," dada alisema, "nimeshangaa kukuona hapa." Mara moja, watoto wake walikimbia nje kutoka nyuma yake.

"Nimewaletea chakula," nilisema.

Mmoja wa mabinti zake aliona

**N**ilijaza mifuko miwili kwa chakula na kushika njia kuelekea kwenye nyumba ya dada katika kata yangu.

biskuti na kusema kwa sauti, "Biskuti!" Kaka zake na dada zake kwa furaha walikusanyika. Binti wa miaka saba alinikumbatia. "Asante, Askofu!" alisema.

Nilitazama ndani ya nyumba yao na kuona kwamba dada huyu alikuwa ana-fua ndani ya sufuria sakafuni. Familia haikuwa na meza na walilala kwenye magodoro juu ya sakafu. Nilitambua kwa kiasi gani walikuwa na uhitaji. Nilifanya mipango kuhakikisha wange-pata meza na kwamba kila mmoja angepata kitanda.

Uzoefu huu ulinisaidia kutambua kwamba Bwana huwaongoza na kuwa-bariki watumishi Wake. Hatuhitaji wito maalumu ili kuwasaidia akina kaka na dada zetu. Tunahitaji tu kuwa kwenye tuni na Roho, kutambua nani anahitaji usaidizi wetu, na kuwa tayari kuwa vyo-mbo katika mikono ya Bwana. ■

**Roberto Atúncar Nieto, Lima, Peru**

# Kurasa Mbili Zilizoja Shukrani

Baba yangu aliteseka maisha yake yote kutokana na kutokujamini na hisia za kutoka na thamani. Alilelewa na baba mlevi ambaye mara kwa mara alimwambia jinsi alivyodhani hakuwa na thamani. Nashukuru, baba yangu kamwe hakuwahi kuwa mlevi, lakini hakuwahi kuniambia mimi na ndugu zangu kumba alikuwa akijivuna kwa ajili yetu au kutusifu kwa mambo tuliyofanya vizuri. Nilipokuwa nikikua, nilijaribu kumfurahisha, lakini daima nilihisi nisingeweza kufua ndafu. Hii ilitusababisha kuwa na uhusiano usio mzuri.

Mwaka mmoja, nilidokeza hili kwa askofu wangu mwenye hekima. Alini-shauri nimwandikie baba yangu barua nikimwambia sababu zote za kuwa na shukrani juu yake. Hili lingekuwa tendo la ujasiri kwangu. Majeraha yangu yalikuwa makubwa, na sikutaka barua yangu ya shukrani kuwa moja ya maudhi. Hivyo niliomba. Nikiwa na Roho akiniongoza, sababu kwamba nilikuwa na shukrani kwa ajili ya baba yangu zilianza kutiririka. Illichukua muda, lakini nilipomaliza, nilikuwa nimejaza kurasa mbili.

Nilipeleka barua yangu, bila kujua baba yangu angejibu nini. Lakini nilijua kwamba sikupaswa kuchagua jinsi atakavyojibu. Nilihitaji tu kujiangalia ndani ya moyo wangu mwenyewe na

kukumbuka kwa nini niliandika barua.

Asubuhi iliyofuata, nilipokea simu kutoka kwa mama yangu wa kambo. Alikuwa akilia. Aliniambia kuwa baba yangu alikuwa amesoma barua tena na tena na tena. Alisema asingeweza kuzungumza na mimi kwa sababu alikuwa analia sana.

“Asante!” mama alisema. “Baba yako alihitaji hili.”

Baadaye siku ile, baba yangu alipiga simu kunishukuru. Alinipigia kila siku kwa siku kadhaa kuelezea jinsi gani barua ilikuwa na maana kwake.


Natamani ningeweza kusema kwamba uhusiano wetu ulikuwa

umeponya kimiujiza, lakini tulikua bado na kazi kubwa ya kufanya. Baada ya muda, moyo wangu ulianza kupona, na uhusiano wetu uliimari. Hatimaye, niliweza kumsamehe.


Miaka michache baadaye, baada ya vita kali dhidi ya saratani, baba yangu alifariki. Nina uhakika sasa anapata uzoefu wa shangwe kuu pale Mwokozi anapomsaidia kupona kutokana na mika ya uonevu. Ninajua kwamba nimepata uzoefu wa uponyaji kuititia nguvu ya Upatanisho ya Yesu Kristo. Mwokozi anaelewa mahitaji yetu na anaweza kutusaidia kuondoa sumu ya maumivu na chuki kutoka kwenye nafsi zetu. Ninajua kwamba shukrani, msamaha, na upendo ni tiba zenye nguvu. ■

**Elise Dahlen, Utah, Marekani**

**B**aba yangu alisoma barua yangu tena na tena na tena. Asingeweza kuzungumza na mimi kwa sababu alikuwa analia sana.







# KUZUNGUMZIA PONOGRAFIA: Linda, Shughulikia, & Ponya

Matumizi haya matatu ya upendo yanaweza kuwasaidia watoto wetu katika hatari za ponografia wanazoweza kukutana nazo.

**N**inafahamu kwa maumivu makali juu ya athari ya ponografia kwa hata wale walio wadogo kabisa katika jamii yetu—watoto wetu. Maadili potovu ya kiwango cha juu, ponografia yanaweza kusababisha aibu, usaliti, uharibifu wa hisia, upotevu wa kujizuia, uraibu uliokithiri, na utekaji wote wa muda, mawazo, na nguvu. Kuna hitaji kubwa kwetu sote—wazazi, familia, walimu, viongozi—kuona hasa, thamani, na kuwalinda watoto na vijana wetu.

Upendo ni kati ya zawadi kubwa za Mungu. Kumpenda Mungu na kumpenda jirani ni amri kuu mbili tulizopewa kutoka kwa Yesu Kristo Mwenyewe. Upendo, ninaamini, pia ni silaha kuu katika kupigana dhidi ya ponografia.

Hakika, kama msemo maarufu unavyosema, “ponografia huua upendo,” lakini acha pia tukumbuke kwamba upendo huua ponografia. Hiyo haina maana kwamba upendo wetu kwa mtu unawenza kubadili uraibu wao au hata tabia zao. Bali upendo unawenza kutupatia msukumo—jinsi tunavyojiandaa, jinsi tunavyojibu, jinsi tunavyosikiliza—hususan kwa watoto wetu. Ikiwa tunakwenda kuwa na tumaini lolote la kufuta maadili haya potovu kutoka ulimwenguni, upendo lazima uwe mbele na msingi wa juhudini zetu zote.

Ninapenda kupendekeza matumizi matatu ya upendo ambayo ninatumai tutayafokasia, kuyakumbatia, na kuyafanya kuwa sheria. Matumizi haya matatu yameunganishwa kwenye awamu tatu za hatari ya ponografia watoto wetu wanawenza kukutana nazo.

Kwanza, tunasema “nakupenda” kwa kuwalinda kweli. Pili, tunasema “bado nakupenda” kwa jinsi tunavyoshughulikia mfichuo wao kwenye ponografia, iwe kwa kukuusudia au la. Na tatu, tunasema “daima nitakupenda” kwa kutoa msaada wa upendo kwa ajili yao pale wanapofanyia kazi uponyaji ikiwa wapepata uzoefu wa matumizi yaliyokithiri au uraibu. Katika kila awamu, upendo ni muhimu.

## 1 ULINZI: “NAKUPENDA”

Pata taswira akilini ya mtoto unayempenda. Wakati una-pomwambia mtoto huyu, “Nakupenda,” hiyo ina maana gani? Kwenye kiini chake, ina maana kwamba tunatoa ulinzi ili kwamba tuweze kuwasaidia wale tunaowapenda kuwa bora na kukabili changamoto za maisha. Sehemu ya ulinzi ni

*Tatizo hili linawaa-thiri wavulana na wasichana wetu, na hatuliongelei vya kutosha.*



kutengeneza mahusiano imara, yenyе uaminifu, na yenyе muendelezo. Aina hizi za mahusiano husaidia kuwaleta watoto wetu karibu. Wakati tunapojenga mahusiano ya uaminifu na kuwinda watoto wetu na wajukuu zetu—au mtoto yejote—tunawapa sehemu salama ya kugeukia. Ulinzi huu huwasaidia kuelewa wao ni akina nani na huwasaidia kufahamu uhusiano wao na Mungu. Kuhisi kuthaminiwa na kupendwa huwasaidia watoto kutazama na kutegemea ulinzi wa Baba wa Mbinguni anayetoa maelekezo kwa ajili ya furaha yao.

Nina wasiwasi kwamba wazazi wengi bado wanaweza wasitambue jinsi ponografia ilivyo hatari au wanaweza kudhani ni tatizo la mvulana wa jirani. Uhaliisa ni kwamba tatizo hili linawathiri wavulana na wasichana wetu, na hatulizungumzii vya kutosha.

Miaka mingi iliyopita, mimi na mume wangu tulisikia hadithi yenyе maana ambayo tumeirudia mara nyingi kwa watoto wetu. Hadithi inahusu nyoka wa zamani mwenye mkia wa kuchacharika ambaye alimuomba mvulana mpita njia

kumpeleka kwenye kilele cha mlima ili aone mawio ya mwisho ya jua kabla nyoka hajafa. Mvulana alisita, lakini nyoka aliahidi kutomuuma kama gharama ya kumbeba. Baada ya makubaliano hayo, mvulana kwa ukarimu alimpeleka nyoka kwenye kilele cha mlima ambapo walitaza-ma mawio ya jua pamoja.

Baada ya kumrudisha nyoka chini ya bonde, mvulana alianda chakula kwa ajili yake na kitanda kwa ajili ya usiku. Asubuhi, nyoka aliuliza, “Tafadhalii, kijana mdogo, unaweza kunirudisha nyumbani kwangu? Ni muda wangu sasa kuondoka katika ulimwengu huu, na ningependa kurudi nyumbani.” Mvulana alihisi amekuwa salama na nyoka alitimiza neno lake, hivyo aliamua angemrudisha nyoka nyumbani kama alivyoomba.

Kwa uangalifu alimwinua nyoka, akamweka karibu na kifua chake, na kumrudisha jangwani nyumbani kwake ili afe. Kabla tu hajamweka nyoka chini, nyoka aligeuka na kumuuma kifuani. Mvulana alilia na kumtupa nyoka chini. “Bwana Nyoka, kwa nini umefanya hivyo? Sasa nitakufa hakika!” Nyoka alimtazama na kumweleza kwa

tabasamu: "Ulijua mimi ni nani uliponibeba."

Katika ulimwengu wa leo, ninawaona wazazi wengi wakimpa mtoto wao nyoka. Ninazungumzia simu janja. Hatuwezi kuweka simu za mkono-ni zenyet intaneti kwenye mikono ya watoto wetu wadogo amba si wakubwa vya kutosha kuwa waliofundishwa vya kutosha, bado hawana uwezo muhimu wa kupambanua mambo na kufanya-uamuzi, na amba hawana udhibitit wa wazazi na nyenzo zingine ili kusaidia kuwalinda. Jason S. Carroll, profesa wa maisha ya familia wa Chuo Kikuu cha Brigham Young, alisema, "Tunawalinda watoto wetu mpaka wakati ambapo wanawezza kujilinda wenyewe." Shina la ubongo, ambalo linahifadhi viini vya burudani vya ubongo, vinajengeka kwanza. Ni mpaka baadaye ndipo uwezo wa kupambanua na kufanya-maamuzi kwenye upande wa mbele wa tabaka la nje la ubongo hujengeka kikamilifu. "Hivyo watoto wana pedeli ya gesi isiyo na breki kamili."<sup>1</sup>

Kila simu inapaswa kuwa na ulinzi, hata za vijana. Huu ni ushauri mzuri pia kwa watu wazima. Hakuna aliyekingwa na muromo wa nyoka mwenye sumu. Baadhi ya wazazi wanatumia simu za kurusha kwa kidole kama mbadala kwa watoto wao ili kupunguza matumizi yabaki kwenye kupiga na kutuma arafa.

Zaidi ya simu janja kuna vyombo vingine vingi ambavyo vinaweza kufikia vyombo vya habari visivytakiwa kuititia intaneti. Utafiti wa karibuni ulionesha kwamba asilimia 79 ya matumizi yasiyotakiwa ya ponografia yanafanyakira nyumbani.<sup>2</sup> Watoto wanaweza kujikuta kwenye ponografia kwa kutumia tablets, simu janja, michezo ya kuliwaza, DVD za kubebeka, na TV janja, kati ya vingine vingi. Ninazifahamu familia ambazo zimetengeneza eneo moja, lenye foleni-kubwa nyumbani kwao ambapo vifaa vya kielektroniki vinatumika. Familia hizi zinaliita "chumba cha vyombo vya habari," na vifaa vyao vyote vimewekwa wazi, kwenye mwanga. Kamwe hakuna mtu ye yoyote anayekuwa peke yake chumbani kwenye kifaa cha vyombo vya habari.

Familia zingine zimechagua sheria kama

hakuna simu kwenye vyumba vya kulala au maliwatoni. Baadhi husema tu, "kamwe usiwe peke yako na simu." Bado wengine taratibu huongeza matumizi kwenye apps ambazo watoto wao wanawenza kutumia pamoja na maunzi laini ambayo huruhusu simu ya mtoto kusanidiwa na wazazi. Kwa njia hii wanafundisha kwamba uaminifu unapatikana na kwamba usalama wa simu ni muhimu.

Vyovoyote mahitaji yalivyo kwa familia zetu, acha tumfundishe kila mwanafamilia kutumia teknolojia kwa busara na katika njia chanya tokea mwanzo—ili kujenga mzingatio wa kimaadili. Acha tuwape elimu watoto katika njia za kujenga ili watumie teknolojia kwa ajili ya wema. Tunaweza kuwafundisha kutathmini kwa kujiuliza wenyewe, "Je, kutumia hii kutatimiza malengo mema?" Chaguzi zetu katika jinsi tunavyozifundisha familia zetu sasa kutaathiri vizazi vijayvo.

Kama wazazi, natumaini tutafikiria umuhimu wa mahusiano yetu na watoto wetu na juhudhi maalumu tunazofanya ili kuwalinda. Tunapoimarisra mahusiano haya ya kupendeza, watoto wataelewa vyema kwa nini Mungu anaonya dhidi ya uovu wa ponografia, watatambua jinsi ya kuiepu-ka, na watakuwa wamejiandaa ikiwa watakutana nayo.

## 2 KUSHUGHULIKIA: "BADO NAKUPENDA"

Kujenga mazungumzo ya kukaribisha, ya wazi, na yenyet kualika amba-yo yanahimiza watoto kushiriki mawazo yao, uzoefu, na maswali pamoja na wazazi wao si rahisi. Tunaweza kuwaalika watoto wa umri wote kuja mbele ikiwa au wakati wanapojenga hatua yoyote ya tatizo la ponografia—kuanzia matumizi ya mapema, yasiyo ya kukusudia ya mara chache, mpaka matumizi makubwa, na chini mpaka kwenye matumizi yaliyokithiri. Majadiliano ya mapema ni mazuri, na watoto watakuja mbele wakiwa tayari zaidi wakati wanapojua wanapendwa na hakuna wanachosema au kufanya kinaweza kubadili upendo huo.

Mara chache sana, hata hivyo, mtoto anakuja mbele kwa kujitolea. Mara nyingi inatokea wakati mzazi mchunguzi anapomjaribu mtoto kwa, "Kuna tatizo?" au "Huonekani kuwa kawaida." Kadiri mtoto anavyohisi upendo, ndivyo inavyokuwa rahisi kwake kufunguka.

Hakikisho hili la upendo linajengwa katika akili zao kutokana na uzoefu mdogo amba huchukua nafasi tena na tena. Matatizo madogo yaliyozungumziwa katika njia ya upendo yanajenga msingi wa majibu mazuri ili kwamba wakati matatizo makubwa yanapokuja, mawasiliano yanakuwa bado wazi. Cha muhimu zaidi, watoto wanajua kwamba mwitikio wako utakuwa, "Bado nakupenda. Siachi kukupenda kwa sababu jambo fulani limetokea. Daima ninakupenda."

Kwa sababu fulani, hatuzungumzi sana na vijana pamoja na watoto kuhusu moja ya hamu kubwa na majaribu makubwa watakayokabiliana

nayo. Kutotaka kwetu kunawaweka kwenye kufundishwa na intaneti, watoto wengine au vijana wabalehe, au hata vyombo maarufu vya habari. Baadhi yetu tunaweza kusita hata kutumia neno *ponografia* karibu na watoto katika juhudhi ya kulinda usafi wao. Linaonekana la aibu sana. Pengine wazazi wetu hawakuwahi kuzungumza nasi wazi hivyo. Vipi ikiwa mazungumzo yetu yanachochaea udadisi? Vipi ikiwa wanataka kujuza zaidi? Ni kwa jinsi gani tunatarajia watoto wetu kuzungumza nasi kuhusu ponografia ikiwa hatujawahi kamwe kuzungumza nao kuhusu hilo?

Wazazi, tunapaswa kuanzisha mazungumzo na kutosubiri watoto waje kwetu. Ninapenda pendekezo la kuwa na mazungumzo ya kawaida, ya mara kwa mara, ya kufariji badala ya tukio la mara-moja. Faida za mazungumzo yenye kujali ni kwamba wazazi na viongozi wa kuaminika ni wataalamu, siyo Google; mazungumzo yanawenza kutokea katika mazingira salama; na mazungumzo huongeza uaminifu wa mtoto. Tunataka watoto wahisi kuandaliwa na kuwezeshwa, siyo kuogopa. Tunataka kuzungumza nao na siyo kuwazungumzia.

Kama wazazi na walimu, hatuvezi kuwasaidia watoto ikiwa sisi wenyewe hatuna elimu. Kufundisha *nini* na *kwa nini* ni muhimu. Tunaweza kujifunza sisi wenyewe na kuwasaidia watoto kuelewa kwa nini ponografia ni mbaya, kwa nini ni hatari sana, kwa nini hatutaki iwaumize, na nini cha kufanya ikiwa watakutana nayo.

Je, tunawapa watoto wetu *kwa nini* ya kutosheleza katika njia zinazoendana na umri wao? Ikiwa sababu pekee tunayowapa ya kuepuka ponografia ni “Ni mbaya,” hiyo inaweza kui-shia kuwa sababu isiyofaa. Badala yake, lazima tuwasilishe kwa nini nyingi kadiri tuwezavyo ili kujenga maadili ya muhimu ambayo yanaleta msukumo kwa vijana wetu.

Kuna sababu tele za kuepuka ponografia, lakini hizi ni motisha chache tu kutoka shirika la Fight the New Drug ambazo zinaweza kuwau-tia vijana wetu:

- Ponografia inaweza kubadilisha na kutandaza nyaya upya kwenye ubongo wako, na utafiti unaonesha kwamba inaweza hata kufanya ubongo wako kuwa mdogo na usioshiriki kikamilifu.
- Ponografia inaweza kuwa uraibu.
- Ponografia itaharibu kujiamini kwako.
- Ponografia inaweza kukuacha mpweke.
- Ponografia inaweza kuwaumiza wale unaowapenda.
- Ponografia inaweza kuharibu kujamiiiana kwenye siha.
- Ponografia imeungana na vurugu.
- Ponografia husababisha watu hatimaye kutokuwa waaminifu.
- Ponografia itakunyang’anya muda wako na nguvu zako.
- Ponografia husababisha msongo wa mawazo, wasiwasi na aibu.

Ningependa kuongeza kuwa ponografia ni kunyume na amri za Mungu. Hizi pamoja na sababu zingine nyingi, tunajenga kesi dhidi ya ponografia, lakini elimu bila utekelezaji hupelekeea kukata tamaa. Lazima tuweke mipaka inayofaa, na yenye kusaidia, ukomo na matarajio. Kuwasaidia watoto kujenga uwazaji wao wenyewe wa kimantiki wa ndani kwa kutaka kukaa mbali na ponografia ni muhimu. Ikiwa mtoto hawezi kujiamulia mwenyewe wapi pa kusimama kwenye suala hili, anaweza kuwa schemu ya takwimu za sasa za kushangaza.

## 3 UPONYAJI: “DAIMA NITAKUPENDA”

Wakati watoto wanapokutana na ponografia na kunaswa nayo, wana-hangaika kuonyesha hisia, kurudia hali ya mwanzo, na kupona. Msaada wa dhati, wa kweli, endelevu, imara, na wenyewe uvumilivu unahitajika pale watoto wanapochukua majukumu kwa ajili ya uponyaji wao na kusonga imbele. Hakuna anayeweza kutoa aina hii ya usaidizi kama mzazi anavyo-weza kutoa. Baada ya kuwa tumefundisha ukweli kwa makini na kibinagsi, baada ya kuwa tumejenga uaminifu na kuhimiza mazungumzo, watoto wanahitaji kujuza kwamba licha ya makosa na chaguzi zao, hakikisho letu litakuwa, “Daima nitakupenda hata iweje.”

Ninakumbuka tukio rahisi lililotokea katika familia yetu miaka iliyopita. Mimi na mume wangu tulikuwa mbali na nyumbani, na kijana wetu mku-bwa alikuwa akiwaangalia watoto wengine. Tulipokea simu kutoka kwa jirani aliyekuwa na wasiwasi akitutahdarisha kwamba gari la zima moto lilikuwa nyumbani kwetu. Tuliharakisha nyumbani na kukuta kwamba mwana wetu wa miaka 10 alikuwa akicheza kwenye ua wa nyuma karibu na shamba la hekari-sita la nyasi ndefu, zilizokauka. Alijaribu kuona ikiwa angeweza kuwasha moto kwa cheche.

Na alifanya hivyo! Muda tuliofika, moto mdogo ulikuwa umezimwa na idara ya moto, na wazima moto walikuwa wamempa elimu mwana wetu, na



Tafuta nyenzo zaidi  
mtandaoni kwenye  
overcoming  
pornography.Church  
ofJesusChrist.org.

majirani walianza kutawanyika. Mwana wetu ali-shikwa na aibu, woga, machozi, na alijua hakika alikuwa matatizoni.

Sote tuliingia ndani. Mwana wetu alikuwa na woga kwamba, japokuwa hali ilikuwa mba-yaa, yote tuliyyoweza kufanya ilikuwa ni kuweka mikono yetu kumzunguka mvulana huyu mzuri na kumhakikishia upendo wetu na faraja kwa-mba hakuumia.

Wakati watoto wanapokutana na ponografia na hasa wanaponaswa kwenye utando wake, watakuwa na aibu, woga, na machozi pia. Ni vigumu kuchukua kitu ambacho kimekuwa gizani na kukiweka kwenye nuru. Inaleta hisia za aibu na kuhitaji msaada. Wanaweza kushindwa na kupata changamoto njiani pale wanaporu-dia hali ya mwanzo na kupona. Uhitaji wao wa upendo endelevu ni muhimu. Hata hivyo, wazazi wanahitaji kufahamu kwamba upendo wao dai-ma utasaidia lakini siyo tu kitu kinachohitajika.

Katika kupona, utahitaji kugeuza upendo huo ulionao kwa mtoto wako kwenye kutafuta nye-nzo sahihi za kusaidia. Upendo wako ni msingi

wa kile kinachopaswa kutokea, lakini ikiwa mtu unayempenda amenaswa, yawezekana ukahitaji kutafuta wataalamu wanaoweza kumsaidia mpe-ndwa wako na kukusaidia pia.

Pale wewe na mpendwa wako mnapotafuta uponyaji, ninatumaini kwamba mtapata nguvu katika Yule ambaye ana nguvu za kuponya maj-eraha yote, kuwaunganisha watu pamoja, na kujenga mahusiano kupita uwezo wetu wa sasa wa kufikiria. Mwokozi wetu, Mponyaji muungwana, ana nguvu ya kuokoa. Tunaweza kuwa wazazi wa watoto wetu na kuwaelekeza Kwake, lakini Yeye pekee anaweza kuwa Mwokozi wao. Na kitu cha kupendeza ni kwamba Yeye anawapenda watoto wetu hata kikamilifu zaidi ya tunavyowapenda—bila kujali chochote. ■

*Kutoka kwenye ujumbe wa hutoba ya msingi ililotolewa kwenye mkutano wa Muungano Dhidi ya Ponografia wa Utah mnano 2018 katika Jiji la Salt Lake, Utah.*

#### MUHTASARI

1. Jason S. Carroll, katika Lisa Ann Thomson, "Mbinu Nane za Kuwasaidia Watoto Kukataa Ponografia," *Liahona*, Aug. 2017, 19.
2. "Ukweli kuhusu Tishio Mtandaoni," Parents Television Council Watchdog (blog), June 21, 2017, [w2.parentstv.org/blog](http://w2.parentstv.org/blog).

# Vijana Wakubwa

## Katika Sehemu Hii

### 44 Miadi na Ponografia

Na wafanyakazi wa *Liahona*  
na Huduma za Familia

### Kidijitali Pekee

#### Jinsi Nilivyojifunza Kujibu Wakati Mtu Anapokiri Anapambana na Ponografia

Jina limefichwa Utah, Marekani

#### Kusonga Mbele baada ya Kugundua Matumizi ya Ponografia ya Mchumba Wangu

Jina limefichwa, Ufaransa Polinisia

#### Nilikuwa Nimepambana Kushinda Ponografia. Kwa nini Yeye Asingefanya Hivyo?

Jina limefichwa, Guatemaala

Tafuta makala hizi na nyingine zaidi:

- Kwenye **liahona.ChurchofJesusChrist.org**
- Katika **Vijana Wakubwa kila wiki** (kwenye sehemu ya Vijana Wakubwa katika app ya Maktaba ya Injili)
- Kwenye **facebook.com/liahona**

### Shiriki Hadithi Yako

Je, una hadithi ya kushiriki? Au je, unataku kuona makala kuhusu mada fulani? Unaweza kuwasilisha makala yako au jibu lako kwenye **liahona.ChurchofJesusChrist.org**.

## Kumtafuta Kristo kwenye Giza la Ponografia

**K**atika kuanda makala kwa ajili ya vijana wakubwa, tunatumia muda mwingu kufikiria kuhusu masuala wanayokabiliana nayo sasa. Yako mengi sana. Lakini tulipokuwa tukipeana mawazo kwa ajili ya mwezi huu, tuliongozwa kwenye mada ambayo imetuathiri sisi binafsi, rafiki zetu, na wengine wasio na idadi: miadi na ponografia. Tulijua kwamba kupanga sehemu hii lingekuwa ni jambo gumu. Hata hivyo ponografia huathiri watu wengi katika kuvunjika mioyo, wakati mwininge katika njia za kuhariblu maisha. Na kwa vijana wakubwa waseja, inaweza kufanya wakati ujao uonekane hata usio na uhakika kuliko ambavyo tayari unaonekana, hasa katika kujiandaa kwa ajili ya ndoa.

Kwa kweli tumeona mkono wa Baba wa Mbinguni ukiongoza kazi yetu wakati tulipoanza kupokea hadithi kutoka kwa vijana wakubwa amba mohusiano yao yameathiriwa na ponografia. Na tunaona kwamba kuna zaidi ya mwangaza hafifu wa tumaini kwenye ndoa za milele zenye furaha, zisizo na uraibu. Kwa nini? Kwa sababu kila hadithi hushuhudia juu ya badiliko la-maisha, uwepo wa-tumaini, nguvu ya uponyaji ya Yesu Kristo na Upatanisho Wake.

Hivyo ukijikuta katika uhusiano amba umeathiriwa na ponografia, tunakualika kusoma sehemu ya mwezi huu, yenye makala zilizotolewa na wengine amba wanajua vyema kwamba mapambano dhidi ya ponografia ni halisi. Makala hizi zinajumuisha mada kama vile jinsi ya kuzungumzia ponografia wakati wa miadi na jinsi ya kuikibili (ukurasa wa 44), jinsi ya kujibu wakati mtu anapokiri kupambana na ponografia (kidijitali pekee), jinsi msamaha na uponyaji vinavyowezekana kwa wote wawili (kidijitali pekee), na jinsi Roho anavyoweza kukuongoza kujua jinsi ya kuendelea katika uhusiano wako (kidijitali pekee).

Tunajua kwamba ikiwa utamtegemea Mwokozi na kumualika Roho katika maisha yako pale unapotafuta majibu, Baba wa Mbinguni atakuongoza kwenye uelekeo sahihi kwa ajili ya hali yako ya kipekee. Giza la ponografia linaweza kuwa limekithiri ulimwenguni, lakini nuru ya Mwokozi ya uponyaji inangara juu ya giza lolote. Yote tunayopaswa kufanya ni kumtafuta Yeye.

Kwa moyo wa dhati,

Chakell Wardleigh na Mindy Selu

Mhariri wa Majarida ya Kanisa sehemu ya vijana wakubwa.

Soma ushauri wa Rais M. Russell Ballard juu ya jinsi ya kufanya wakati uhusiano wako wa miadi umeathiriwa na ponografia katika makala yake ya toleo la kidijitali ya *Liahonaya* mwezi huu.



PICHA KUTOKA GETTY IMAGES, IMETUNIKA KWA MALENGO YA KIELELEZO, INEANDALIWA KWA MINDO

**VIJANA WAKUBWA**

---



# Miadi na Ponografia

## Na wafanyakazi wa Huduma ya Familia na *Liahona*

Kama vijana wakubwa, sote tunajua kwamba miadi inaweza kuwa ya kuvutia, ya kuogopesha, ya kuridhisha, na ya kutia hofu vyote kwa pamoja. Pale tunapoanza kuwa wawazi kila mtu kwa mwenzake, kiuhalisztunatamani kujua mengi zaidi kuhusu kila mmoja, na kuongeza uwazi ni muhimu katika kujengna na kukuza mahusiano. Ni nini ndoto zetu, hofu, na imani? Tunahisi vipi kuhusu ndoa na familia? Ni changamoto zipi tumekutana nazo hapo nyuma au sasa ambazo tunapaswa kuzishiriki?

Jinsi ilivyo ya kuogopesha kuzungumzia (au kuuliza) kuhusu matatizo ya ponografia kunavyo-weza kuwa, *kuto kuzungumzia* kunaweza kupelekea matatizo ya kuteketeza baadaye. Kila tatizo la

ponografia la mtu ni la kipekee na lenye changamoto, na unaweza hata usijue ikiwa ni tatizo au jinsi ya kuzungumzia pamoja na mtu uliye na miadi naye, hivyo ni muhimu kwamba utafute mwongozo kutoka kwa Roho. Hakuna suluhisho moja kwa kila hali, lakini katika makala hii, tunatoa baadhi ya mapendekezo kwa wale katika yenu mnaoweza kuwa mnauliza:

- Ni kwa jinsi gani ninaweza kuzungumzia mada ya ponografia na mtu niliye na miadi naye? Na ni wakati gani mufaka kuuliza/kusema?
- Ni kwa jinsi gani ninaweza kujua ikiwa ninapaswa kusonga mbele katika uhusiano na mtu ambaye ana historia ya matumizi ya ponografia?
- Ni kwa jinsi gani tunaweza kushirikiana pamoja kushinda ponografia?

Msaada na tumaini katika kukabili ponografia kwenye mahusiano ya miadi.

Ujumbe wa mhariri: Kwa sababu "miadi" humaanisha mambo tofauti katika tamaduni tofauti, kwa madhumuni ya makala hii, tunamaanisha kwendwa kwenye miadi, ndani ya viwango vyta injili, ili kuweza kumfahamu mtu, na kujenga nao uhusiano ambaa ungeweza kupeleke na ndoa.



# Kwa Wale Ambao Wamepambana au Ambao Wanapambana

Ikiwa umepambana na ponografia kipindi cha nyuma au ikiwa unapambana sasa, wazo la kuwa na miadi linawezza kukuletea hisia ya kukosa tumaini au wasiwasi. Lakini ikiwa una hamu ya dhati ya kuondoa ponografia kutoka katika maisha yako (au tayari umeiondoa), jua kwamba kwa juhudzi zako mwenyewe na kwa msaada kutoka kwa Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo, uhusiano wa kudumu, wenyi siha unawezekana kwako. Fikiria maswali yafuatayo unapoanzisha uhusiano.

## 1. Je, Tunahitaji Kweli Kulizungumzia?

Swali la kawaida ni, "Je, ninahitaji kweli kushiriki historia yangu ya matumizi ya ponografia pamoja na mtu niliye na miadi naye, hata kama

nimetubu kwa ajili ya hilo?" Au "Je ninahitaji kuzungumzia matatizo yangu ya sasa ya ponografia na mtu niliye na miadi naye?" Kwa ujumla, suala hili *linahitaji* kujadiliwa—katika muda sahihi na katika njia nyeti. Unapokuwa na mazungumzo haya, weka akilini kanuni kadhaa muhimu:

- Muda—Mazungumzo yanapaswa kufanyika wakati uhusiano unaendelea katika hali ya dhati ambayo itauhitaji.
- Uwazi—Mahusiano yanapaswa kujengeka katika uaminifu na uwazi. Japokutwa mtu uliye na miadi naye anaweza kuchagua kusitisha uhusiano, wanahitaji kuelewa asili ya tatizo, maendeleo yako ya sasa katika kulishughulikia, na mpango wako katika kulishughulikia ikiwa litatokea tena siku za baadaye.
- Msamaha—Kuwa muwazi kuhusu matumizi yako ya ponografia na mtu uliye na miadi naye haimaanishi unahitaji kwenda kwenye maelezo ya undani wakati wa kulijadili. Ikiwa umetubu na unahisi umesamehewa, hupaswi kuhisi hatia kuhusu hilo tena. Bwana hakumbuki dhambi zetu pale tunapokuwa tumetubu (ona Mafundisho na Maagano 58:42), hivyo majadiliano yako na mtu uliye na miadi naye si zaidi kuhusu "kuungama" bali zaidi kuhusu kujenga uaminifu, kushiriki mipango yenu kwa ajili ya uponyaji endelevu, na kupata uungaji wao mkono.
- Uponyaji—Hata ikiwa umetubu, matumizi ya muda mrefu au ya kiwango cha juu ya ponografia yanaweza kuwa na madhara ya muda mrefu ya kibiolojia, kisaikolojia, kijamii, na kiroho. Mchakato wa uponyaji unaweza kuwa juhudzi kubwa na inayochukua muda mrefu, lakini uponyaji kamili na halisi unawezekana. Kupitia mchakato huo, utahitaji msaada na uungaji mkono unaofaa, ambao unapaswa kujumuisha mwenza wako mtarajiwa.



## 2. Je, Niko Tayari kwa Uhusiano wa Dhati?

Moja ya tofauti kubwa kati ya mtu ambaye yuko tayari kwa ajili ya uhusiano wa dhati na mtu ambaye hayuko tayari ni utayari wao kuwa wawazi kwa mtu waliye na miadi naye. Ikiwa unapambana na ponografia, unaweza aidha kuacha hofu ipeleke uhusiano wako mahala pasipo na uaminifu au kutumia imani kutatua changamoto pamoja.



Japokuwa inaweza kuwa yenye kuleta wasiwasi na ya kuogopesha kushiriki historia yako ya ponografia, kuepuka kutaongeza tu hisia zako za woga na aibu. Woga wako wa kumpoteza mtu huyo unaweza hata kukusababisha ukatae au kuepuka kushiriki hadithi yote, suala ambalo linawenza kuvunja uaminifu na kuharibu uhusiano wako baadaye.

Kwa upande mwagine, wakati unapoheshimu uhuru wa kuchagua wa mtu uliye na miadi naye, utaheshimu uchaguzi wao wa kubaki katika uhusiano wakijua yote *mema na mabaya*. Unaweza bado kuwa

na hofu juu ya matokeo, lakini ni muhimu kutambua kwamba, kwa kupata taarifa zote, mtu mwagine anaweza pia kukusaidia katika juhudu zako na hamu ya kuondoa ponografia kwenye maisha yako. Lakini haijalishi ikiwa uhusiano wako unaimarika au la, kwa msaada wa Mungu, unaweza kuendelea katika njia ya uponyaji.

## **Kwa Wale Ambao Wana Miadi na Mtu Ambaye Amepambana**

Kwa sababu wastani wa umri wa utambulisho wa kwanza kwenye ponografia ni miaka 11 na ni rahisi sana kufikia ponografia, idadi kubwa ya vijana wakubwa wamepata uzoefu wa ponografia katika njia fulani mpaka kufikia miaka 18. Hii inaweza kuwa kadiri miadi inavyokutana. Lakini utambulisho si sawa na uraibu, na kuna viwango tofauti vyta kujihusisha na ponografia (ona Dallin H. Oaks, "Kupona kutohana na Mtego wa Ponografia," *Liahona*, Okt. 2015, 50–55). Lakini habari njema ni kwamba Upatanisho wa Yesu Kristo unaweza kutoa nguvu na uponyaji kwa wote wanaoutafuta. Haya ni baadhi ya maswali ya kuzingatia wakati uhusiano wako unapoendelea.

### **1. Lini na Kwa jinsi gani Ninapaswa Kuuliza kuhusu Ponografia?**

Kuamua lini na kwa jinsi gani kuongelea hili pamoja na mtu uliye na miadi naye linawenza kuwa jambo la kujadili pamoja na wazazi wako, ndugu zako wakubwa, viongozi wa Kanisa, au ye yote ambaye unadhani atatoa ushauri mzuri. Tafuta njia ambayo inaonekana kuwa sahihi kwako na kisha kuwa na mazungumzo hayo katika wakati muafaka, pale unapojitoa au kuweka maana zaidi katika uhusiano wako.

Hiyo haina maana kwamba unahitaji kuanza kila miadi ya kwanza kwa swali kuhusu maisha yao ya nyuma, lakini pale uhusiano wenu unapokua, unaweza kutafuta mwongozo wa Roho kukusaidia kujua namna gani na wakati gani wa kuuliza kuhusu historia yao ya ponografia.



## 2. Je, Ninapaswa Kujibu Vipi?

Wakati wewe na mtu uliye na miadi naye mnapoanza kushiriki hisia zenu za uaminifu, inaweza kuleta uponyaji. Ni muhimu kuwa makini juu ya mawazo yako mwenye-we na hisia pale matumizi ya ponografia yanapofichuliwa—inaweza kukufanya uwe mkosoaji, mwenye hasira, kushikwa na ganzi, au kuhisi kudanganywa. Lakini wakati huohuo, kufichua kwao kunaweza pia kuongeza uaminifu, huruma, upendo, na uelewa katì yenu. Fikiria hisia zao na za kwako mwenyewe wakati unapojibu.

## 3. Ni Kwa Jinsi Gani Ninasonga Mbele?

Kugundua kwamba mtu uliye na miadi naye anapambana na ponografia inapaswa kuwa sababu ya wasiwasí, lakini usisaliti uaminifu wao kwa kushiriki mapambano yao binafsi kwa watu wengine. Kuzungumza kwa ujasiri na askofu au mtaalamu, au, na rafiki au kiongozi wa kuminika kwa ruhusa ya mtu uliye na miadi naye, kunaweza pia kusaidia.

Wakati wa kuamua ikiwa utaendelea na uhusiano au la, unapaswa daima kutafuta mwongozo kutoka kwa Roho. Lakini mapendekezo yafuatayo yangeweza pia kusaidia:

- Waulize ni kiasi gani cha ponografia kime-athiri maisha yao na wapi wapo katika mchakato wa uponyaji. Wanahitaji kuwa wameonesha hamu yao ya kuondoa ponografia kutoka katika maisha yao kwa kuchukua hatua yoyote muhimu inayofaa.
- Tambua kwamba baadhi ya aina za matumizi



ya ponografia (kwa mfano, ponografia ya mtoto) ni kiashirio kikuu kwamba mtu huyo anahitaji msaada wa kitaalamu na anaweza kuwa hayuko salama.

- Tambua kwamba nguvu ya Upatanisho wa Mwokozi ni halisi. Unaweza kusamehe, na wanaweza kuponywa.
- Amua kwamba hutatafuta chochote zaidi ya uaminifu mkamilifu katika uhusiano wako na kustahili kufunga ndoa hekaluni.
- Elewa kwamba uponyaji utachukua muda. Kurudia tena kunaweza kutokea, na wale wanaojaribu kupona watahitaji uungaji wako mkono. Hii hujumuisha kufahamu vichocheo vyao (mambo yanayoweza kuwasababisha kugeukia ponografia) na kuwasaidia au kusaidia kuanzisha ulinzi unaofaa.
- Ikiwa uhusiano wako unaendelea kuelekea kwenye ndoa, hakikisha kwamba nyote wawili mnakubali kwamba ponografia haikubaliki na haiakisi uhusiano wa kujamiiiana wenyе siha.

Sehemu muhimu zaidi ya kusonga mbele ni kutegemea kile Roho Mtakatifu anachokupa msukumo kufanya, ambacho kinaweza kuwa chochote mbali na kuendeleza uhusiano ukiwa na uelewa kwamba matumizi ya ponografia lazima yasitishwe kwenye kusitisha uhusiano

lakini kuendelea kuunga mkono juhudzi za kubadilika. Chochote unachoamua, mtu uliye na miadi naye anapaswa kuelewa kwamba mambo yanaweza kubadilika kutegemeana na maendeleo yao au kutoendelea kwao katika kushinda ponografia.

## Kushirikiana Pamoja Kushinda Ponografia

Kushinda ponografia kunaweza kuchukua muda na kuwa vigumu, lakini kunawezekana. Na hatimaye, kushirikiana pamoja katika kuishinda kunaweza kui-marisha uhusiano wenu pale nyote wawili mnapopata uelewa wa kina wa Upatanisho wa Yesu Kristo na kujifunza kuungana mkono kuititia majoribu. Zingatia yafuatayo mnaposhirikiana pamoja kuishinda:

- Ukurasa wa mtandao wa Kanisa **overcoming pornography.ChurchofJesusChrist.org** unatoa rasilimali nyingi (ikijumuisha taarifa juu ya programu ya Kanisa ya kupona kutokana na uraibu) ambazo zinaweza kuwasaidia nyote wawili kutafuta mchakato huu wa uponyaji.
- Fikiria kuwa na mahala na muda maalumu ili kujadili ponografia ili kwamba isiwe fokasi ya uhusiano wenu. Pale mnapolizungumzia, usishushe hadhi au kusimanga. Uhusiano wako unapaswa kuwa sehemu salama ambapo nyote mnaweza kuhisi kuperendwa na kuungana mkono, si kuhojiwa au kushushwa hadhi.
- Matendo ya kiroho yanaweza kusaidia kutoa ulinzi dhidi ya majoribu. Himizaneni kuendeleza na kuimarisha tabia za mara kwa mara za kiroho—ikijumuisha usomaji wa maandiko wenye maana na kuabudu hekaluni (inapowezekana), kuitakasa siku ya Sabato, kuwatumikia wengine, kufunga mara kwa mara, na sala ya dhati—pamoja na ongezeko la hamu ya kuimarisha uhusiano wenu na Mwokozi na Baba wa Mbinguni. Uhusiano huo

unaweza kusaidia kupunguza nguvu ya ponografia katika maisha yenu. Ufuasi unatafutwa kote katika maisha, na nguvu tunayopata kama wafuasi wa Kristo itatusaidia kushinda changamoto zetu zote katika maisha, si tu ponografia.

- Ikiwa juhudzi zako mwenyewe hazioneshi kufanikiwa, usiogope au kuona aibu kutafuta msaada wa mtaalamu wa afya katika masuala ya uraibu wa ngono. Wanaweza kukusaidia kupata utambuzi zaidi kwenye kushughulikia matumizi ya ponografia na kukomesha visababishi vyake.
- Kumbukeni kwamba tumezungukwa na vyombo vya habari visivyoofaa ambayyo hutushawishi kufanya dhambi. Ikiwa mtu uliye na miadi naye ameridia tena, haraka jinsi gani wanarudi kwenye njia ni ishara nzuri ya kujitolea kwao kuondoa ponografia katika maisha yao. Lakini ikiwa utaanza kuhisi kama unapata msukumo zaidi wa kuona badiliko kuliko wao wanavyohisi, unapaswa kufikiria upya kuendeleza uhusiano wako.
- Ushawishi wako kwa mtu uliye na miadi naye una-weza kuwa na nguvu kubwa, lakini haupaswi kuwa sababu ya msingi kwenye badiliko lao la tabia. Hamu ya msingi ya kubadilika inatakiwa kutoka ndani, si kutoka kwako.

Zaidi ya yote, tafuta mwongozo kutoka kwa Baba wa Mbinguni na kumbuka kwamba daima kuna tumaini kuititia Mwokozi. Neema Yake inatosha kutuponya na kutubadilisha. Upatanisho Wake upo kwenu nyote kwa ajili ya kuwapa nguvu, kuwasaidia kusamehe. Hata hivyo, mtu anayepambana na ponografia anapaswa kutafuta usaidizi wa Mwokozi wao wenye ili kuishinda. Hakuna ye yote anayeweza kufanya hivyo peke yake. Kuwa na imani, na mtumainie Baba wa Mbinguni. Yeye atakuongoza katika hali yako ya kipekee. ■



## Simu za mkononi zina bei ghali hapa Chile,

lakini niliweka lengo mnamo 2016 kupata pesa za kutosha kununua simu. Kwa mwaka mzima, nilinunua pipi na *alfajores*\* kwa jumla na kuzi- uza kwa rafiki zangu shulenii. Nilitunza kila kitu nilichopata. Sikwenda kula nije ya nyumbani, na sikwenda kwenye sinema.

Sikutaka kuwaomba wazazi wangu simu. Nilitaka kuwa na uwezo wa kusema niliipata mwenyewe. Baba yangu alinitia moyo. "Carol, vizuri sana," angesema.

Nilijifunza mengi. Hakuna cha bure. Malengo yanahitaji juhudii, lakini hatupaswi kukata tamai. Wakati tunapopata vitu na kutambua juhudii inayotumika kuvipata, tunavithamini zaidi.

Nilijifunza kwamba ninapaswa kuamua kile ninachotaka kupata na wapi ninataka kwenda. Kama ninataka ndoa ya hekaluni, ninahitaji kwenda kanisani na seminari na baadaye chuo na kwenye shughuli za vijana waseja. Na ninahitaji kuwa na miadi na wavulana wenye kustahili. Kufikia malengo kunahitaji dhabihu sasa kwa kitu kizuri cha baadaye.

**Carol,** 15, Chile

\* Biskuti ya kitamaduni wa Amerika ya Kusini.



# VIJANA

## KATIKA SEHEMU HII



52

- 52 Kutoka kwenye Uonevu mpaka kwenye Ubatizo**  
Na Mzee Hugo Montoya

- 54 Takdiri ya Kiungu**  
Na Emma C.

- 56 Marafiki Walioshiriki Nuru Zao pamoja Nami**  
Na Mariana M. Lara

- 58 Kutokuwa Mwoga Kushiriki Ukweli**  
Na Michael R. Morris

- 62 Maswali & Majibu**

- 64 Neno la Mwisho: Jiwe Kuu la Pembeni la Imani Yetu**  
Na Rais Gordon B. Hinckley

PICHA NA LESLIE NILSSON

**N**ilipokuwa na umri wa miaka 17, nilikutana na shinikizo kubwa la kundi rika kwenye shule yangu ya upili. Marafiki niliokutwa nao hawakuwa na viwango sawa na vyangu. Mimi na rafiki zangu tulishiriki pamoja kwenye shughuli nydingi za kufaa kama kucheza mpira wa kikapu au mpira wa miguu. Lakini pia walikuanya pombe na kuvuta sigara—shughuli mbili ambazo sikufanya pamoja nao.

Siku moja kundi letu lilikuwa nje ya shule yetu tukisoma kwa ajili ya jaribio ambalo tungefanya baadaye siku hiyo. Pamoja nami walikuwa ni rafiki zangu wa karibu sana, Juan na Francisco (majina yamebadilishwa). Ghafla, mmoja akatoa kiberiti na sigara. Nilidhani rafiki zangu walikuwa wamechoka kusoma na walikuwa wamesahau kwamba nilikuwa pale. Niligundua sikuwa sahihi pale waliponigeukia na kusema, "Sasa ni wakati wa Hugo kujifunza jinsi ya kuvuta."



# KUTOKA KWENYE UONEVU MPAKA KUBATIZWA



**Na Mzee  
Hugo Montoya**

Wa Sabini

Kabla hata sijapata nafasi ya kujibu, Juan na Francisco walinirukia na kunishika mikono yangu, mmoja kila upande. Walishusha mikono yangu pale mmoja aliposukuma sigara katikati ya midomo yangu. Mwili wangu haraka ulikataa hili, na nilitema sigara chini, mbali na mimi. Punde baada ya hilo, nilihisi mvumo wa ngumi iliyokazwa ikiungana kwa pembe mraba na mfupa wangu wa shavu. Walinithia, wakisema, "Tunawasha sigara tena, na utajifunza jinsi ya kumeza moshi. Usiiteme chini. Ukiitema, hatma yake haitakuwa nzuri."

Dakika ile, nilijua nilikuwa matatizoni. Niliumba macho na kusema sala ya haraka nikiomba aina fulani ya usaidizi. Punde tu nilipohitimisha sala, gari ya mwalimu wetu ilifunga breki na kusimama karibu yetu. Mwalimu wetu alitoka nje ya gari na kutuuliza kile tulichokuwa tukifanya. Rafiki zangu waliniachia. "Tunajiandaa kwa ajili ya jaribio," walimhakikishia mwalimu. Tulikwenda shuleni na kufanya jaribio, na suala hilo liliisha.

Licha ya uzoefu huo kuwa mgumu, niliwasamehe rafiki zangu kwa kile wali-chofanya. Nilijua hawakuelewa viwango vyangu na uamuzi wangu kuishi Neno la Hekima, hivyo niliwasamehe na kuchagua kutokuwa na hisia mbaya juu yao. Nilipohitimu shule, nilienda misheni lakini niliendelea kuwasiliana na Juan na Francisco. Niliwaandikia barua mara kwa mara nikishiriki nao injili na ushuhuda wangu wa Yesu Kristo. Niliwaalika watubu

na wahudhurie kanisani. Kwa mshangao wangu mkubwa, mmoja wao alihudhuria.

Nilikuwa nimewaalika rafiki zangu mara kwa mara kwenye mikutano ya Jumapili kabla, lakini hakuna aliyekubali mpaka sasa. Japokuwa sikuweza kuhuduria pamoja na Juan, kaka zangu na baba yangu walikuwepo kumsaidia na kumpa urafiki. Familia yangu walimkubali,

nia ya kweli kwa wengine; tabasamu na acha wajue kuwa unawajali.<sup>1</sup> Hiki ndicho Bwana alichonisaidia mimi kufanya kwa Juan na Francisco. Kwa sababu ya hilo, nina marafiki wakuu wawili ambao nime-wahi kuwajua, na sasa tunafanya kazi pamoja kuunga mkono ufalme wa Mungu kama waumini wa Kanisa.

Daima inua juu viwango nya Kanisa,

### *Urafiki wako na mfano wa uadilifu utawabariki rafiki zako na vizazi vijavyo.*

na Juan alijihisi vizuri kanisani. Alianza kubadiliwa kidogo kidogo mpaka alipofanya uamuzi wa kubatizwa. Nilikuwa na msisimko kwa ajili yake na hata kuwa na msisimko zaidi wakati aliponiambia kwamba alikuwa amejifunza kumpenda Yesu Kristo kwa sababu ya barua zangu. Niliporudi nyumbani kutoka misheni yangu, nilikuwa karibu pia na Francisco, na baada ya muda, yeye na mke wake pia walibatizwa. Leo, Juan na Francisco bado ni rafiki zangu wa karibu.

Matukio haya yamewekea alama maisha yangu. Nimejifunza kwamba njia nzuri zaidi ya kuleta ushawishi katika maisha ni kuishi kwa uadilifu, kuwapenda wengine, na kufikia. Kijitabu cha *Kwa Nguvu ya Vijana* kinasema, "Ili kuwa na marafiki wema, kuwa rafiki mwema. Onyesha

hata kama upo katika hali ngumu kama niliyokuwa nayo. *Kwa Nguvu ya Vijana* inaelekeza, "Unapojitahidi kuwa rafiki kwa watu wengine, usipuuze viwango vyako. Kama rafiki zako wanakuomba kufanya mambo ambayo si sahihi, kuwa wa kwanza kusimamia ukweli."<sup>2</sup> Hata kama inaonekana kama kila mmoja anafanya kile kilicho tofauti na amri, baki imara kwa sababu mfano wako zako wana-weza kuufikiria wakati wa nyakati zao za uhitaji. Katika baadhi ya matukio kama langu, urafiki wako waweza kuwa jambo ambalo linawasaidia wao kujifunza, kutubu, na kuongoka. ■

#### **MUHTASARI**

1. *Kwa Nguvu ya Vijana* (2011), 16.
2. *Kwa Nguvu ya Vijana*, 16.

# Takdiri ya Kiungu

*Rafiki yangu daima alikuwa na furaha muda wote.*

*Ni nini kingeweza kumuudhi?*

## **Na Emma C.**

**N**atokea Ufaransa, lakini mimi na dada yangu tuliishi kwa mwaka mmoja mashariki ya Marekani kama wanafunzi wa kubadilishana. Kipindi hicho, tulikutana na watu wengi lakini mmoja ambaye aliacha msukumo mkubwa kwangu alikuwa msichana aliyeitwa Destiny. Alikuwa mmoja wa marafiki zangu niliowapenda zaidi. Tulifanya mambo mengi pamoja, wakati wa shule na baada ya shule na pamoja na dada yangu. Destiny daima alikuwa mwenye furaha. Hicho ndicho kitu nilichopenda zaidi kwake.

Kisha siku moja nilimuona katika hali ya wasi-wasi ambayo sikuwahi kumuona nayo kabla. Nilimwuliza nini lilikuwa tatizo. Alisema hakupenda kuliongelea. Kisha niliona karatasi mkononi mwa-ke. Niliichukua na kuisoma.

Mtu fulani alikuwa amemwandikia vitu vibaya visivoaminika. Ujumbe wa siri ulisema alikuwa mbaya, kwamba hakuna aliyempenda, kwamba hakuwa na lengo lolote la kuwa hai, na kwamba alipaswa kujua. Sikuweza kuamini mtu kama yeze angeweza kushambuliwa vile. Iliniathiri sana kujua maumivu aliyokuwa akipitia.

Tangu hapo, nilifanya juhudu kubwa zaidi kuwa rafiki wa Destiny—si tu kutumia muda pamoja naye, bali daima kuwepo kwa ajili yake, na hasa kuwa mkweli. Nilimwelezea kwamba yeze alikuwa binti wa Mungu, aliyebarikiwa na asili takatifu, aliystahili kupendwa na mwenye uwezo wa mambo makubwa.

Ni vigumu kujaribu kujipenda mwenyewe wakati wengine wanapokutendea vibaya na kukosoa. Nilipo-kuwa na urafiki na Destiny, nilijifunza kuwa wakati mwiningine njia nzuri ya kuwasaidia wengine ni kuwapenda tu na kuwasaidia kujua wao ni akina nani hasa.

Mwishoni mwa mwaka, nilipopaswa kurudi Ufaransa, Destiny aliniambia jambo ambalo daima nitalithamini. “Emma,” alisema, “umeniokoa. Kabla hujaja, nilitaka kujiuia. Lakini wewe na dada yako mmenisaidia sana, kwa kujali tu. Leo ninajipenda, na ninawapenda.”

Kuna watoto wengi shulenii wanaovumilia ukatili, ambao wanatendewa vibaya au kutengwa. Tafuta njia ya kuwafikia. Zungumza nao, wafikirie, kuwa mkarimu kwao. Ndicho ambacho Mwokozi angefanya, na wakati mwiningine kusema tu halo au kutabasamu kunawenza kubadili kila kitu. ■

*Mwandishi anaishi Ufaransa.*



**Na Mariana M. Lara**

**N**ilikuwa nikiishi na mama yangu kwenye mji mdogo huko Mexico ambapo watu wote walifahamiana. Nilijua mema na mabaya, lakini nilikuwa nimekanganyikiwa na nilikuwa msichana pekee anayeshiriki kikamilifu katika mji wote.

Nilitaka kuwa sehemu ya jamii, hivyo nilifanya kitu kimoja ambacho kilikuwa na maana hapo nyuma: kuwa na mpenzi. Hili nilikuwa kosa la kwanza nililoanza kufanya. Nilianza kujingiza kwenye makundi rika na kuamini kwamba nilikuwa mkubwa vya kutosha kufikiria kwa ajili yangu mwenyewe, ambayo ilimaanisha kuwa msichana asiyeshiriki kikamilifu ambaye aliihi gizani.

Niliishi gizani kwa mwaka mmoja, kwa kila siku iliyopita kuwa yenye giza zaidi. Maamuzi yangu mabaya yalipelekea

mizozo na familia yangu, na nilitambua nisingweza kuendelea kuishi nao. Lakini haikuwa mpaka kifo cha rafiki wa karibu Mtakatifu wa Siku za Mwisho ambapo nilitambua kuna kitu kilikuwa kinakosekana. Kwa bahati mbaya, nilimlaumu Mungu pamoja na injili. Niliacha kuamini kwamba baraka zilikuja kutokana na kuwa mtiifu. Nilijua kwamba ikiwa nisingeama kuanza kuishi injili, ningeendelea kupuuzia muunganiko wangu na Kanisa na kuendelea kuishi katika namna ya ulimwengu.

Nilikuwa nimekaa juu ya kitanda changu kwenye chumba chenye giza, nikilia na kujionea huruma mwenyewe wakati nilipotambua kwamba

nilikuwa na woga—woga wa kuwa pale peke yangu bila mtu wa kuzungumza naye, woga wa kutoweza kurekebisha maovu yote niliyokuwa nimetenda, woga kwamba hakuna yeyote ambaye angensi samehe, hasa Mungu.

Hatimaye, nilihamia Minnesota, Marekani, pamoja na babu na bibi yangu, ambao si waumini wa Kanisa. Baba yangu wa kambo alisafiri pamoja nami, na Jumapili yangu ya kwanza huko, tulikwenda



# MARAFIKI Ambao **WALISHIRIKI** **NURU** Yao pamoja Nami

Kanisani, lakini kwa ajili ya mukutano wa sakramenti tu. Kuelekea hitimisho la mukutano nilikuwa tayari nimekwisha amua kuondoka Kanisani, lakini kwa mshangao wangu, wakati tulipokuwa tukielekea kwenye gari, tulimwona askofu akitukimbilia. Alituuliza maswali machache na kutualika kuhudhuria tena Jumapili iliyofoata—na tulifanya hivyo.

Jumapili iliyofoata, wakati mukutano wa sakramenti ulipokuwa ukimalizika, kabla sijasimama, nilikuwa nimezungukwa na wasichana kutoka kwenye

kata—wasichana ambao wangenisaidia kubadili maisha yangu.

Ghafla nilikuwa nimeingia kwenye ulimwengu tofauti kabisa: ulimwengu uliokuwa na askofu na rais wa Wasichana ambao walinjali na, zaidi ya yote, wasichana ambao walijaribu kuishi injili kila siku, waliojitatihidi kuishi viwango vya juu na kusimamia kilicho sahihi. Waling'ara sana kiasi kwamba wange-weza kuangaza njia mbele yangu.

Hapo ndipo nilipotambua kile nilichopaswa kufanya: "Nuru [yangu] na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo [yangu] mema, wamtukuze Baba [yangu] aliye mbinguni" (ona Mathayo 5:16). Na hivyo nilianza kwa kwenda kanisani na

kwenye shughuli za Mutual kila wiki, kusoma Kitabu cha Mormoni na kuomba kila siku, kuvala kwa staha, kutumia lugha nzuri, kwenda hekaluni, na kujiandaa kupata baraka yangu ya baba mkuu.

Nilikuwa nimebadilika kikamilifu, lakini sikutambua hilo mpaka kwenye kambi ya Wasichana, ambapo nilihisi Roho Mtakifu na kugundua kwamba nilikuwa na ushuhuda—ushuhuda ambao ungenikumbusha kwamba Mungu ananipenda, kwamba ana mpango kwa ajili yangu, na kwamba hataki mimi niwe peke yangu. Ushuhuda angavu na imara kwamba ulinibadili. Ushuhuda wa kushiriki na kuangaza si tu njia yangu bali ya wengine. Ushuhuda ambao hauna woga kung'ara kwenye giza. ■

*Mwandishi anaishi Baja California, Mexico.*

*Nilikuwa nikihisi  
woga na mpweke.  
Kisha nilihamia  
nchi nyingine na  
kwenda kanisa-  
ni kwa mara ya  
kwanza baada ya  
muda mrefu.*



# KUTOKUWA MW



# OGA KUSHIRIKI UKWELI

*Akiwa amejiami na ushuhuda wa injili pamoja na baraka za injili hiyo, Fabian hakuruhusu umri wake mdogo kumzuia kuwa mmisionari muumini mwenye nguvu, asiye na woga.*

**Na Michael R. Morris**

Majarida ya Kanisa



Jua linazama huko Las Tomas, ujirani ulio-jengwa juu ya mteremko wenyewe mchanga ukiangalia Antofagasta. Chini, mianga inaanza kung'ara pale siku inapomalizika katika jiji hili la bandari huko Chile ya kaskazini.

Ni Jumamosi usiku, na Fabian H. Mwenye mia-ka 13 angeweza kuwa akifurahia pamoja na rafiki zake. Lakini Fabian, muumini mpya wa Kanisa, badala yake anachagua kutumia jioni pamoja na wamisionari wa muda wote. Ni wakati wa "kusaidia kukusanya Israeli."<sup>1</sup>

Kati ya waumini wote waliojitelea waliofanya kazi na Kellen VanNatter na Jordan Shelton wakati wa umisionari wao wa muda wote huko Chile, Fabian anang'aa kuliko wengine.

"Ikiwa alikuwa na muda, alikuwa nje pamoja na sisii tukifanya kazi ya umisionari," anasema Kellen. "Wakati likizo ya majira ya joto ilipoisha, alikuwa na huzuni si kwa sababu alipaswa kurudi shule bali kwa sababu hakuwa na muda wa kutosha kwenda na sisii."

Jordan, aliyekuwa mmisionari mwenza wa Kellen kwa miezi kadhaa, anaongeza, "Fabian yawezekana alikwenda pamoja nasi mara nne au tano katika wiki—kila wiki—wakati tulipotumikia pamoja Antofagasta. Alikuwa muumini mmisionari bora tuliyewahi kufanya naye kazi."

Ni nini kinamfanya mvulana kuwa radhi kufanya kazi ya umisionari licha ya dharau kutoka kwa wanafunzi wenzake na kupuuzwa na watu asio-wajua? Kwa Fabian, jibu liko katika baraka ambazo yeye na familia yake wamepata tangu walipoikubali injili—baraka anazotaka kushiriki na wengine.

### "Shangwe Isiyoelezeka"

Fabian alianza kujifunza masomo ya wamisionari muda mfupi baada ya wamisionari wa muda wote kuja na kugonga. Bado anakumbuka mkutano wake wa kwanza wa sakramenti.

"Sikumfahamu yeyote nilipoingia ndani ya jengo la ibada, hivyo nilikuwa kidogo mwoga," anasema. "Lakini nilihisi kitu fulani cha ajabu.



"Yeye daima hushiriki uzoefu wake *mwenyewe* binafsi—kama jinsi alivyohisi wakati alipokwenda kanisani

Nilihisi kama nilikuwa Kanisani kwa miezi au miaka.

Wakati wa ubatizo wake wiki chache baadaye, "nilihisi shangwe isiyoelezeka wakati wa kuzamishwa ndani ya maji na kuinuliwa juu tena. Nilihisi kama mtu mpya, nikijua kwamba nilikuwa ninakwenda kumfuata Yesu Kristo na kufanya kadiri niwezavyo kutii amri Zake."

Pale wazazi wa Fabian ambao hawakuwa na ndoa, Leonardo na Angela, walipojunga na kijana wao wakati wa masomo ya wamisionari, walijifunza kuhusu ndoa ya hekalu na familia za milele. "Wiki moja baadaye, baba yangu alipanga tarehe ya ndoa," anasema Fabian. "Mama yangu alifurahi sana."

Miezi minne baada ya Fabian kujiunga na Kanisa, Angela alimfuata kwenye maji ya ubatizo. "Hiyo ilikuwa ni baraka ya kupendeza," anasema.

Baraka zingine haraka zilifuata. Leonardo, ambaye alikuwa amebatizwa akiwa mdogo, alirudi kwenye kushiriki kikamilifu Kanisani. Kujifunza injili kukawa jambo kuu nyumbani kwao. Wanafamilia wakakua pamoja. Leonardo alipata kazi ya kudumu. Na Fabian alipokea Ukuhani wa Haruni.

"Ninapenda kuwa na ukuhani ili kumba niweze kuitisha sakramenti kwa waumini wa kata na kuwasaidia kufanya upya maagano yao," anasema Fabian. "Nina furaha hasa wakati ninapopitisha kwa familia yangu na kwa wazee walionifundisha. Mtazamo wa kujivunia baba yangu anaonipa anaponiona nikipitisha sakramenti unanifanya niwe na furaha sana."

### **"Hilo Lingekuwa la kupendeza Sana"**

Fabian alianza kufanya kazi ya umisionari kabla hata hajabatizwa.

"Niliwaambia watatu kati ya rafiki zangu kwamba nitabatizwa. Wawili kati yao walikuja," anasema. "Ninapenda kushiriki injili ili kwamba rafiki zangu waelewe kile tunachoamini na kile tunachofanya kanisani na ili kwamba waweze kujifunza injili, kubatizwa, na kuwa na maisha ya furaha. Ningekuwa na furaha ikiwa mmoja wao angebatizwa na kuwa mmoja wa washiriki wa akidi yangu. Hilo lingekuwa la kupendeza sana."

Fabian anaenda shulen na Kitabu cha Mormoni, na hubeba vipeperushi ya wamisionari kuwapa rafiki zake.

Anafurahia kujibu maswali kuhusu Kanisa na kuwaalika marafiki kwenye mikutano ya Jumapili na usiku wa shughuli ya vijana. Na haogopi kuwaendea watu mtaani na, kama wamisionari walivyomfundisha, kuwaalika kujifunza kuhusu Kanisa na kuijandaa kwa ajili ya ubatizo.

"Fabian hajali ikiwa mtu anafikiria yeye ni wa ajabu kwa kushiriki ushuhuda wake," anasema Kellen. "Anajua anafanya jambo sahihi. Anajua kwamba mambo ya kiroho ni muhimu kuliko kitu kingine chochote."

Wakati Fabian anaposhiriki ushuhuda wake, Jordan anasema, anavuta nguvu kutoka kwenye uongofu wake, upendo wake wa injili, na baraka zake.

"Aliona baraka zilizokuja kwa familia yake, ndicho kitu kinachompa msukumo wa kuwa shujaa na mwenye kujiamini katika kushiriki injili na rafiki zake," Jordan anasema. "Kuna wakati alikuwa akishuhudia kwa mchunguzi wa kanisa kuhusu vile ilivyokuwa baraka kwa wazazi wake kufunga ndoa lakini jinsi iliyokuwa vigumu kwake kusubiri kwa miezi minne baada ya ubatizo wake kwa ajili ya mama yake kubatizwa. Hisia zake zilimzidi, na alitokwa machozzi. Kisha alishuhudia kwamba ikiwa



Haishangazi kwamba mojawapo ya lengo kubwa la Fabian ni kuwa mmisionari wa muda wote baada ya kuhitimu shule ya upili.

"Ninataka kushiriki ukweli pamoja na wale ambao hawaufahamu," anase-ma. "Ninataka kuwaalika kuosha dhambi zao. Ninataka kuwafundisha jinsi

wanavyoweza kuwa familia ya milele. Ninataka kuwaalika wawe na furaha sasa na kuishi katika hali ya furaha isiyo na mwisho baada ya maisha haya." ■

#### MUHTASARI

1. Russell M. Nelson, "Tumaini la Israeli" (mkutano wa vijana wa ulimwengu wote, Juni 3, 2018), [HopeofIsrael.ChurchofJesusChrist.org](http://HopeofIsrael.ChurchofJesusChrist.org).

kwa mara ya kwanza na jinsi anavyohisi anaposoma Kitabu cha Mormoni.

tutatii amri, Mungu atatupatia uangalizi.


Ushuhuda wa Fabian unamfanya kuwa muumini mmisionari mwenye nguvu, anaongeza Kellen.

"Yeye hayuko kama, 'Ee, nilisikia mtu anasema hili kanisani.' Badala yake, yeye daima hushiriki uzoefu wake *mwenyewe* binafsi—kama jinsi alivyohisi wakati alipo-kwenda kanisani kwa mara ya kwanza na jinsi anavyohisi anaposoma Kitabu cha Mormoni. Ni wa hakika na halisi."

#### "Daima Ninajisikia Vizuri Zaidi"

Kwa Fabian, kushiriki injili huleta baraka nyiningine.

"Wakati mwingine mambo mabaya huto-ke shulen, lakini kisha wamisionari huja kugonga mlangoni kwangu na kuuliza ikiwa ningekuwa tayari kuwasaidia kufundisha," anasema. "Baada ya kwenda nao, ninahisi kana kwamba sina matatizo tena. Daima ninahisi vizuri zaidi wakati ninapokwenda nao, ninaposoma maandiko pamoja nao, na kuwasaidia kushiriki injili. Kushiriki injili na hadithi ya uongofu wangu huimarisha ushuhuda wangu. Na kufundisha injili kunanipa fursa ya kuwa mfano kwa wengine, ikijumui-sha mdogo wangu wa kike."



*Fabian anajiandaa kwa ajili ya jioni ya kufundisha injili pamoja na Mzee Kellen VanNatter (juu, katikati) na Jordan Shelton (juu, kulia).*



#### HAKUNA KITU MUHIMU ZAIDI

"Wapendwa vijana wangu wa kipekee, mliletwa duniani katika wakati huu hasa, wakati muhimu zaidi katika historia ya ulimwengu, kusaidia kukusanya Israeli. Hakuna *chochote* kinachotokea katika dunia hii sasa ambacho ni muhimu zaidi ya hicho. Hakuna *chochote* chenyeh matokeo makubwa. *Hakuna kabisa.*

"Kukusanya huku hakuna budi *kumaanisha* kila kitu kwenu. Hii ni kazi amba-yo kwayo wewe ultumwa duniani."

Russell M. Nelson, "Tumaini la Israeli" (mkutano wa vijana ulimwenguni kote, June 3, 2018), 2018, [HopeofIsrael.ChurchofJesusChrist.org](http://HopeofIsrael.ChurchofJesusChrist.org).

# “Ninapataje marafiki ambao wana viwango vizuri?”

*“Huruma ya marafiki walio kama Kristo hugusa kwa kina na kubadili maisha yetu. Tunapaswa kukumbuka vyema kwamba Bwana mara nyingi hutuma ‘baraka kutoka juu, kupidia maneno na matendo ya wale wanaopenda.”*

Mzee Joseph B. Wirthlin (1917–2008) wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, mkuu wa Oktoba 1997.



### Ukarimu Ni Muhimu

Waonyeshe upendo na kuwa mkarimu. Onyesha kwamba unawajali na unajali furaha yao. Ikiwa hawaonyeshi kwamba wanakujali na si wakarimu, pengine hutataka kuendelea kutafuta urafiki huo.

*Madi B., miaka 15, Arizona, Marekani*



### Shiriki injili

Unaweza kupata marafiki wapya wenye viwango vizuri kwa kwenda kufundisha pamoja na wamisionari. Wanawajua vijana kadhaa wanaohitaji rafiki Kanisani.

*Mzee Quintanilla, miaka 20, misheni ya Barbados Bridgetown*

### Omiba kwa ajili ya Rafiki Zako

Ninaomba sana ili kuona ikiwa rafiki zangu ni marafiki sahihi ambao wanawenza kunisaidia kuinua viwango vyangu na ushuhuda wangu wa Yesu Kristo.

*Imanol M., miaka 18, Chihuahua, Mexico*



### Mungu Atakusaidia

Nimegundua kwamba  
ikiwa nitaenda nje ya  
njia yangu kutafuta watu  
ambao wanaonesha nuru  
ya Kristo, hilo limeleta tofauti kubwa.  
Baba wa Mbinguni anafahamu hamu  
yako na ikiwa utafanya sehemu yako,  
ndipo Yeye atajibu maombi hayo.  
*Olivia T., miaka 18, Utah, Marekani*

### Ishi Viwango Vyako

Kuwa mfano wa kuishi viwango vyako.  
Na ikiwa una marafiki ambao hawana  
viwango sawa na vyako, waonyeshe kwa-  
mba wao ni wa kipekee mbele za Mungu.  
Yesu alifundisha kila mmoja na kuwafu-  
ndisha kufuata njia Zake.

*Bernard B., miaka 19, Palawan, Ufilipino*

*Majibu yanakusudiwa kwa ajili ya msaada na  
mtazamo, si kama matamko rasmi ya mafundisho  
ya Kanisa.*



## Nini mtazamo wa Kanisa juu ya mazingira?

Neno la msingi katika kuelewa mtazamo wetu juu ya mazingira ni *usima-mizi*. Haimaanishi kwamba watu wanamiliki dunia na wanaweza kuitumia vyovyote wanavyopenda bali tunawajibika kwa jinsi tunavyotumia rasilimali zake (ona Mafundisho na Maagano 104:13–15). Japokuwa “viko vya kutosha na kubaki” (Mafundisho na Maagano 104:17), Mungu anataka tutumie rasilimali za dunia kwa hekima (ona Mafundisho na Maagano 59:20).

Mungu aliumba dunia na kutangaza uumbaji Wake kuwa “mwema sana” (ona Mwanzo 1:1, 31). Dunia hii iliumbwa kuwapa hifadhi watoto wa Mungu kama sehemu ya mpango Wake wa wokovu. Dunia haina budi kusafishwa na kupokea utukufu wa selestia (ona Mafundisho na Maagano 88:18–19).

Mungu aliumba dunia si tu itumike bali pia ya kupendeza. Vitu vya dunia “vimefanywa kwa faida na matumizi ya mwanadamu, kwa kuridhisha jicho na kufurahisha moyo,” vilevile kuchangamsha nafsi” (Mafundisho na Maagano 59:18–19).

Tunapaswa kumheshimu Mungu kwa kutambua uumbaji Wake, kuonye-sha shukrani kwa uumbaji huo, na kujitahidi kuufanya kuwa wa kupendeza. Tunapaswa kutunza rasilimali, kulinda asili, na kuepuka uchafuzi na takataka.

### Unafikiria Nini?

“Ni kwa jinsi gani ninaweza  
kushinda hisia za upweke?”

Wasilisha jibu lako na, ukipenda, picha ya  
ubora wa hali ya juu kabla ya Novemba  
15, 2019, kwenda liahona.Churchof  
JesusChrist.org (bofya “Wasilisha Makala  
au Maoni”).

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya  
urefu au ufanuzi.

# Jiwe Kuu la Pembeni la Imani Yetu

**Na Rais Gordon B. Hinckley (1910-2008)**

Rais wa 15 wa Kanisa

---

**K**atika kila hekalu jipya tuna sherehe ya jiwe la pembeni ikienda sambamba na utamaduni ambaao una kiini katika nyakati za kale. Kabla ya matumizi ya jumla ya saruji, kuta za msingi wa jengo ziliwekwa kwa mawe makubwa. Mtaro ungechimbwa, na mawe yangewekwa kama msingi imara. Kuanzia kwenye alama ya mwanzo, ukuta wa msingi ungejengwa katika uelekeo mmoja kuelekea jiwe la pembeni; kisha pembe ingekunjwa na ukuta kujeengwa kuelekea pembe inayofuata, ambapo kutoka hapo jiwe lingine lingewekwa, ambapo kutoka hapo ukuta ungejengwa kuelekea pembe inayofuata, na kutoka hapo kuelekea sehemu ya mwanzo. . . . Jiwe la mwisho lilisemekana kuwa jiwe kuu la pembeni, na uwewkaji wake ulikuwa sababu ya kusheherekeea sana. Jiwe hili la pembeni likiwa mahala pake, msingi ulikuwa tayari kwa ajili ya jengo kusimama. Hivyo analojia ambayo Paulo alitumia kuelezea Kanisa la kweli:

"Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu;

"Na mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni;

"Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana" (Waefeso 2:19-21).

Tunayo mawe ya pembeni ya msingi ambayo juu yake Kanisa hili kuu la siku za mwisho limeanzishwa na Bwana na kujengwa, "likikaa barabara pamoja." Mawe hayo ni muhimu hasa kwa kazi hii, msingi hasa, nanga ambazo juu yake linasimama. . . . [Lakini] ninataja jiwe kuu la pembeni, ambaye tunamtambua na kumheshimu kama Bwana Yesu Kristo. . . .

Yeye ni jiwe kuu la pembeni la Kanisa ambalo linabeba jina Lake, Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Hapana jina jingine walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo (ona Matendo ya Mitume 4:12). Yeye ni sababu ya wokovu wetu, mtoaji wa uzima wa milele (Ona Waembrania 5:9). Hakuna ye yeyote aliye sawa Naye. Kamwe hajawahi kuwepo. Kamwe hatakuwepo. Shukrani ziwe kwa Mungu kwa ajili ya zawadi ya Mwana Wake Mpandwa, ambaye aliutoa uhai Wake kwamba sisi tuweze kuishi, na ambaye ni jiwe la pembeni, lisilohamishika la imani yetu na Kanisa Lake. ■

*Kutoka katika hotuba ya mkuu wa Oktoba 1984.*

# Mawe Manne ya Pembeni ya Kanisa

Rais Gordon B. Hinckley alishuhudia kwamba Yesu Kristo ni jiwe kuu la pembeni la imani yetu. Alifundisha

pia kwamba kuna mawe mengine ya msingi ambayo Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho limejengwa juu yake.



## Bwana Yesu Kristo

*Bwana na Mwo-kozi wetu. Jiwe kuu la pembeni ambalo juu yake imani yetu na Kanisa vimeje-ngwa.*



## Ono la Kwanza

*Lilifungua kazi ya ajabu ya urejesho.*



## Kitabu cha Mormoni

*Kinazungumza kama sauti kutoka mavumbini kikiwa na maneno ya manabii waki-shuhudia juu ya Mwokozi wa wana-damu.*



## Ukuhani

*Kupitia nguvu na mamlaka yake, wanaume wanatenda katika jina la Mungu katika kuhudumia masu-la ya ufalme Wake.*



VIJANA WAKUBWA

**JE, MWENZA WAKO  
MTEGEMEWA ANA TATIZO  
LA PONOGRAFIA?**

*Kuna tumaini na msaada. Hapa ni  
jinsi unavyoweza kusonga mbele  
kwa imani.*

42



VIJANA

**USHAWISHI WA  
MARAFIKI WAZURI**

52-57,  
62

NJOO, UNIFUATE

**WAEFESO 2: NI NINI  
MAWE YA PEMBENI  
YA KANISA?**

64

KANISA LA  
**YESU KRISTO**  
LA WATAKATIFU  
WA SIKU ZA MWISHO

# Rafiki



Sehemu ya watoto ya *Liahana*, inayochapishwa na Kanisa La Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Halo kutoka  
**D. R. Congo!**  
Ona kurasa R4-R7



**Na Rais  
Dallin H. Oaks**

Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza

# Kuwapenda Wengine kama Yesu Anavyotupenda



**Y**esu aliwapa wafuasi wake amri kuu: "Mpenda-ne, kama niliviyowapenda ninyi" (Yohana 15:12). Kama wafuasi wa Kristo, tunapaswa kuishi kwa amani na wengine. Hiyo hujumuisha watu ambao hawaamini mambo sawa na yale tunayoamini.

Hapa kuna baadhi ya njia tunazoweza kuwapenda wengine kama Mwokozi anavyotupenda:

- Kuwa mkarimu kwa watu ambao wako tofauti.
- Onyesha heshima kwa imani zao.
- Kamwe usimuonee au kumtukana yeyote.
- Kuwa msikilizaji mzuri.

- Kuwa mpole. Usibishane kwa hasira.
- Simamia kwenye kilicho kweli.
- Waambie wengine kuhusu injili kwa njia ya unyenyekevu. "[Zungumza] ukweli katika upendo" (Waefeso 4:15).


Amri ya Mwokozi wetu ya kupendana kama Yeye anavyotupenda pengine ni changamoto yetu kuu. Ninaomba kwamba tuweze kujaribu kuonyesha upendo katika yote tunayofanya. ●

*Imetoholewa kutoka "Kuwapenda Wengine na Kuishi kwa Utofauti," Liahona, Nov. 2014, 25–28.*

# Manabii na Mitume

Maandiko yanasema Kanisa "limejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembedi. (Waefeso 2:20). Hii humaanisha kwamba Yesu Kristo anaongoza Kanisa kuitia manabii na mitume leo.

Paka rangi picha za watu wanaozungumza katika mkutano mkuu. Au paka rangi picha zao baada ya mkutano wakati unapozungumza na familia yako kuhusu hotuba mlizozipenda sana. Paka rangi moyo kila mara unaposikia mtu akimtaja Yesu. Yeye anakupenda!



Ukurasa huu unaunga mkono ukurasa wa 155 wa Njoo, *Unifuate—Kwa Ajili ya Watu Binafsi na Familia*.

# Umbali wa Sala Tu

*Prodi alikuwa  
mwoga kurudi  
kulala. Vipi ikiwa  
angepata ndoto  
nyingine ya kutisha?*



## **Na Lucy Stevenson**

Majarida ya Kanisa

*“Sali, Yeye yupo”*

(Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 12).

**P**rodi aliketi kitandani kwa mshtuko. Moyo wake ulikuwa ukidunda kwa kasi.

Mvua ilinyesha kwa vishindo vidogo vidogo juu ya paa wakati alipokuwa ameketi gizani. Aliweza kusikia maji yakidondoka kutoka kwenye mtini wa Kiafrika nje ya dirisha lake, na hewa ilikuwa nzito na yenze joto. Prodi alivuta pumzi ndefu na kujaribu kutulia. Ilikuwa ni ndoto tu.

Alitambaa kutoka kitandani na kuchungulia chumbani kwa wazazi wake. Mama na baba walikuwa wamelala kwa utulivu. Dada yake mdogo, Célia, alikuwa amejikunja ndani ya kitanda chake pia. Kila kitu kilikuwa SAWA. Familia yake ilikuwa salama.

Prodi alirudi kitandani na kujaribu kusinzia tena. Alijirusha na kugeuka, kisha kujirusha na kugeuka tena na tena. Alijuwa ndoto yake haikuwa kweli, lakini ilikuwa ya kuogopesha! Japokuwa alikuwa amechoka, aliogopa kusinzia tena. Vipi ikiwa angepata ndoto nyngine ya kutisha?

Prodi alilala chali na kutazama dari. Alijaribu kufikiria mawazo ya furaha. “Baba wa Mbinguni, je, kweli upo? Na je, unasikia na kujibu sala ya kila mtoto?” Wimbi la upepo lilikuja juu ya Prodi wakati alipofikiria maneno ya wimbo wake alioupenda sana wa msingi. Dada Kioska alikuwa amewafundisha kwamba Baba wa Mbinguni



daima alikuwa akiwalinda.

Wangeweza kusali kwake wakati wowote, mahala popote. Prodi alijua nini cha kufanya.

Alishuka kitandani na kupiga magoti ili kusali.

“Baba mpendwa wa Mbinguni,” alisali,

“ninaogopa sana. Tafadhali iweke salama familia yangu. Na tafadhali nisaidie nipate usingizi na nisipate tena ndoto mbaya.”

Prodi alimaliza sala yake na kurudi kitandani. Mwili wake ulitulia, na akili yake ilihisi amani. Punde alisinzia.

Kulipokucha asubuhi, Prodi aliamshwa na juu lenye joto lililong’ara kupitia dirishani. Aliweza kusikia masufuria yakigongana jikoni na aliamka kumtafuta Mama.≈Célia alikuwa mezani akila kiporo cha mihogo. Mama alikuwa akipasha mihogo mingine kwa ajili yake pia.

“*Habari ya asubuhi*,” Mama alisema. “Ulilalaje?”

“Nilikuwa na ndoto ya kutisha,” Prodi alisema. “Lakini kisha nikasali. Baba wa Mbinguni alinisaidia kuhisii salama.”

“Pole kwa kuwa na ndoto mbaya,” Mama alisema. Alimkumbatia Prodi kwa muda mrefu. “Lakini ninafurahi ulisali. Inaonekana kama vile Baba wa Mbinguni kweli alikusaidia.”

“Ni kweli,” alisema Prodi. “Niliweza kusinzia tena, na sikuwa tena na ndoto mbaya.” Prodi alimkumbatia Mama kwa nguvu. Alikuwa na furaha kujua kwamba licha ya woga aliohisi, Baba wa Mbinguni alikuwa umbali wa sala tu. ●

**Funua ukurasa kukutana na mvulana kutoka kwenye hadithi hii!**

# Halo kutoka Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo!



**Habari, Sisi  
ni Margo na  
Paolo!**



Tunatembelea  
Jamhuri ya  
Demokrasia ya  
Kongo, au D. R.  
Congo.

## D. R. Congo

iko Afrika ya kati.  
Takriban watu  
milioni 80  
wanaishi huko.



Sehemu kubwa ya D. R. Congo imefunikwa na misitu ya mvua. Ni nyumbani  
kwa wanyama wa kuvutia wa aina  
mbalimbali, kama vile tembo, sokwe,  
na faru. Mnyama huyu anaitwa Okapi.

D. R. Congo inajulikana kwa  
utamaduni wake mzuri wa  
sanaa, ikijumuisha sanamu  
za mbao, vikapu vya  
kusukwa, na barakoa.





Katika D. R. Congo, watu wengi wanazungumza Kifaransa kanisani. Hiyo ndiyo lugha rasmi ya nchi. Lakini kuna lugha zingine takriban 250 zinazozungumzwa huko D. R. Congo!

Wamisionari kutoka kanisa letu walianza kufundisha watu katika D. R. Congo mnamo 1986. Sasa takriban watu 60,000 huko ni waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.



**Asante kwa kitalii  
D. R. Congo pamoja  
nasi. Tutaonana wakati  
mwingine!**



## **Kutana na baadhi ya rafiki zetu kutoka D. R. Congo!**



"Jumapili moja, kulikuwa na wanajeshi kila mahali na wazazi wangu walisema ilikuwa vigumu kwenda kanisani. Niliwaambia wazazi wangu kwamba tulipaswa kuhudhuria angalau mkuiano wa sakramenti. Kwa pamoja tulione-sha imani na kwenda kanisani kuitakasa siku ya Bwana."

**Prodi K., miaka 7, Kinshasa,  
Jamhuri ya Demokrasia ya  
Kongo**



"Ninapenda kuwasaidia wengine. Siku moja katika darasa langu, mtoto alikuwa na huzuni kwa sababu wakati wa mapumziko hakuwa na chochote cha kula. Nilimwendea na kushiriki naye kile nilichobeba kwa ajili ya kula."

**Célia Tshidibi K., miaka 5,  
Kinshasa, Jamhuri ya  
Demokrasia ya Kongo**

**Je, wewe unatoka D. R. Congo?  
Tuandikie! Tungependa kusikia  
kutoka kwako. Ona ukurasa wa R24.**

# Sitaki Kuwa Tofauti!



**Na Eliza Broadbent**

(Imetokana na hadithi ya kweli)

*"Thamani ya nafsi ni kubwa mbele za Mungu"*

*(Mafundisho na Maagano 18:10).*

Mika siku zote alitazamia darasa la dansi. Alipenda kusikiliza muziki. Alipenda kufanya mazoezi mruko wake wa kipepeo na kufanya hivyo kwa usahih. Na alipenda hasa wakati darasa lote lilipopiga hatua pamoja. Wakati walipofanya hivyo, ilikuwa ni kama wacheza dansi wote walikuwa wanafanana. Ilikuwa ni kama hakuwa pekee mwenye Down syndrome.

Leo walikuwa wakijifunza hatua mpya ya dansi. Mika alimtazama mwalimu wake akiruka hewani. Aliwatazama wasichana wengine wakijaribu. Baadhi walipatia mara moja. Baadhi walijaribu mara kadhaa. Mika alijaribu tena na tena, lakini hakuweza kupatia.

"Unaweza kunisaidia, mwalimu?" Mika aliuliza.

Msichana pembeni yake alimtazama Mika. Kisha akamgeukia rafiki yake aliyekuwa pembeni. "Kwa nini anazungumza hivyo?" alinong'ona. Wasichana wote



wawili waligeuka na kumtazama Mika.

Njiani kuelekea nyumbani baada ya darasa, Mika alikuwa kimya njia nzima.

Walipofika nyumbani, Mama alikuwa akikanda kinyanya jikoni. Alikuwa na unga kwenye shavu. Wakati mwingine hilo lilimfanya Mikaacheke. Lakini leo alidondosha tu mkoba wake sakafuni na kuzama ndani ya kiti mezani.

“Dansi ilikuwaje?” Mama aliuliza.

“Mbaya,” Mika alisema. “Niliomba kusaidiwa, na msichana akasema nazungumza vya kuchekesha. Kisha akanitazama kwa mshangao.” Mika alitazama chini. “Sitaki kwenda tena kwenye dansi.”

“Jamani, Mikal!” Mama alisema. “Pole. Mimi na baba tunapenda kukutazama ukidansi. Tunaona fahari kwa juhudu yako kubwa!”

Mika alihisi machozi yakimlenga. “Sipendi Down syndrome ndani yangu. Sipendi kwamba uso wangu uko tofauti. Natamani isingekuwa vigumu kwangu kuifunza mambo mapya. Napaswa kufanyia mazoezi hata kuzungumza!”

Baba aliketi pembedi ya Mika na kuweka mkono wake kumzunguka. “Mika, tunakupenda *sana*. Hatungeweza kubadili kitu kimoja kuhusu wewe.”

Lakini Mika alitikisa tu kichwa chake na kuficha uso wake kwa mikono yake. “Sitaki kuwa tofauti. Nataka Down syndrome yangu iondolewe kwangu!”

Mama na Baba walikuwa kimya kwa muda.

“Nina wazo,” Mama alisema. Mika alichungulia kupitia upenyo wa mikono yake. “Kwa nini usiombe na kumuuliza Baba wa Mbinguni jinsi *Yeye* anavyohisi kuhusu wewe?”

Mika alifikiria kuhusu hilo. Alipenda kuomba. Taratibu, alikubali kwa kichwa. “Unaweza kuandika swalii ili niweze kukumbuka nini cha kuomba?”

Mama aliandika swalii. Kisha Mika alichukua karatasi na kwenda chumbani kwake kuomba.

Wakati aliporudi jikoni dakika chache baadaye, uso wa Mika ulikuwa uking’aa kama mwanga wa balbu. “Baba wa Mbinguni amejibu!” alisema.

“Amesema nini?” Mama aliuliza.

“Amesema, Mika, nakupenda jinsi ulivyo,” Mika alisema. “Na *Yeye* amesema hivyo kwa sauti KUBWA!”

Wiki iliyofuata kwenye dansi, Mika hakuhofia kile wasichana wengine walichofikiria kuhusu Down syndrome yake. Badala yake, alimwona msichana mwingine, Sara, ambaye alionekana mwenye huzuni. Sara alikuwa na wakati mgumu kujifunza hatua mpya pia.

Mika aliporudi nyumbani, aliamua kumuandikia Sara ujumbe. Alichora picha nyingi za moyo. Mama alimsaidia kwenye matamshi.

“Mpendwa Sara,” Mika aliandika. “Wewe ni mcheza dansi mzuri. Ninataka kuwa rafiki yako. Ninafurahi upo kwenye darasa langu la dansi.”

Mika hakutaka kucheleva kumpa Sara ujumbe. Alitaka Sara ahisi furaha na kupendwa kwenye dansi pia. ●  
*Mwandishi anaishi Utah, Marekani.*



# Mzee Stevenson Anazuru Chile



Mitume wanasaferi kote ulimwenguni kuwahudumia watu na kuwafundisha kuhusu Yesu Kristo.

Mzee Gary E. Stevenson na Dada Lesa Stevenson walisafiri pamoja na Rais Russell M. Nelson na Dada Wendy Nelson kwenda Chile kwa ajili ya tukio muhimu sana. Hekalu jipya lilikuwa likiwekwa wakfu katika jiji la Concepción!

Hekalu hili jipya la kupendeza ni la pili kujengwa Chile na ni hekalu la 18 katika Amerika ya Kusini.



Watoto walikuja na wazazi wao kumsikiliza Rais Nelson akitoa sala maalumu kuweka wakfu hekalu.

Laura na Alicia O. walisaidia kuweka jiwe la mwisho nje ya hekalu. Hili linaitwa jiwe la pembeni la hekalu. Hatimaye hekalu lilikuwa tayari kuwekwa wakfu.

Matetemeko mengi hutoka Chile. Hekalu la Concepción Chile lina msingi maalumu kulilinda kuto kana na uharibifu ikiwa tetemeko litapiga.

“Leo imekuwa bila shaka na hisia ya mbinguni.”

Sasa waumini wenye kustahili wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwishiwanaweza kuingia ndani ili kuunganishwa na familia zao na kutumikia kwa kufanya ubatizo wa hekaluni!

# Mzee Renlund Anawatembelea Watoto

Mzee Dale C. Renlund anatembelea sehemu nyingi akiwa na mke wake, Dada Ruth L. Renlund, kuwasaidia watu kuji-funza kuhusu Yesu Kristo. Anatoa hotuba na kuzungumza na wamisionari. Lakini popote anapokwenda, jambo analolipenda zaidi ni kukutana na kusalimiana kwa mkono na watoto. Wakati mwagine huwatembelea hata katika Msingi!



Huko Bolivia

Huko Japani



Huko Peru



Huko Korea ya Kusini

“Je, unataka kujua siri? The *Friend* ni jarida la Kanisa ninalolipenda zaidi. Mara zote ninalisoma kwanza!”



Mzee Renlund anataka watoto kila mahali wajue kwamba Baba wa Mbinguni anawajua na anawapenda.

# Kofia Nyeupe kwa ajili ya Florence

**Na Jordan Monson Wright**

(Imetokana na hadithi ya kweli)

Florence Onyekwe mwenye miaka kumi na tatu alifika kwenye sehemu yake ya kawaida ndani ya soko lenye watu wengi huko Onitsha, Nigeria. Mtaa ulikuwa umejaa wachuuzi wakiwaita wanunuzi wenye shughuli nyingi. Wanawake wakiwa na mizigo iliyokaa vizuri bila kushikiliwa vichwani wakati wakitembea. Shule ilikuwa imefungwa kwa ajili ya likizo, na Florence alijua rafiki zake walikuwa wakifurahia mapumziko. Lakini Florence alitumia likizo yake kwa kuuza majani machungu hapa sokoni. Ilikuwa ndiyo njia pekee ya kupata fedha kwa ajili ya ada yake ya shule.

Florence hata hivyo hakulalamika. Hata hivyo, mama yake alitumia masaa mengi sokoni kila siku aki-  
enza viazi vitamu ili



kununua chakula kwa ajili ya familia. Mama alifanya kazi kwa bidii kubwa. Wazazi wake wote walifanya hivyo. Lakini bila elimu ya kutosha, kuli-kuwa tu na mengi wangeweza kufanya. Florence alikuwa karibu kumaliza elimu yake ya msingi. Pengine ikiwa angeendelea na shule, angeweza kupata kazi ambayo ingemlipa vizuri na kusaidia familia yake.

Wakati aliporudi nyumbani, Florence aliwakuta waza-zi wake na kuwaaliza, "Je, mnadhani ningeweza kwenda shule ya sekondari? Na labda chuo kikuu?"

Mama alimtazama Nnam (baba) na kutikisa kichwa chake. "Chuo Kikuu kinahitaji pesa nyingi kuliko kiasi tulichonacho," alisema Nnam. Florence alitazama chini kwenye viatu vyake. Hakutaka Mama na Nnam kuona jinsi alivyokatishwa tamaa.

Siku chache baadaye, Florence alipita hospitali kuchukua dawa. Hospitali ilikuwa na shughuli nyingi kama vile sokoni, japokuwa hazikuwa na kelele. Florence alikodolea macho wauguzi waliovaa kofia ngumu, nyeupe.

Alijiona mwenyewe ndani ya sare kama ile, akiwasaidia wagonjwa na kuwashughulikia watoto katika hospitali kubwa. Pengine yeye angeweza kuwa muuguzi.



Florence alijua wazazi wake walikuwa sahihi—kupata elimu kungekuwa vigumu. Lakini Florence alijua jinsi ya kufanya kazi kwa bidii. Aliamua kujaribu.

Licha ya shughuli nyingi zilizojaza siku yake, Florence alitenga muda wa kusoma. Alifaalu majaribio ya shule ya sekondari, na Nnam alikopa pesa za kutosha kwa ajili yake kwenda. Baadaye alikuta kwamba serikali ingesaidia kulipia shule ya uuguzi. Ndoto zake ziliikuwa zinaweza kufikika!

Lakini ilipofika wakati wa kuanza shule ya uuguzi, Florence alihisi shaka kidogo. Vipi kama ingekuwa ngumu sana? Vipi kama angekuwa mpweke? Florence alinamisha kichwa na kuomba, "Mungu Mpendwa, tafadhal ni pe nguvu za kwenda shule ya uuguzi na kufanya kazi kwa bidii."

Kwenye shule ya uuguzi, Florence alijifunza jinsi ya kutoa dawa na kuweka vifaa safi kutokana na bakteria. Wakati mwengine wagonjwa wake walipata nafuu, lakini wakati mwengine hawakupata nafuu. Florence aliomba mara kwa mara kwa ajili ya ujasiri. Baada ya miaka mitatu mirefu, Florence alihitimu akipata zawadi ya mwanafunzi bora katika darasa lake. Ndoto yake ilikuwa imetimia! Alipaswa kuva kofia nyeupe ya uuguzi, *na* aliweza kupata kipato cha kutosha kuisaida familia yake.

Miaka mingi baadaye, Florence alizuru tawi dogo huko misheni ya Ghana Accra. Mume wake, Christopher Chukwurah, alikuwa rais wa misheni huko. Florence alikutana na baadhi ya watoto katika tawi lake ambao



mara zote hawakwenda shule. Hawakuwa na uhakika nini cha kufanya kwa ajili ya wakati wao ujao. Walimkumbusha Florence kuhusu yeye wakati alipokuwa mtoto. "Nini ninaweza kusema ili kuwasaidia?" Florence alionomba kimya kimya.

Kisha akahisi msukumo dhahiri: Waambie kuhusu maisha yako.

Florence alifikiria kuhusu maisha yake. Alikuwa amefanya kazi hospitalini huko Nigeria na Marekani. Alikuwa ameolewa na mwanaume mzuri, na kwa pamoja walikuwa wamepata Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Alikuwa amekuwa mama. Sasa alikuwa akiwasaidia wamisionari kuwa wenye afya na kufanya kazi kwa bidii. Baba wa Mbinguni alikuwa amemsaidia kuwa muuguzi. Alimwezesha kufanya mengi zaidi ya alivyofikiria. Angeweza kufanya vivyo hivyo kwa watoto hawa.

Florence aliwaangalia watoto na kutabasamu. "Unajua zile kofia nyeupe ambazo wauguzi huva? Niliona kofia kama ile na kuamua kuwa muuguzi . . ." ●

*Mwandishi anaishi Michigan, Marekani.*



Picha hii inamuonyesha  
Florence wakati hatimaye  
alipopata kofia yake  
mwenyewe nyeupe.





**Na Brooklyn P., miaka 9, Utah,  
Marekani**

**M**waka uliopita nilichukua kitabu katika maktaba kuhusu msichana ambaye alianzisha blogu. Nilidhani kingekuwa kitabu cha kufurahisha kwa sababu mhusika mkuu alikuwa na umri sawa na mimi, na mama yangu ni mwana blogu. Hivyo nilidhani kingekuwa kitabu ambacho ningeweza kujihusisha nacho.

Nilikuwa nimesoma kurasa chache tu za kitabu wakati msichana alipolitaja bure jina la Bwana. Sikupata hisia nzuri za ndani baada ya kusoma sehemu ile. Lakini nilindelea kusoma, nikitumaini lilikuwa jambo la mara moja tu. Nilisoma kurasa zingine kadhaa, na alilitaja tena.

Nilikwenda na kumwambia mama yangu kuhusu kile nilichopata. Sikujua ikiwa ninapaswa kuendelea kusoma au la. Mama yangu aliniambia uchaguzi ulikuwa wangu. Lakini alikubali pengine halikuwa jambo zuri kuendelea kusoma kama msichana alisema mambo ambayo tulijua

ni mabaya. Mama yangu alisema kwamba haikuwa vizuri hasa kama msichana alikuwa akilitaja bure jina la Bwana.

Nilifikiria nitaona ikiwa lingetokea zaidi, hivyo nilisoma kitabu juujuu. Nilikuta kwamba kulitaja bure jina la Bwana ilikuwa ni jinsi msichana alivyokuwa akizungumza mara kwa mara. Niliamua kurudisha kitabu maktaba bila kukisoma zaidi.

Nilihisi huzuni kwamba mwandishi wa kitabu alilitaja bure jina la Bwana. Lakini baada ya kurudisha kitabu maktaba, nilihisi furaha kwamba nilifanya uchaguzi sahihi. Najua nilikuwa nikifuata “Viwango vyangu vya Injili kutoka kwenye kitabu changu cha *Imani kwa Mungu* ambacho kinasema, “Nitasoma na kutazama tu mambo ambayo yanampendeza Baba wa Mbinguni. Ninajua tunapaswa tu kutumia majina ya Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo kwa unyenyekevu na kwa heshima. ●

## Je, Ninapaswa Kuendelea Kusoma?



# Nayaweza mambo yote katika Kristo, anitiaye nguvu

(ona Wafiliipi 4:13).





**Na Dada**  
**Joy D. Jones**  
Rais Mkuu wa  
Msingi

# Changamoto ya Hekalu



*"Mioyo ya watoto itawageukia baba zao" (Mafundisho na Maagano 2:2).*

Jumapili moja mimi na washauri wangu tulizuru mkuu tano wa Kanisa. Tulitoa mahubiri kuhusu hekalu na mambo maalumu yanayotokea pale. Baada ya mkutano mvulana wa miaka 12 aliyeitwa Colby alikuja kwangu na kunisalimia kwa mkono. Tulipiga domo kuhusu hekalu. Kisha nilimpa changamoto ya kutafuta jina la familia ili kulipeleka hekaluni.

Muda mfupi baadaye, nilipata barua kutoka kwa Colby. Hapa kuna kile Colby alichoniambia:

“Nilikwenda nyumbani na kupata jina jipya. Ilitokea kwamba nilimpata babu yangu-mkuu wa tatu!

“Muda mfupi baadaye nilikwenda hekaluni na kubati-zwa kwa ajili yake. Ilikuwa kweli maalumu kwa sababu

kaka yangu aliweza kunibatiza na baba yangu aliweza kunithibitisha kwa ajili ya babu.

“Nilipata hisia nzuri za ndani ambazo zililetu amani. Nilihisi kama kile nilichofanya kwa ajili ya babu yangu kilikuwa kizuri hasa kwa sababu sasa anaweza kwenda kwenye ufalme wa celestia kuishi pamoja na familia yake. Kwa siku yote hiyo, nilikuwa na hisia nzuri sana za ndani.

“Niligundua pia kwamba hakuna anayewafahamu wazazi wa babu yangu mkuu wa tatu, hivyo ninaweza kutafuta majina yao na kuyapeleka hekaluni pia!”

Colby ni mfano mzuri kiasi gani wa kuonekana! Bila kujali una umri gani, unaweza kuwa mfano kwa familia yako na rafiki zako. Unaweza kushiriki injili na kila mtu unayemfahamu—hata mababu zako! ●

# Onyesha na Sema

Mkutano mkuu upo mwezi huu! Hapa ni kile baadhi ya watoto hufurahia kuhusu mkutano.



**N**inapenda kusikiliza hadithi na kwaya ikiimba. Ninapenda pia kusikiliza mifano wanayotoa.  
**Yuri H., miaka 8, Taoyuan, Taiwan**



**N**inapenda kumsikiliza nabii kwa sababu Bwana huzungumza kupitia yeye.  
**Andrés C., miaka 12, Valle del Cauca, Colombia**



**N**inapenda kuangalia mkutano kwa sababu ninapenda kujifunza kutoka kwa manabii, na ninapenda kutumia muda huo pamoja na familia.  
**David J., miaka 9, Sololá, Guatemala**



**Abel C. and Tina S., miaka 10 na 9, kaunti ya Bong, Liberia,** ni kaka na dada. Abel anapenda mkutano “kwa sababu huo ndio wakati tunapomuidhinisha nabii wetu kama Rais wa Kanisa kila mwaka.” Tina “anapenda wakati nabii anazungumza kuhusu mahekalu.”



**Anna B., miaka 10, Maharashtra, India,** aliangalia mkutano pamoja na mama yake. Yeye huja na shajara yake na kalamu kwenye kila mkutano ili kuandika shuhuda na jumbe anazosikia.



**David na Juliana M., miaka 4 na 6, South Holland, Netherlands,** hujaza mabakuli 15 kwa asusa na kuweka picha ya Mtume au mshiriki wa Urais wa Kwanza kwenye kila moja. Wakati mmoja wa Akina kaka anapozungumza, wanakula kile kilichomo kwenye chombo!



# Kumtumikia Bwana kwa Kihispania

**Na Jennifer Maddy**

(Imetokana na hadithi ya kweli)

**F**ikiria kwamba rafiki yako amekupa kitabu kizuri kuliko vyote ambacho amewahi kusoma. Unafunua jalada . . . na unagundua huwezi kusoma kitabu. Kimeandikwa kwa lugha tofauti! Ungefanya nini?

Katika miaka ya mwanzo ya Kanisa, Kitabu cha Mormoni kilikuwa kimechapishwa kwa Kiingereza tu. Rais Brigham Young aliwaita wamisionari wawili kuhubiri injili Mexico na kutafsiri Kitabu cha Mormoni kwa Kihispania. Lakini walihitaji msaada zaidi kufanya hilo. Walijua kidogo tu kwamba ng'ambo ya bahari, Mungu alikuwa amemuandaa mtu ambaye angewapa msaada hasa waliohitaji.


Meliton Gonzalez Trejo alitoka kwenye familia ya kitajiri huko Hispania. Alisoma kwa bidii shulen na kuwa afisa katika jeshi la Hispania. Daima alivutiwa na dini, lakini hakuna alichopata kilihi kwa sahihi. Siku moja alisikia afisa mwingine akizungumza kuhusu kundi la watu waliojiita "Watakatifu." Walikuwa waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho,

na nabii wa Mungu alikuwa amewaongoza hadi Rocky Mountains Marekani. Meliton alihisi hamu kubwa ya kukutana nao. Alijiunga na kikosi cha jeshi kilichopelekwa Ufilipino, akitumaini hii ingesaidia kumfikisha Marekani baadaye. Lakini Meliton alijikuta akiwa na shughuli nyingi kwamba kuwatemebelea Watakatifu kulianza kuonekana si muhimu sana.

Kisha Meliton akawa mgonjwa sana. Alikumbuka sababu ya kwa nini alikuwa amekuja Ufilipino na alimwomba Mungu kuhusu kile alichopaswa kufanya. Usiku ule, Meliton alipata ndoto maalumu. Alijua alipaswa kwenda kwenye Rocky Mountains.

Pale Meliton alipopona ugonjwa wake, aliendelea na safari yake kuelekea Marekani. Aliwasili California mnemo Julai 4, 1874, na kuelekea Jiji la Salt Lake.

Wakati Meliton alipofika Salt Lake, alipata tatizo: angeweza kusoma Kiingereza lakini hakuwa amewahi kukizungumza. Asingeweza kuzungumza na yeoyote! Lakini aliamua kwamba ikiwa asingeweza kuzungumza



na watu, angepata umakini wao kwa njia nyingine. Meliton alivaa sare yake ya jeshi la Hispania na kute-mbea kote katika mitaa ya jiji. Kama alivyotumaini, watu wengi walimtambua! Hatimaye alioneckana na muumini wa Kanisa aliyeitwa Kaka Blanchard, profesa wa chuo kikuu ambaye alizungumza Kihispania. Kaka Blanchard alimsaidia Meliton kupata makazi Salt Lake na kumfundisha injili. Punde Meliton alibatizwa.

Kaka Blanchard pia alimtambulisha Meliton kwa Rais Brigham Young. Meliton alimwambia Rais Brigham Young kwamba zaidi ya kitu chochote, alitaka kutafsiri Kitabu cha Mormoni kwa Kihispania.

Rais Young alimuomba Meliton kuwasaida wamisionari ambao walikuwa wanakwenda Mexico kutafsiri sehemu za Kitabu cha Mormoni kwa Kihispania. Meliton alitumia wiki nyingi kutafsiri maneno ya Kiingereza kwa Kihispania. Kila usiku alirejea tafsiri yake pamoja na wamisionari. Walizungumza Kihispania kidogo lakini walihisi tafsiri hii muhimu ilihitaji mzungumzaji mzawa wa Kihispania. Walijua Meliton alikuwa jibu la sala zao. Mnamo 1875 tafsiri ilichapishwa. Ilikuwa ikiitwa Trozos

*Selectos del Libro de Mormon* (Vifungu Vilivyochoaguliwa kutoka Kitabu cha Mormoni).

Wamisionari sasa walikuwa tayari kwenda Mexico. Walipakia nakala 1,500 za maandiko yaliyotafsiriwa juu ya farasi na kuanza safari yao. Kwa mara ya kwanza, wazungumzaji wa Kihispania waliweza kusoma Kitabu cha Mormoni kwa lugha yao wenye! Japokuwa Meliton alikuwa ameishi maelfu ya maili mbali na Hispania, Baba wa Mbinguni alimuongoza mahali ambapo alihitaji kuwa hasa. Kwa sababu ya ujasiri na imani ya Meliton, alisaidia kuleta neno la Mungu kwa watu wasio na idadi. ●

*Mwandishi anaishi Utah, Marekani.*



Meliton Gonzalez Trejo (1844–1917) alitumikia misheni kadhaa huko Mexico na kubatiza baadhi ya waumini wa kwanza wa Kanisa huko. Mnamo 1886 Meliton alisaidia kumalizia tafsiri ya Kitabu chote cha Mormoni kwa Kihispania.

# Safari za Kimisionari za Paulo

**Na Marissa Widdison**  
Majarida ya Kanisa




Baada ya Yesu kufufuka, Mtume Paulo alisafiri kwenda miji mbalimbali kuwafundisha watu kuhusu Yesu. Hakukuwa na magari wala ndege kipindi hicho, hivyo alitembea sana! Wakati mwagine alisafiri kwa mashua.




Paulo aliwafundisha watu makanisani na nyumbani.  
Alifundisha watu juu ya vilele vyta miamba na mitaa ya mji.



Watu wengi hawakupenda kile  
Paulo alichofundisha. Wakati  
mwingine Paulo alifungwa  
gerezani. Wakati mwingine  
Paulo aliugua.



Lakini katikati ya magumu haya  
yote, Paulo alikuwa na imani.  
Alisema, "Nayaweza mambo  
yote katika Kristo." Alijua Mungu  
angemsaidia kuwa imara.



Yesu Kristo anaweza kunisaidia kuwa imara pia.  
Yeye ananipenda, nami ninampenda Yeye! ●

# Yesu Anaweza Kunisaidia Kufanya Mambo Magumu



# Wapendwa Wazazi,

Mojawapo ya ujumbe muhimu wa Agano Jipywa ni kwamba tunaweza kupata amani na furaha katika Kristo, licha ya hali ya maisha yetu. Jarida la mwezi huu linashiriki ushuhuda sawa na huu.

- Kwenye ukurasa wa R4, mvulana anapata faraja baada ya kuota ndoto mbaya.
- Kwenye ukurasa wa R8, msichana mwenye Down syndrome anakumbushwa kwamba Baba wa Mbinguni anampenda.
- Kwenye ukurasa wa R15, bango linafundisha kwamba mambo yote yanawezekana kwa msaada wa Yesu Kristo.
- Kwenye ukurasa wa R20–23, Paulo anaweka mfano wa imani.

Mnaposoma jarida hili pamoja, tafuteni jinsi Yesu na Baba wa Mbinguni walivyowasaidia watu katika kila hadithi. Ungeweza kupigia mstari maneno ambayo yanaelezea changamoto walizopata. Kisha zungushia duara maneno ambayo yanaelezea usaidizi upi walipokea. Kama familia, zungumzeni kuhusu jinsi wakati mwingine majaribu yanavyoondolewa, na wakati mwingine tunavyofanywa imara kuvumilia majaribu yetu. Vyovoyote vile, Yesu na Baba wa Mbinguni wanatupenda na wapo kwa ajili yetu!

Tunatumaini mmekuwa na mwezi wenyre furaha,

*Rafiki*

## Jinsi ya Kutuma Kazi ya Sanaa ya Mtoto Wako kwe- nye Liahona

Nenda kwenye liahona.ChurchofJesusChrist.org na ubofye "Vasilisha Makala au Jibu." Au itume kwa barua pepe kwa liahona@ChurchofJesusChrist.org likiwemo jina la mtoto wako, umri, jiji la makazi, na maelezo haya ya ruhusa: "Mimi, [ingiza jina lako], natoa ruhusa kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kutumia wasilisho la mtoto wangu kwenye majarida ya Kanisa, kwenye mitandao ya Kanisa, na kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii." Tuna hamu ya kusikia kutoka kwako!



**Tafuta Liahona iliyofichwa ndani!**

## YALIYOMO

- R2** Kuwapenda Wengine kama Yesu Anavyotupenda
- R4** Umbali wa Sala Tu
- R6** Halo kutoka Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo!
- R8** Sitaki Kuwa Tofauti.
- R10** Mitume kote Ulimwenguni: Mzee Stevenson Anazuru Chile
- R11** Mitume kote Ulimwenguni: Mzee Renlund Anawatembelea Watoto
- R12** Kofia Nyeupe kwa ajili ya Florence
- R14** Je, Ninapaswa Kuendelea Kusoma?
- R15** Wazo Zuri: Nayaweza mambo yote katika Kristo
- R16** Changamoto ya Hekalu
- R17** Onyesha na Sema
- R18** Mifano ya Ujasiri: Kumtumikia Bwana kwa Kihispania
- R20** Hadithi za Maandiko: Safari za Umisionari za Paulo
- R23** Ukurasa wa Kupaka Rangi: Yesu Anaweza Kunisiaidia Kufanya Mambo Magumu